# Achilieni Wachungaji Wangu Waende!

## Sababu ya Yesu Kukawisha Marejeo Yake

**Na Wesley McDonald**

**wesmcdonald@live.com**

**wesmcdonald7@gmail.com**

**Kitabu hiki hakiwezi kunakiliwa au kuchapishwa tena bila idhini ya mwandishi, Wesley McDonald.**

**Nenda kwa letmypastorsgo.com usome mtandaoni au upakue nakala za pdf za kitabu hiki bure.**

Picha hii ilitolewa katika kitabu kiitwacho, Pointed Pen Parables
Robert M Eldridge, *Pointed Pen Parables:*(Nashville, TN: Southern Publishing Association, 1968,) 30
Used by permission: Review and Herald Publishing Association, Silver Spring, MD

Image edited by Clay Doss

# Yaliyomo

**Yaliyomo** .......... 2
**Shukrani** .......... 4
**Uidhinishaji** .......... 5
**Sura ya 1** .......... 6
**Toleo Fupi –** .......... 6
**Mada Muhimu zaidi Kwanza** .......... 6
  **Jambo moja ambalo sote hukosea.** .......... 6
  **Maswali ya Kuzingatia** .......... 7
**Sura ya 2** .......... 8
**Njia Zetu Zinalinganaje na Njia za Mungu?** .......... 8
  **Swali: Je, hata inawezekana kwetu sisi kuharakisha au kukawisha ujio wa Kristo?** .......... 8
  **Maswali ya kuzingatia** .......... 10
**Sura ya 3** .......... 11
**Kumaliza Mpango wa Siri wa Mungu** .......... 11
  **Maelezo ya Kusudi la Sura ya Tatu** .......... 11
  **Malaika wa Saba: Onyo la Mwisho la Mungu kwa Wanadamu** .......... 11
  **Tarumbeta ya Saba: Mpango wa Siri wa Mungu** .......... 12
  **Maswali ya Kuzingatia** .......... 18
**Sura ya 4** .......... 19
**LAKINI – "ameweka siku . . ."** .......... 19
  **Maswali ya Kuzingatia** .......... 23
**Sura ya 5** .......... 24
**Ni Wangapi Watapotea Ikiwa …?** .......... 24
  **Usalama: Fikiria hali ifuatayo.** .......... 24
  **Maswali ya Kuzingatia** .......... 26
**Sura ya 6** .......... 27
**Majukumu ya Washiriki na Wachungaji** .......... 27
  **Maswali ya Kuzingatia** .......... 31
**Sura ya 7** .......... 32
**Ni Nani Atatoa Huduma ya Uchungaji kwa Makanisa Yaliyopo?** .......... 32
  **Maswali ya Kuzingatia** .......... 37

**Sura ya 8** ........ 38
**Asili ya Mfumo wa Huduma wa Kiprotestanti** ........ 38
**Kaskazini mwa Marekani – Kulinganisha Viwango vya Ukuaji wa Makanisa na Washiriki, kutoka mwaka wa 1863 hadi 1932, na kutoka 1932 hadi 2017.** ........ 41
**Maswali ya Kuzingatia** ........ 43
**Sura ya 9** ........ 44
**Athari ya Kutotumia Mfumo Asili wa Kiadventista katika Uinjilisti** ........ 44
**Mawazo ya Kitume, Waadventista wa Awali** ........ 45
**Kuangalia hatua 6 zinazohusika katika kuachana na mfumo wa huduma wa Biblia hadi tulipo sasa** ........ 47
**Maswali ya Kuzingatia** ........ 52
**Sura ya 10** ........ 53
**Mfumo wa Biblia – Usimamizi wa Kanisa la Nyanjani Leo** ........ 53
**Hapa kuna swali unahitaji kujibu.** ........ 55
**Sura ya 11** ........ 56
**Mfumo wa Biblia – Uchungaji wa Kitaaluma Leo** ........ 56
**Huduma ya Yesu Duniani** ........ 57
**Huduma ya Mtume Paulo** ........ 60
**The Adventist Pioneers' Ministry** ........ 65
**Sura ya 12** ........ 66
**Mfumo wa Biblia – Huduma ya Wasioajiriwa** ........ 66
**Ushiriki wa Kila Mshiriki** ........ 68
**Sura ya 13** ........ 70
**Mpango wa Mungu Bado Unafanya Kazi Leo** ........ 70
**Ulinganisho wa Ukanda wa Magharibi na Divisheni** ........ 71
**Ulinganisho wa Bara la Afrika na Divisheni** ........ 72
**Mifano miwili inayotosha kuzingatiwa** ........ 73
**Misheni ya Mongolia** ........ 73
**Eneo la Magharibi mwa Kenya – Mradi wa Elimu** ........ 73
**Mpango wa Mungu Hujabadilika** ........ 74
**Sura ya 14** ........ 74
**Wingu Kubwa Zaidi la Mashahidi** ........ 75

# Shukrani

Ningependa kutambua baadhi ya wale ambao wamenitia moyo, kunisaidia na kuniombea nilipokuwa nikiandika kitabu hiki. Nasema baadhi yao, yamkini kwa sababu siwezi kuwakumbuka wote ambao wamehusika.

- Yesu, Mwokozi wangu, aliyenitunuku fursa ya kuweza kutoa fundisho hili. Alinipitisha katika tajriba mbalimbali, nyingine zenye machungu na nyingine za furaha. Bila aina hizo mbili za tajriba, Kamwe singepata uzoefu wa maisha unaohitajika ili kuandika kitabu kama hiki.
- Familia yangu. Linda, mke wangu ambaye amekuwa kando yangu kwa miaka 45. Binti yangu Sabra Johnson na mume wake Nick Johnson.
- C.J. Doss. C.J. alivutiwa na Mungu kuniundia tovuti na mchoro wa jalada la kitabu change pasipo hata bila ya mimi kuulizia. Shukrani nyingi zimwendee.
- Baadhi ya wafanyikazi wa kanisa ambao wamekuwa wa msaada katika uandishi wa kitabu.
    - Justin Lawman, Rais wa Eneo Jipya la Kaskazini Kusini mwa Wales, Australia. Mchungaji Mkuu wa sasa wa Kanibera, Australia.
    - Paul Geelan, Katibu Mkuu, Eneo Jipya la Kaskazini Kusini mwa Wales, Australia.
    - Gary Blanchard, Mkurugenzi wa Vijana, Ukanda Mkuu wa Waadventista wa Sabato.
    - Lucian Cristescu, Mkurugenzi wa Mahubiri wa zamani, Ukanda wa Romania.
    - Vadim Butov, Rais wa zamani, Eneo la Volga, Urusi. Mwinjilisti wa sasa wa kimaeneo katika Eneo la Viktoria, Australia.
    - Jose Cortes, Sr., Rais wa zamana, Eneo la New Jersey.
    - Reginald Sibanda, Mkurugenzi wa Uinjilisti wa zamani, Divisheni ya Afrika Kusini-Bahari ya Indi.
    - Jerome Davis, Rais wa zamani, Eneo la Baharini.
    - Dkt. P. Gerard Damsteegt, Profesa wa muda mrefu katika Chuo Kikuu cha Andrews, na mwandishi wa *Je, Waadventista Wametupilia Mbali Mfano wa Biblia wa Uongozi wa Kanisa?*
    - Peter Roenfeldt, Katibu mstaafa wa Mahubiri katika Divisheni ya Ulaya,, Tovuti yake sasa - http://www.newchurchlife.com/
    - David Klinedinst, Mwinjilisti, Eneo la Chesapeake.
    - James DieuJuste, mchungaji na mwalimu, kwa sasa akitumika katika Eneo la Kaskazini Mashariki.
    - Michael Horton, Mkurugenzi wa Mahubiri, Eneo la Baharini.
    - Joel Bohannon, Mchungaji, Eneo la Baharini.
    - Na wengine.

# Uidhinishaji

"Nimemfahamu Wes McDonald kwa miaka mingi, nikisikiliza semina zake. Nilimpa nafasi ya kuwazungumzia wachungaji na washiriki wangu nilipokuwa nikifanya kazi kama rais wa eneo nchini Urusi. Aliwazungumzia washiriki wangu na kupanua mtazamo wetu wa kanisa la usoni. Sasa kwa kuwa kitabu chake kimefika nina furaha. Wes anatoa jawabu-tendi kuhusu uhuishaji na urekebishaji wa kanisa letu kama kanisa la nyumbani na kimataifa. Anaturejesha kwenye msingi wa siri za zamani za kanisa letu kuhusu ukuaji na ufanisi. Anapigia debe njozi ya kweli ya Agano Jipya kuhusu huduma ya kitaaluma na kuhusika kwa kila mshiriki katika kuitangaza Injili kote ulimwenguni. Sasa wakati umewadia wa kuleta mabadiliko ya kujitosheleza katika ulimwengu wa Magharibi, ambayo hayawategemei wachungaji. Kitabu hiki ni cha lazima kusomwa na mtu yeyote ambaye ambaye anataka Yesu aje upesi."

Mchungaji Vadim Butov, mwinjilisti wa Eneo la Viktoria, Australia

"Mwinjilisti Wesley McDonald ni mchungaji/mhubiri ambaye Mungu ametumia kuwaleta wengi katika Ufalme wake. Amefunza na kuihubiri habari njema kote ulimwenguni. Semina zake zimekuwa na mafunzo kemkem katika kuwasaidia wachungaji na wainjilisti kuimarika katika kuwaongoza waume kwa wake kwa Kristo. Utapata msukumo unapojifunza kuwa zana kubwa mikononi mwa Mwenyezi."

Jerome L. Davis, Rais Mstaafu wa Eneo la Baharini la Waadventista wa Sabato.

"Wes McDonald ameandika kitabu kidogo cha nguvu sana na cha muhimu kabisa kwa wakati ambao tunaishi. Kila Mchungaji, kiongozi wa kanisa na wainjilisti watafanya vyema wakichukua muda wao kukisoma. Kanuni anazosisitiza, ni sawia na maono waliyokuwa nayo watangulizi wetu walikuwa nayo kwa kanisa la Mungu kusonga mbele na kuieneza Injili kote ulimwenguni. Ninaamini kuwa kijitabu hiki kiliandikwa 'Kwa wakati kama huu."

Linda Chodak, Shemasi, Kanisa la Waadventista wa Sabato la Sheboygan, Wisconsin.

# Sura ya 1

## Toleo Fupi –
## Mada Muhimu zaidi Kwanza

Mara kwa mara huwa nina fursa ya kutoa mafunzo yanayosisitiza umuhimu wa kupanda makanisa katika maeneo ambayo hayajawahi kuwa na kanisa la Waadventista. Katika ziara zangu, wakati mwingine nimehojiwa kuhusu yale ninayoangazia katika semina zangu. Ikiwa hakuna muda wa kutosha, kuna toleo fupi ambalo huwa natoa kuangazia hoja muhimu. Kwa sababu huenda wewe na mimi hatufahamiani, na sijui kiwango chako cha mvuto, una muda kiasi gani, au ikiwa utamaliza kusoma kitabu hiki, ningependa wewe pia uwe na aina hiyo ya jibu fupi kabla ya kuendelea kusoma kitabu chote. Ningependa kwanza uwe na toleo fupi.

### Jambo moja ambalo sote hukosea.

Karibu Wakristo wote, wakiwemo Waadventista wa Sabato, wanakosea kabisa katika kufanya jambo moja. Wakristu wa imani zote husema kuwa lengo lao kuu ni kuuangazia ulimwengu kuhusu wokovu katika Yesu. Wanataka Kuwaokoa wenye dhambi waliopotea haraka iwezekanavyo. La kusikitisha, makanisa mengi yanashikilia kuwa wachungaji, ambao hususan wameitwa na Mungu kuuhubiri ulimwengu habari njema, watumie muda wao kila wikendi kuwahubiria washiriki ambao tayari wanamjua Yesu. Aidha, wachungaji hawa wanatarajiwa kuendesha mikutano mingine mingi ya kila aina, halfa za kijamii, maadhimisho na mapatano. Wao huendesha shughuli za kanisa na bodi za shule; na mara kwa mara huwatembelea washiriki ambao tayari wana uhusiano na Yesu. Orodha ya matarajio ya washiriki kwa wachungaji ni ndefu sana.

Wakati uo huo, mamilioni ya watu kote ulimwenguni kamwe hawapati kusikia kuwa Yesu alikufa ili wapate ondoleo la dhambi, na wanaishia kushushwa makaburini bila wokovu. Ukristo wa sasa hauelekezi rasilimali zake kimsingi katika utume wa Yesu. Katika baadhi ya maeneo ulimwenguni, kanisa limegeuka kujitumikia, huku likitumia asilimia ndogo tu ya wakati kila mwaka kuwaokoa waliopotea. Katika hali zingine, washiriki kanisani ndio wanaofaidika na matoleo yao ya zaka na sadaka. Ingawa washiriki hurudisha zaka na sadaka kwa hamu ya kuzitumia kuwaelimisha wasiolifahamu Neno, wao hawatambui kuwa madai na mahitaji yao kwa mchungaji yanazuia hiyo kazi kufanyika. Hawafahamu kuwa kwa kutumia muda wa mchungaji, wanamfanya mchungaji kuwatumikia wao wenyewe, huku waliopotea wakibakia wapotovu.

Sasa kwa kuwa umesoma toleo fupi kwanza, ninaomba kuwa uendelee kusoma sehemu iliyobakia. Nataka upate kufahamu historia ya namna tulivyojipata katika tatizo hili, kile ambacho Mungu anataka tufanye, na namna ya kutekeleza kazi tuliyoitiwa kwa ufanisi zaidi. Kwa kufanya kazi kulingana na mapenzi ya Mungu na kwa nguvu za Roho Mtakatifu, tunaweza kuharakisha ujio wa Yesu mara ya pili.

## Maswali ya Kuzingatia

1. Je, kazi aliyotuitia Yesu ina umuhumi gani kwangu?

2. Je, ninafanya nini kusaidia kueneza habari njema? (Mathayo 24:14)?

3. Je, ninatarajia nini kutoka kwa mhudumu/mhubiri/mchungaji wangu?

4. Je, mahitaji yangu ya kiroho yanawezaje kushughulikiwa kwa kumtegemea Mungu badala ya kumtegemea mhudumu/mhubiri/mchungaji wangu?

# Sura ya 2

## Njia Zetu Zinalinganaje na Njia za Mungu?

Je, sisi kama Waadventista wa Sabato, tunafananishaje mtindo wetu wa sasa wa huduma na mtindo uliotumiwa na kanisa la kwanza katika siku za mitume? Je, kazi ya mhubiri wa sasa, inafananaje na ya mtume Paulo, ambaye ni kielelezo cha wahubiri? Je, wahubiri wa Kiadventista leo wanafanya kazi sawa na ile iliyofanywa na wahubiri Waadventista  katika miaka ya 1800? Ingawa tuna kanuni zilizo sahihi, je, inawezekana mbinu za uinjilisti tunazotumia sasa zikawa ni kizuizi katika kutangazwa kwa Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa ulimwengu wote? Je, yawezekana tunakawisha kurudi ka Kristo badala ya kuharakisha kurudi kwake?

### Swali: Je, hata inawezekana kwetu sisi kuharakisha au kukawisha ujio wa Kristo?

Ellen White aliandika katika *Tumaini la Vizazi Vyote,* (toleo la 1898) ukurasa wa 633, "Mungu ameteua siku, ambayo atauhukumu ulimwengu.' *Matendo ya Mitume 17:31*. Kristo anatuambia ni lini siku hiyo itawadia. Hasemi kuwa ulimwengu wote utaokolewa, lakini kwamba 'Habari hii ya ufalme itahubiriwa kwa ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; na hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.' **Kwa kuipeleka injili ulimwenguni, uwezo uko kwetu wa kuharakisha kurudi kwa Bwana wetu.** Hatupaswi tu kutazamia bali pia kuharakisha ujio wa siku ya Mungu. 2 Petro 3:12. Laiti kanisa la Kristo lingefanya kazi lililoteuliwa na Kristo kufanya, ulimwengu wote ungekuwa kabla ya sasa umeonywa, na Bwana Yesu angekuwa amekuja duniani kwa nguvu na utukufu mkubwa."[1]

Ikiwa kanisa la Kristo lingefanya kazi yake kama lilivyoamriwa na Kristo, Kristo angerejea kabla ya 1898. Zaidi ya karne moja imepita tangu 1898. Je, ni nini ambacho hatujakuwa tukifanya kama Kristo alivyotuagiza? Je, ni vipi tumekosea? Katika kitabu *Elimu*, Ellen White anafafanua ulimwengu kama 'nyumba ya wenye ukoma'. Hapa ndipo wenye ukoma waliishi na kupokea matibabu. Ukoma ni mojawapo ya magonjwa yaliyojulikana kumtisha mwanadamu zaidi, na "nyumba za wenye ukoma" zilikuwa mahali mlimojaa dhiki kuu. Ellen White anaandika kuhusu huruma za Mungu na hamu ya kumaliza masumbuko hayo. Katika ukurasa wa 264 aliandika, "Roho wake 'hutuombea kwa kuugua kusikoelezeka'. Kama maumbile yote yanayvougua  na kusumbuka kwa uchungu pamoja." (Warumi 8:26, 22), moyo wa Baba wa milele huumia kwa huruma. Ulimwengu wetu ni nyumba kubwa ya ukoma, onyesho la mateso ambayo  hata haturuhusu mawazo yetu kutafakari. Ikiwa tungeitambua hali hii kama ilivyo, mzigo wetu ungekuwa mkuu zaidi. Walakini Mungu ameubeba wote. Ili kuangamizwa dhambi na matokeo yake alimtoa Mwanawe Mpendwa, **na ametupa hayo mamlaka kwa ushirikiano naye, kuleta mateso haya kwa kikomo chake. 'Tena Habari Njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."**[2]

---

[1] Ellen White, *Tumaini la Vizazi Vyote*: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1898,) 633.

[2] Ellen White, *Elimu*: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1903,) 263-264.

Je, Kristo angerejea upesi namna gani baada ya 1844, ikiwa "kanisa la Kristo lingewajibikia kazi lililopewa na Bwana"?[3] Mnamo 1884, hususan miaka 40 baada ya 1844, ujumbe ufuatao kutoka kwa Ellen White ulichapishwa katika kitabu , *Roho ya Unabii*, *Toleo la 4*, ukurasa 291-292. Ujumbe ulichapishwa tena katika *Pambano Kuu,* ukurasa 457-458.

"Historia ya Israeli ya kale ni mfano maridhawa wa tajriba ya zamani ya Waadventista. Mungu aliwaongoza watu wake katika Harakati za Kiadventista, kama vile alivyowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri. Katika masikitiko makuu, imani yao ilijaribiwa kama ile ya Waebrania kwenye Bahari ya Shamu. Ikiwa wangezidi kutumaini mkono uliokuwa ukiwaongoza hapo mwanzo, wangeuona wokovu wa Mungu. Ikiwa wote waliounganika kutenda kazi 1844 wangeupokea ujumbe wa malaika wa tatu na kutangaza kwa nguvu za Roho Mtakatifu, Bwana angeunganika na juhudi zao kwa njia ya ajabu. Mafuriko ya nuru yangeangaziwa ulimwengu. **Miaka mingi iliyopita wenyeji wa dunia wangeonywa, kazi ya kufunga ulimwengu kukamilika, na Kristo angekuja kwa ukombozi wa watu wake.**

**"Haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba Israeli wazunguke jangwani kwa miaka arobaini; alitamani kuwaongoza moja kwa moja hadi nchi ya Kanaani, na kuwaweka huko, watu watakatifu wenye furaha**. Lakini 'hawangeweza kuingia kwa sababu ya kutoamini.' [Waebrania 3:19.] Kwa sababu ya anguko lao na kuasi imani, waliangamia jangwani, na wengine wakainuliwa kuingia katika nchi ya ahadi. **Vivyo hivyo, haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba kuja kwa Kristo kukawie sana, wala watu wake kubakia katika ulimwengu huu waa dhambi na huzuni kwa miaka mingi.** Lakini kutokuamini kuliwatenganisha na Mungu. Kadiri walivyokataa kufanya kazi waliyoitiwa, ndivyo wengine walivyoinuliwa kuutangaza ujumbe. Kwa huruma kwa ulimwengu, Yesu anakawisha kuja kwake, ili wenye dhambi wapate nafasi ya kusikia onyo hilo, na kupata kujificha ndani yake kabla ya ghadhabu ya Mungu kumwagwa"[4]

**"Miaka mingi iliyopita wenyeji wa dunia wangekuwa wameonywa, kazi ya kufungua historia ya ulimwengu kukamilika, na Kristo angekuwa amekuja kwa ukombozi wa watu wake."[5] EGW – chapisho la 1884.**

Hapa kuna taarifa ya kusisimua kutoka kwa Ellen White katika *Christ's Object Lessons,* ukurasa wa 373 na 374, "Kila mwaka mamilioni ya watu mamilioni ya roho za watu wanapata kwenye uzima wa milele bila maonyo na bila kuokolewa. Saa hadi saa katika maisha yetu tofauti, fursa za kufikia na kuokoa roho za watu hufunguliwa kwetu. Hizi fursa zinaendelea kuja na kuondoka. Mungu angependa tuzitumie vizuri. Siku, wiki, na miezi inapita; tumepungukiwa na siku moja, wiki moja, na mwezi mmoja, katika kufanya kazi yetu. Ikizidi sana pengine miaka

---

[3] Ibid.

[4] Ellen White, *Roho ya Unabii,* Vol. 4: (Battle Creek, MI: Seventh-day Adventist Publishing Association, 1884,) 291–292.

[5] Ibid.

michache tu, na sauti ambayo hatuwezi kataa kujibu itasikika ikisema, "Toa hesabu ya uwakili wako"[6]

Hapa kuna kitu muhimu kutoka kwa Ellen White katika Barua ya 110, iliyoandikwa 1902, zaidi ya miaka 100 iliyopita. "Kama watu, tunadai kuwa tunatoa ujumbe wa malaika wa tatu kwa ulimwengu … inasikitisha kiasi gani kwamba tangazo hili bado halijaanza katika maeneo mengi! Kwa miaka mingi Bwana ameweka mbele ya watu wake umuhimu wa kuingia katika maeneo mapya. Laiti Mungu angefanya hii kazi! Laiti angehuisha na kuwapa nguvu wafu, mifupa mikavu ya nyumba ya Israeli, kwa kumwaga Roho Mtakatifu juu ya watu wake!"[7]

Kitabu hiki kimeandikwa ili kutusaidia kufahamu:

1. Sababu ya kukawia kwa marejeo ya Kristo tangu 1844
2. Namna tumeshindwa kufuata maagizo ya Kristo kwa kanisa
3. Tunachostahili kufanya, kutubu na kuharakisha ujio wa Yesu
4. Namna ya kufuata maelekezi maalum ya Mungu, kufikia kila sehemu ya ulimwengu na Ujumbe wa Malaika wa Tatu haraka kuliko tulivyowahi kudhani

*Wafilipi 4:13*, "Nayaweza yote katika Yeye anitiaye nguvu."

Mungu atusaidie kutubu, kufanya mabadiliko yanayohitajika sana, kuharakisha ujio wa Yesu, na bado kuwa hai atakapokuja tena.

## Maswali ya kuzingatia

1. Kanisa langu linafananaje na kanisa la mitume?
2. Ni wapi utendaji wa kanisa langu huenda umepungukiwa?
3. Tutawezaje kusaidia ushirika wetu kufanana na ushirika ulioanzishwa na kupendwa na mitume?

[6] Ellen White, *Christ's Object Lessons:* (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1900,) 373-374.

[7] Ellen White, *Letter 110-1902*, (July 7, 1902), paragraphs 12 and 13.

# Sura ya 3

## Kumaliza Mpango wa Siri wa Mungu

### Maelezo ya Kusudi la Sura ya Tatu

Nimejumuisha sura hii kwa sababu zifuatazo:

1. Inatoa maarifa yanayohitajika katika kufahamu unabii muhimu sana katika Kitabu cha Ufunuo, ambao ulisaidia Waadventista wa kwanza kugundua kwamba hukumu ilianza 1844 na kwamba Ujio wa Pili ulikuwa wa karibuni.

2. Inaonyesha kuwa haraka ya kurudi kwa Yesu inategemea ushirikiano wa mwanadamu katika kutimiza *Mathayo 24:14* and *Ufunuo 14:6 -12.* Ikiwa Waadventista wa kwanza wangeelewa hili, kamwe hawangeweka tarehe ya kurudi kwa Kristo.

3. Inatupelekea kufahamu kuwa Kristo alitaka kurudi kwake kuwe muda mfupi baada ya 1844, lakini ikawa muhimu kwake kukawisha kurudi kwake.

4. Inaonyesha ni nani anahusika na Yesu kuwa na hitaji la kurudi kwake.

Sura hii inaweka msingi wa sura zitakazofuatia, ambazo zinaelezea mabadiliko muhimu tunayofaa kufanya ili kuharakisha marejeo ya Kristo. Katika fundisho hili tutakuwa tukitumia Biblia, maandishi ya Ellen White, na maandishi mengine ya Waadventista waanzilishi.

*2 Timotheo 2:15* inasema, “Jitahidi kujionesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mfanyakazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.” Sasa, hebu tuanze kwa kusoma baadhi ya vifungu vya maandiko katika Ufunuo 11 na 12.

### Malaika wa Saba: Onyo la Mwisho la Mungu kwa Wanadamu

Kitabu cha Ufunuo kina *saba* nyingi: Makanisa saba, mishumaa saba, mihuri saba, tarumbeta saba, n.k. Tarumbeta (Baragumu) katika Ufunuo ni baadhi ya mafungu magumu zaidi katika maandiko kutafsiri. Hata miongoni mwa wasomi wa Biblia wa Kiadventista, hakuna makubaliano ya pamoja ulimwenguni katika tafsiri ya kila kipengele cha tarumbeta saba katika Ufunuo. Hata hivyo, wasomi wote wa Kiadventista wanakubaliana kuhusu jambo moja: tarumbeta saba ni maonyo ya hukumu, wakati wa vipindi saba vya kihistoria, ambavyo vinafululiza katika historia ya Wakristo kutoka karne ya kwanza Baada ya Kristo hadi mwisho wa dahari. Tarumbeta ya saba na ya mwisho, inayopatikana katika sura ya 10 na 11 za Ufunuo,

*Ufunuo 11:15*, “Kisha, malaika wa saba akapiga tarumbeta yake. Na sauti kuu zikasikika mbinguni zikisema, ‘Sasa *Ufalme* wa ulimwengu umekuwa Ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala akiwa mfalme milele na milele.”

Ukisoma Ufunuoa 11:15 peke yake, ni rahisi kupata dhana kuwa hakuna kipindi cha wakati kati ya kupigwa kwa tarumbeta ya saba na kurudi kwa Kristo. Hakuna kutajwa kwa kitu chochote kinachofanyika kati ya matukio haya mawili. Kwa wengine, hili linaweza kuwapelekea kuweka wakati wa kurudi kwa Kristo. Hata hivyo, ukilinganisha andiko na maandiko, tunapata ufahamu zaidi. Ufunuo 11:19 inatoa habari zaidi kuhusu onyo la tarumbeta ya saba.

*Ufunuo 11:19* inatuambia, **"**Kisha hekalu la mungu mbinguni likafunguliwa, na sanduku la agano lake likaonekana hekaluni mwake. Kukatokea umeme, sauti, ngurumo, tetemeko la ardhi, na mvua kubwa ya mawe."

Katika *mstari wa 19*, tunapata tukio mbinguni linalofanana na patakatifu pa Agano la Kale na Patakatifu pa Patakatifu Zaidi. Mahali Patakatifu Zaidi palikuwa pale ambapo sanduku la agano lilikuwa. Kuhani Mkuu ndiye mtu pekee ambaye angeweza kuingia Patakatifu pa Patakatifu. Aliruhusiwa kupaingia mara moja tu kila mwaka, siku ya Upatanisho – siku ya Hukumu kwa Israeli.

Ellen White anasaidia kufafanua Ufunuo 11:19 katika *Pambano Kuu*, ukurasa wa 433. "Hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni, na ikaonekana ndani ya Hekalu lake sanduku la agano lake.' *Ufunuo 11:19.* Sanduku la agano la Mungu liko patakatifu pa patakatifu. Katika huduma ya hema ya duniani, iliyotumika kama mfano na kivuli cha vitu vya mbinguni *(Waebrania 8:5),*' sehemu hii ilifunguliwa tu wakati wa Siku Kuu ya Upatanisho kwa utakasao wa patakatifu. Kwa hivyo, tangazo la kwamba Hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni na sanduku la agano lake likaonekana inaashiria kufunguliwa kwa mahali patakatifu pa patakatifu mno mbinguni mnamo 1844, wakati Kristu aliingia huko ili kufanya kazi ya upatanisho ya kufungua historia ya ulimwengu."[8]

Kutokana na hili, tunafahamu kuwa kupigwa kwa tarumbeta ya saba kunatangaza mwanzo wa mfano ule wa siku ya upatanisho; mwanzo wa hukumu ya upelelezi, ambayo inafanyika kabla ya Kristo kurejea. Ni hukumu inayotangulia ujio wa Kristo, ambayo ilianza Oktoba 22, 1844, na ingali inaendelea mbinguni. Hukumu hii itakamilika mud tu kabla ya Yesu kurejea. Hadi wakati huo, hatima ya milele ya kila mtu ambaye amewahi kuishi inaamuliwa. Kwa wale wangali hai, hatima yao ya milele inaweza kuamuliwa hata wanapoendelea na shughuli zao za kila siku. Ukweli kwamba Kristo aliingia patakatifu pa patakatifu mno mbinguni mnamo 1844, ni ukweli uliodhibitiwa katika kanisa la Waadventista.Ni jambo lisilo na shaka kwa waumini waaminifu wa Kiadventista.

## Tarumbeta ya Saba: Mpango wa Siri wa Mungu

Sasa, hebu tuangalie *Ufunuo 10:7*. Tutagundua kitu ambacho kinaendelea wakati wa kupiga baragumu ya saba – kitu ambacho lazima "kikamilishwe" kabla ya Yesu kurejea. *Ufunuo 10:7* "Lakini wakati yule malaika wa saba atakapotoa sauti ya tarumbeta yake, Mungu atakamilisha **mpango wake wa siri** kama alivyowatangazia watumishi wake manabii."

Je, "mpango wa siri ya Mungu" ambao ulistahiili kukamilika wakati malaika alikuwa anaanza kulia ni upi? Malaika wa saba amekuwa akipiga tarumbeta kwa muda mrefu sana – zaidi

[8] Ellen White, *Pambano Kuu kati ya Kristo na Ibilisi:* (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1911,) 433.

ya miaka 170. Sasa ni miaka mingi sana imepita tangu alipoanza. Je, “mpango wa siri ya Mungu” ulikamilika katika siku “atakapoanza kupiga”? Ni muhimu tupate kufahamu “mpango wa siri ya Mungu” ni nini, kwa sababu inafafanua jukumu letu kama Wakristu wa leo. Biblia inatueleza namna ya kugundua maana ya vifungu vya maandiko katika *Isaya 28:10,* “kwa maana ni amri juu ya amri, sheria juu ya sheria; kanuni juu ya kanuni; mstari baadya ya mstari; huku kidogo na huku kidogo:”

Barua za mtume Paulo kwa Warumi, Waefeso, na Wakolosai zinaelezea maana ya “mpango wa siri ya Mungu“ katika *Ufunuo 10:7*

*Warumi 16:25–26*

25Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu na kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele,

26ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii imani:

Katika kutoa maoni kuhusu *Warumi 16:25-26*, Ellen White aliandika, “Kabla ya kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, Mwana wa Mungu alitolewa kufa, na ukombozi ndiyo siri ambayo ‘ilikaa kimya kwa nyakati za milele’ (Warumi 16:25, R.V.).”[9]

"Katika miaka yote ya umilele, Mungu Baba na Mungu Mwana walifahamu kuhusu kilele cha uasi na maasi ya shetani. Walijua kuwa Shetani angepanga kumjaribu Adamu na Hawa na kuutumbukiza ulimwengu huu kwa mateso na mauti. Upendo mkuu wa Mungu Baba na Mungu Mwana ulidhihirishwa katika mpango wa wokovu kabla ya hii dunia kuumbwa. Mpango wa wokovu ulijulikana tu na Mungu Baba na Mungu Mwana –„ ilikaa kimya kwa nyakati za milele’ (Warumi 16:25, R.V.).”[10]. Ilifichwa hata kwa malaika lakini ikafichuliwa wakati maarifa ya mpango wa wokovu yalihitajika – wakati Adamu na Hawa walipotenda dhambi. Mpango wa ukombozi, wokovu katika Kristo, ndio ‘mpango wa siri ya Mungu’ ambao lazima uhubiriwe kwa ulimwengu wote kabla ya Kristo kurejea, ili kuwapa wanadamu wote fursa ya kuokolewa. Itakuwa ‘imekwisha’ wakati watu wa Mungu watatimiza Mathayo 24:14, "Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."

*Waefeso 3:1–6*

1Kwa sababu hiyo mimi Paulo ni mfungwa wake Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi mataifa;

2ikiwa mmesikia habari ya uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu;

---

[9] Ellen White, *In Heavenly Places:* (Washington, D.C: Review and Herald Publishing Association, 1967,) 291.

[10] Ibid

[3]**Ya kwamba kwa kufunuliwa nalijualishwa siri hiyo;** (kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache,

[4]Kwa hayo, myasomapo, **mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo)**

[5]Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho;

**[6]Ya kwamba Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi ya ke iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili:**

"Mpango wa siri ya Mungu" katika *Ufunuo 10:7* ni sawa na "mpango wa siri ya Kristo" katika *Waefeso 3:4*. Mataifa wanaweza tu kuwa 'washirika' baada ya kusikia kuhubiriwa kwa Injili. Ilikuwa ni siri kwa Wayahudi kwa sababu hawakuelewa vizuri kwamba wokovu katika ufalme wa Mungu ulikuwa uwe na ushirika sawa kati ya Wayahudi na Mataifa. Huku ikifunuliwa kwa njia ya ishara katika enzi nyinginezo (Adamu, Abrahamu, Yakobo, nk.), haikufunuliwa kwa njia sawa na ile ya wakati wa mitume (tajriba ya Petro na Kornelio, tajriba ya Paulo katika njia ya Dameski, siku ya Pentekoste, nk.). Hata mtume Petro hangewahi kwenda nyumbani kwa Kornelio kushiriki Injili, ikiwa Mungu hangempa maono ya wanyama wasio safi kwenye karatasi.[11] Kwa hivyo, kumaliza "mpango wa siri ya Mungu" katika siku za mwisho wa historia ya ulimwengu ni kumaliza jukumu la kuhubiri ujumbe wa wokovu kwa kila mtu duniani. Ilianza katika siku za mitume na itakamilika kabla tu ya kuja kwa Yesu mara ya pili. 'Jumbe za Ufunuo 14 ni zile ambazo kwazo ulimwengu utajaribiwa; ndizo ujumbe wa milele na zinafaa kutangazwa kila mahali."[12] Kwa Waadventista leo, ina maana ya kutimiza kuhubiri Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa ulimwengu wote kwa dharura na kwa haraka, huku tukitafuta usaidizi wa Roho Mtakatifu. Ufunuo 14:6 yasema, "Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa." Hili likifanyika, basi Yesu atarejea.

Katika *Waefeso 6:18-20* na *Wakolosai 4:2-3*, Paulo anaangazia zaidi maana ya 'mpango wa siri ya Mungu.'

*Waefeso 6:18–20*

[18]Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;

[19]Pia na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kwa kufumbua kinywa change, ili niihubiri kwa ujasiri ile siri ya Injili,

[20]ambayo kwa ajili yake mimi ni mjumbe katika minyororo; hata nipate ujasiri katika huyo kunena jinsi inipasavyo kunena.

---

[11] *Matendo ya Mitume 10:1 – 11:18.*

[12] Ellen White, *Manuscript Releases,* vol. 17: (Washington, D.C.: Ellen G. White Estate, 1987,) 15. Written on November 8, 1896.

*Wakolosai 4:2–3*

2Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukurani;

3mkituombea na sisi pia, kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo, ambayo kwa ajili yake nimefungwa:

Kwa nini Paulo alikuwa katika "minyororo" (gerezani) mara kadhaa? Alikuwa kizuizini kwa sababu alikuwa akiwahubiri Mataifa kuhusu "mpango wa siri ya Kristo". Sababu ya Paulo kuwa gerezani ni ile ile sababu ambayo wahubiri wengi katika maeneo mbalimbali ya ulimwengu wametumwa gerezani. Wamerushwa mashimoni na magerezani, wakivumilia mateso na hata kifo kwa kutoshughulikiwa au kwa kuuawa; kwa sababu ya kuihubiri habari ya wokovu katika Kristo kwa ulimwengu.

Paulo pia anaongea kuhusu 'hii siri' katika *Wakolosai 1:25-27*, kifungu maarufu watu wengi wanapofikiria mara kwa mara kufafanua hii 'siri.'

*Wakolosai 1:25–27*

25Ambalo nimefanywa mhudumu wake, sawasawa na uwakili wa Mungu, niliopewa kwa faida yenu, nilitimize lile neno la Mungu;

26Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake:

27Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu:

Utagundua kuwa 'hii siri' ilikuwa imefichwa kwa enzi za zamani lakini sasa inafunuliwa kwa 'watakatifu wake'. Kile ambacho kilikuwa kinafunuliwa kwa 'watakatifu wake' ni 'utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa.' Mtu anapompokea Kristo kama mkombozi wa maisha yake, pia anaahidiwa fursa ya kuwa na Roho Mtakatifu akifanya kazi katika maisha yake; kumpa tabia kama ya Kristo. Hii ndiyo maana ya kuwa na "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu."

Ellen White alichangia suala hili katika kitabu chake *Elimu*, uk. 171-172 ". . . Biblia; wakati kanuni zake zimekuwa vipengele vya tabia, matokeo yamekuwa gani? Ni mabadiliko gani yamefanywa maishani? "tazama ya kale yamepita, mambo yote yamekuwa mapya.' 2 Wakorintho 5:7. Kwa nguvu zake, waume kwa wanawake wamevunja minyororo ya tabia ya dhambi. Wamekataa ubinafsi. Wachafu wamekuwa waaminifu, walevi wamekuwa timamu, wavujaji wamekuwa safi. Nafsi ambazo zimechukua mfano wa Shetani zimebadilishwa na kuchukua sura ya Mungu. Mabadiliko haya yenyewe ni muujiza wa miujiza. Mabadiliko yaliyofanywa na Neno ni mojawapo ya siri kubwa ya Neno. Hatuwezi kuielewa; tunaweza tu kuamini, kama Maandiko yasemavyo, ni "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.' Wakolosai 1:27

"Ujuzi wa siri hii hutoa ufunguo kwa mengine yote. Hufungulia roho hazina ya ulimwengu, uwezekano wa maendeleo yasiyo na kipimo"[13]

Kwingineko anasema, "Ikiwa Kristo atakuwa ndani yetu tumaini la utukufu, tutatembea kama alivyotembea; tutaiga maisha yake ya kujitolea ili kuwabariki wengine; tutakinywea kikombe, na kubatizwa na ubatizo; tuakaribisha maisha ya kujitolea, majaribio, na kujikana nafsi kwa ajili ya Kristo. Mbingu itakuwa rahisi sana, kujinyima kokote tuwezako ili tuipate."[14]

Watu wa Mataifa hawangeweza kuwa na Kristo ndani yao, "tumaini la utukufu" ila tu iwe kwamba Paulo na wengine walikuwa wakiwahubiria Injili. Vivyo hivyo, hili linaweza kutokea katika siku zetu ikiwa tunaihubiri Injili kwa ulimwengu wote. Jumbe za Malaika wa Tatu, Injili, "utajiri usiogundulika wa Kristo"[15] lazima uhubiriwe "kwa kila taifa, jamaa, lugha na watu."[16] Kuwapa Injili kutawapa fursa ya kuokolewa; kupata ondoleo la dhambi zao; na kuwapa nafasi ya kupata utakaso na nguvu za Roho Mtakatifu zigeuzazo maisha ya wanadamu zikifanya kazi ndani yao. Watawezeshwa kuwa na Kristo ndani yao, 'tumaini la utukufu.'[17] Kisha, na hapo ndipo tu, yaweza kusemwa kuwa "mpango wa siri wa Mungu"[18] umekamilika.

Kukamilika kwa 'siri ya Mungu' katika *Ufunuo 10:7*, kumewekwa wazi kama kuihubiri Injili kwa ulimwengu wote. Hata hivyo, kifungu hikik kinatuletea balaa leo.

*Ufunuo 10:7* "Isipokuwa katika siku za sauti ya malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi wake hao manabii."

Katika kifungu hiki, Biblia inaonyesha kuwa kuhubiriwa kwa Injili kwa ulimwengu wote kulipaswa kukamilika kufikia wakati ule malaika alianza kutangaza, mnamo 1844. "Atakapoanza kupida" inaashiria kuwa kuna ***kipindi cha wakati*** ambacho malaika atakuwa akipiga baragumu. Haionyeshi mlipuko mmoja wa tarumbeta. Maneno "yapaswa kumaliza," yameoanishwa na wakati ambapo tarumbeta ilikuwa inaanza kulia. 'Siku' moja katika unabii wa Biblia ni sawa na mwaka mmoja (*Hesabu:14:34, Ezekieli 4:5-6, Danieli 9:24-27, Mwanzo 29:27-28).* Kwa sababu *Ufunuo 10:7* inatuambia kuwa 'siri ya Mungu', 'itatimizwa' katika 'siku' ambazo malaika ataanza 'kutangaza,' inadhirisha kuwa hii itakuwa kwa kipindi cha miaka, ila si kipindi kirefu cha miaka.

Wengine wanaweza kujiuliza ikiwa kuna kitu kibaya hapa. Bibiblia ilitabiria kuwa kuhubiriwa kwa Injili kwa ulimwengu wote kulipaswa kukamilika katika siku ambazo malaika alikuwa anaanza kulia, kuanzia 1844 – lakini kuhubiriwa kwa Injili kwa ulimwengu wote

---

[13] Ellen White, *Elimu*: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association,) 171–172.

[14] Ellen White, *Ushuhuda kwa Makanisa*, Vol. 2: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1871,) 72.

[15] *Waefeso3:8*

[16] *Ufunuo 14:6*

[17] *Wakolosai 1:27*

[18] *Ufunuo 10:7*

hakukuwa kumekamilika kufikia wakati huo. Yesu hajarudi, wala hatujauhubiria ulimwengu wote baada ya muda huu wote kupita Je, ni nini kiliharibika? Je, ni uelewa wetu wa unabii usio sahihi, au kuna kitu kingine kibaya? Jibu linapatikana katika tafsiri sahihi ya kifungu "yapaswa kumalizika." Kwa wale ambao wangetaka kufahamu zaidi kuhusu kifungu hiki katika lugha ya Kiyunani, angaalia maelezo chini ya ukurasa. [19]

Kifungu cha maneno "yapaswa kuwa,' kinachopatikana katika tafsiri ya *King James,* hakipatikani katika kifungu cha Kigiriki. Maneno hayo yaliongezwa ili kutupa maana ile ile inayopatikana katika maandishi asili ya Kiyunani. Kifungu hicho kilikuwa cha kuelekeza watu wa Mungu waliosalia na walioishi katika karne ya 19 kumaliza kuitangaza Injili kote ulimwenguni "katika siku za sauti ya malaika wa saba, atakapoanza kulia" *(Uf. 10:7).* Walipaswa kufanya kazi haraka na kwa uamuzi pindig baada ya 1844. Kifungu hiki hakisemi kuwa "siri ya Mungu' ***ingemalizika*** "wakati atakapoanza kulia," bali kwamba '***inapaswa kumalizika'*** wakati huo. Ikiwa 'siri ya mpango wa Mungu' ingemalizika kwa wakati uliotabiriwa, kulitegemea wale ambao walikuwa wakiishi wakati huo. Kuuhubiri ulimwengu kulianza katika siku za mitume, na kungekamilishwa na watu wa Mungu waliosalia pindi tu baada ya 1844. *Mathayo 24:14* lazima ingetimizwa kwanza kabla ya utimilifu wa *Ufunuo 10:7*.

Huu ni mfano wa kitu kinachoitwa unabii wa masharti, ambao kwa kiasi fulani unafanana na ule unabii wa Yona. Katika kitabu cha Yona, utabiri wa kuharibiwa kwa Ninawi haukutimizwa katika wakati uliotabiriwa kwa sababu watu walitubu na Mungu akawapa rehema.

Vivyo hivyo, haki na huruma ya Mungu inadai kwamba wenyeji wa dunia wapokee ujumbe wa mwisho wa tahadhari, kabla ya kipindi cha upelelezi kufungwa na wenye dhambi wasioutubu

---

[19] Katika *Ufunuo 10:7,* neno "malizika" ni ***τελέω*** *"teleo"* katika Kigiriki. *"Teleo"* ina maana ya:

**"1** kuleta kikomo, kufunga, kumaliza. . .. **2** kufanya, kutekeleza, kukamilisha, kutimiza . . . 2a . . . kutekeleza yaliyomo katika maagizo. 2b . . . kufanya kama ilivyoamriwa, na kwa ujumla inahusu dhana ya wakati, kutekeleza kitendo cha mwisho kinachokamilisha mchakato, kukamilisha, kutimiza." Angalia https://www.biblestudytools.com/lexicons/greek/kjv/teleo.html and https://www.bibletools.org/index.cfm/fuseaction/Lexicon.show/ID/G5055/teleo.htm

*"Teleo"* katika kifungu hiki limeandikwa katika mhemko wa kiunga. Lugha ya Kiyunani inaweza kuonyesha 'mhemko' katika tahaji ya kitenzi. Sio lugha zote zenye uwezo huo. Lugha zingine huongeza maneno kuashiria 'mhemko'. Mhemko katika viambishi vya Kigiriki huruhusu hali ya kutokuwa na uhakika. Mtu anaweza kuwa anataka jambo lifanyike wakati fulani, lakini kufanyika au kutofanyika kwake kwa wakati huo kunategemea hali itakavyokuwa. Hapa, mhemko ni wa masharti. Tazama http://www.ntgreek.net/lesson29.htm and https://www.ntgreek.org/learn_nt_greek/subj-detail-frame.htm

Ikumbukwepia kwamba Agano Jipya katika tafsiri ya King James lilitafsiriwa kutoka kwa maandishi ya Kigiriki yaitwayo Textus Receptus. Katika *Ufunuo 10:7*, maandishi ya Textus Receptus yana neno *"teleo"* lililoandikwa katika mhemko huo. Hata hivyo, katika tafsiri nyingine nyingi za sasa, maandishi mengine ya Kigiriki yametumika kama msingi wa tafsiri. Katika tafsiri hizo, neno "teleo" haliko katika mhemko wa Ufunuo 10:7, na kwa hiyo kutoa maana tofauti kama vile'itakamilika', n.k . Waadventista wa kwanza walitumia tafsiri ya King James katika kugundua ukweli wa unabii wa Biblia.

kupotea milele. Sharti wapewe nafasi ya kutubu na kuokolewa. Jukumu la kuwapa hiyo nafasi limepewa kanisa. Kwa kushindwa kuuonya ulimwengu haraka, tumechukua nafasi muhimu katika kukawisha marejeo ya Yesu. Na kwa sababu hiyo, watu wengi wamepotea, na wengine wengi wanaendelea kupotea kila siku. Hiyo basi, tuungame na tutubu mara moja dhambi yetu ya kupuuza habari ya wokovu kwa ulimwengu. Kuna wengine kanisani ambao wamekuwa waaminifu kwa jukumu lao la kushiriki Ujumbe wa Malaika wa Tatu bila kukawia. Hata hivyo, maneno ya Danieli 5:27 yanaweza kutumika kwa wengi wetu – "Umepimwa kwa mizani, na umepatikana umepungua." Acha tujitoe au tujitolee maisha yetu upya ili kuharakisha kurudi kwa Yesu.

### Maswali ya Kuzingatia

1. Je, ninaweza kufanya nini kusaidia kuufunulia ulimwengu 'mpango wa siri ya Mungu', na kwa hivyo kuharakisha ujio wa pili wa Kristo?

2. Je, mimi binafsi ninaufahamu kikamilifu mpango wa siri ya Mungu? Je, nina maswali gani? Ni muhimu kuweza kuyajibu maswali yetu wenyewe, ili tuweze kuyajibu maswali ya watu wengine.

3. Je, kumkubali Kristo kama mkombozi wangu kumeyabadilisha vipi maisha yangu? Shiriki hizo shuhuda na wengine! Hizo shuhuda huwasha moto ndani ya waumini wapya; hamu ya kumfuata Kristo na kuwa zaidi kama yeye.

4. Je, ni kwa namna gani naweza kuwa mkarimu zaidi kwa maisha ya kujitolea, majaribu, na kujikana kwa ajili ya Kristo?

5. Je, ni nani ninayemfahamu anayeweza kunisaidia kuufunua mpango wa siri ya Mungu kwa ulimwengu?

6. Je, ni shughuli za namna gani ninazofaa kupnaga ili kushiriki na wengine mpango wa siri ya Mungu?

# Sura ya 4

## LAKINI – "ameweka siku . . ."

*Matendo ya Mitume 17:31* "Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu." Je, kifungu hiki kinaashiria siku maalum, ambayo Bwana ameweka kwa ajili ya kurudi kwa Kristo ama ni unabii wa masharti? Kwanza, lazima tufahamu kwamba siku 'ambayo atauhukumu ulimwengu' sio wakati wa sauti ya malaika wa saba. *Ufunuo 10:7* inaita kipindi cha hukumu ya upelelezi, "siku za sauti ya malaika wa saba." Hali ya wingi ya "siku za," inaashria ***kipindi cha wakati***, wala sio siku maalum. Ile 'siku, ambayo atauhukumu ulimwengu,' ni sawa na 'siku ya Bwana' ambayo inatajwa katika *2 Petro 3:3-12*, ndio Ujio wa Pili wa Yesu.

*2 Petro 3:3–12*

"3Mkijua kwanza neno hili ya kwamba katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe,

4na kusema, iko wapi ahadi ile ya kuja kwake? Kwa maana, tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa.

5Maana hufumba macho yao wasione neno hili ya kuwa zilikuwako mbingu tangu zamani, na nchi pia, imefanyizwa kutoka katika maji, na ndani ya maji, kwa neno la Mungu:

6kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.

7Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.

8Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na maiak elfu ni kama siku moja.

9Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali woete wafikilie toba.

10**Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka ka mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.**

11Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katiak mwenendo Mtakatifu na utauwa,

12mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka?"

“Kama kanisa la Kristo lingefanya kazi yake teule kama ilivyoagizwa na Bwana, ulimwengu wote ungekuwa tayari umeonywa, na Bwana Yesu angekuwa amekuja kwa nguvu na utukufu mwingi.”[20] Kuhubiriwa kwa Injili ni kazi teule kwa kanisa, na tumekuwa tukiihubiri injili katika makanisa yetu kila Sabato kwa zaidi ya karne moja na nusu. Mbona Yesu bado hajaja? Kulikoni? Tumekuwa tukihubiri na kuhubiri na kuhubiri, na Yesu bado hajaja. Kama ilivyotajwa hapo awali, wachungaji wanalemewa, wakijaribu kutosheleza matakwa ya wale ambao tayari wamesikia na kukubali mwaliko wa injili. *Luka 10:2,* **“Mavuno ni mengi lakini wafanyakazi ni wachache.”** Wafanyakazi wachache waliopo wanajishughulisha sana kuwatunza washiriki wa kanisa.

Nchini Marekani tunatumia msemo, “Je, tunahubiria kwaya?”. Mataifa mengine yanatumia misemo tofauti kuelezewa jambo lilo hilo. Wao husema, “Je, tunabisha milango ambayo tayari imefunguliwa?” Katika *Ufunuo 3:20,* Yesu anasema, “Tazama nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kufungua mlango, nitaingia kwake, name nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.” Yesu hutumia wakati wake kubisha milango iliyofunfwa. Tunatarajiwa kufuata mfano wa Yesu na kufanya vivyo hivyo. Badala yake, tumekuwa tukipoteza pesa nyingi, vipawa na wakati, kwa kubisha milango ambayo tayari iko wazi. Kwa sababu hiyo, mamilioni ya watu wamekwenda makaburini kama waliopotea, hata watakapoamka katika ufufuo wa pili – mwisho wa milenia, kukabili kifo cha milele.

Mnamo Mei 25, 2011, Mheshimiwa Bharrat Jagdeo, Rais wa taifa la Guyana, alitoa hotuba kuu katika kikao cha wanabiashara wa Guyana. . Yamkini, masimulizi yake kuhusu jukumu la kanisa yalikuwa sahihi sana, haswa kwa mtu ambaye sio Mkristo Rais Jagdeo ni Mhindu. Sehemu za hotuba yake zilichapishwa katika jarida la *Adventist World,* katika toleo la Agosti 2011. Nikinukuu kutoka kwa jarida hilo, “Kuwahubiria waongofu mara moja kila wiki hakutaibadilisha jamii, Jagdeo aliwakumbusha wajumbe wa kikao. Maisha ya ‘Yesu’ hayakuwa na tabia ya sala tu, bali pia huduma’, alisema. ‘Kwa hiyo hatuhitaji tu kusali katika majengo mizuri, bali pia twende katika jamii, mahali watu wako” [21]

Je, inawezekana kwamba Mhindu, Rais wa Guyana, alielewa bora kinachohitajika katika kuieneza injili kutuliko? Kauli yake iligonga ndipo. Laiti mfano wetu ungekuwa mzuri kama kauli yake.

Yesu anasema katika *Luka 4:18,* “Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa.”

*Marko 2:17* inatuambia, “Yesu aliposikia aliwaambia, wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.” **Kuwaita “wenye dhambi katika toba” ndilo jambo moja la muhimu zaidi tunaloweza kufanya.**

---

[20] Ellen White, *Tumaini la Vizazi Vyote:* (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1898,) 633-634. 12

[21] *Barbara Savory, “Guyana’s President Lauds Adventists,” Adventist World, August 2011. 3-4.*

Kwa sababu ya kutoamini kwao, iliwalazimu Waisraeli kutangatanga jangwani kwa miaka 40, na watu wazima wakafa nyikani. Watoto wao waliruhusiwa kuingia katika nchi ya ahadi. Je, hii inasema nini kuhusu imani ya Waadventista wakati tumekuwa tukitangatanga kwa zaidi ya miaka 170 tangu 1844? Hiyo ni zaidi ya mara nne kushindwa Waisraeli walivyotangatanga nyikani. Je, sisi ni wabaya zaidi ya mara nne ya Waisraeli wasioamini?

Jambo la pekee ambalo Mungu aliwauliza Waisraeli kufanya lilikuwa kwenenda kwa imani kwa kutii maagizo yake yote wapte kuingia katika nchi ya ahadi. Kwa kumtii Mungu, Waisraeli wangeingia katika Kanaani ya duniani miaka 40 mapema, ingawa bado wangekufa duniani. Kitu ambacho Mungu anauliza kanisa la masalio kufanya leo ni kuuhubiri Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa Ulimwengu wote, kwa msaada wa nguvu ya Roho Mtakatifu. Kwa kufanya hivyo, tutaingia katika Kanaani ya mbinguni, ambapo ‘hakutakuwako na kifo tena, wala huzuni, au kilio, wala hakutakuwako na maumivu yoyote; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.” *Ufunuo 21:4.* Huko, Yesu atatuambia “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu. Umekuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako.” *Mathayo 25:21.* Hatuna chochote cha kupoteza chenye umuhimu wa milele ila kufaidi kwa kila kitu ikiwa tutaishi kwa imani yenye utiifu kwa amri zake. Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, pamoja na malaika wote wanasubiri kutusaidia kufanya kazi waliyotuitia haraka.

Nukuu chache zifuatazo kutoka kwa Ellen White ni muhimu sana.

*Review and Herald*, (Machi 27, 1894, aya 14). “Kwa nini Bwana amekawia sana kurudi kwake? Jeshi lote la mbinguni linasubiri kutimiza kazi ya mwisho kwa ulimwengu huu uliopotea, na bado kazi inangoja. Ni kwa sababu wachache wanaodai kuwa na mafuta ya neema kwenye vyombo vyao na taa zao, hawajakuwa taa ziwakazo  na kuangaza ulimwenguni. **Ni kwa sababu wamishonari ni wachache.** [22]

“Kwa miaka arobaini, kutokuamini, kunung’unika, na kuasi kuliwazuia Waisraeli wa kale kuingia katika nchi ya Kanaani. Dhambi zile zile zimekawisha Israeli ya sasa kuingia katika Kanaani ya mbinguni. Katika hali zote mbili ahadi za Mungu hazikuwa na dosari. Ni kule kutokuamini, kuupenda ulimwengu, kutojitolea, na ugomvi kati ya watu wanaojidai kuwa wa Mungu ambako kumetuweka katika ulimwengu huu wa dhambi na mateso kwa miaka mingi. – *Maandishi 4, 1883.* Huenda tukalazimika kubakia hapa katika ulimwengu huu kwa muda mrefu zaidi kwa kutotii agizo la Mungu, kama vile wana wa Israeli walivyofanya; ila kwa ajili ya Kristo, watu wake hawapaswi kuongeza dhambi juu ya dhambi kwa kumlaumu Mungu kwa matokeo ya mienendo yao mibaya. — Barua 184, 1901.”[23]

Tumeshtakiwa kwa kosa la ‘kuasi’ dhidi ya Mungu! Kwa bahati nzuri, maonyo na mashtaka ya Mugnu dhidi yetu pia ni Ishara zake za upendo na uvumilivu wake. Hamu yake kubwa ni kutona tukitubu na kutii. Hataki kungoja sana ili arudi na kutupeleka nyumbani. Mnamo 1849, chini ya miaka 4 baada ya Tamauko Kuu la Oktoba 22, 1844, Dada White alilandika yafuatayo katika *Broadside 2*, aya 13, iliyochapishwa Januari 31, 1849, “Niliona kuwa muda wa Yesu kuwa

---

[22] Ellen White, *The Review and Herald*, March 27, 1894, par. 14.

[23] Ellen White, *Evangelism:* (Washington, D. C.: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 696.

katika mahali  patakatifu pa patakatifu ulikuwa karibu kukamilika, na muda huo unaweza kudumu si kitambo sana. . ."[24]

Yesu alitamani kuja kwa mara ya pili punde baada ya 1844. Bila kutapatapa kuhusu jambo hilo, hatukuwa tayari kuuambia ulimwengu kuhusu Yesu, wala hatukuwa tayari kukutana naye.

Kuhusu hali ya masharti ya unabii wa marejeo ya Kristo, dada White aliandika katika *Evangelism, ukurasa wa 695 na 696:*

"Malaika wa Mungu katika jumbe zao kwa wanadamu wanaonyesha kuwa muda ni mfupi sana. Na hivyo ndivyo imekuwa ikifunuliwa kwangu. Ni kweli kwamba muda umeendelea zaidi kuliko vile tulivyotarajia katika siku za kwanza za ujumbe huu. Mwokozi wetu hakuonekana haraka kama tulivyotarajia. Lakini je, Neno la Bwana halikuwa la kweli? Hasha! Ikumbukwe kuwa ahadi na vitisho vya Mungu ni sawa kimasharti.

"Mungu alikuwa amewapa watu wake kazi ya kutekelezwa duniani. Ujumbe wa malaika wa tatu ulipaswa kutolewa, mawazo ya waumini yaelekezwe katika patakatifu pa mbinguni, ambapo Kristo aliingia kufanya upatanisho kwa watu wake. Marekebisho ya Sabato yalipaswa kuendelezwa. Ukiukaji wa sheria ya Mungu lazima urekebishwe. Ujumbe lazima utangazwe kwa sauti kuu, ili wakaazi wote wa dunia wapate kupokea maonyo. Watu wa Mungu lazima wajitakase nafsi zao kwa njia ya kuitii kweli, na wawe tayari kusimama bila lawama mbele ya Mungu siku hiyo inakuja.

"Laiti Waadventista, baada ya tamauko kuu la 1844, wangeshikilia imani na kukaza mwendo kwa umoja katika ufunguzi wa uthibitisho wa Mungu, wakipokea ujumbe wa malaika wa tatu wakiuhtangaza ulimwenguni kwa nguvu za Roho Mtakatifu, wangeuona wokovu wa Mungu, naye Bwana angefanya kazi pamoja na juhudi zao, kazi ingekamilika, na Kristo angekuja kuwapokea watu wake kwa thawabu yao.."[25]

Je, ni muda kiasi gani utapita baadya ya jumbe za kweli kufikia ulimwengu wote? Hakutakuwa na kukawia kwa matukio ya mwisho.

Ujio wa Bwana hutakawia baada ya ujumbe kufikia mataifa yote, ndimi na watu wote. Je, sisi tunaodai kuwa wanafunzi wa unabii tutasahau kwamba uvumilivu wa Mungu kwa waovu ni sehemu ya mpango wake mkubwa wa uvumilivu, ambao kwao anatafuta kuendesha wokovu wa roho?"[26] – The Review and Herald, Juni 18, 1901.

Hoja kuu kwetu kukumbuka ni dhahiri. Haraka ya kurudi kwa Yesu kunategemea kwa kiwango kikubwa, wewe na mimi.

---

[24] Ellen White, *Broadside 2*, January 31, 1849, par. 11.

[25] Ellen White, *Evangelism:* (Washington, D. C: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 695-696.

[26] Ellen White, *Review and Herald,* June 18, 1901, 1.

## Maswali ya Kuzingatia

1. Je, ninawezaje kuwa nikiishi kama Waisraeli nyakati za Bibilia?

2. Je, ninawezaje kuishi tofauti na Waisraeli waliopungukiwa na imani na kutembea nyikani kwa miaka 40?

3. Je, nianze lini kutangaza Ujumbe wa Malaika wa 3? Je, naweza kufanya nini ili kuueneza haraka na kwa namna ifaayo?

4. Je, ni kwa njia gani ninaweza kuwasaidia wengine kumpata Kristo?

# Sura ya 5

## Ni Wangapi Watapotea Ikiwa …?

Wengine wanaweza kuwa na wasiwasi kuhusu usalama wa waumini ikiwa wachungaji wao watakuwa nje ya makanisa yao kwa muda, wakihubiri na kufungua makanisa. Je, waumini wanaweza kusimama kiroho, na je, makanisa yataweza kuendelea?

Kutokana na mapitio ya data na kuongea na viongozi wa kidini katika maeneo mbalimbali ya ulimwengu, jambo moja ni wazi kabisa; wakati wachungaji wana makanisa 10 na zaidi (wengine wana 30 hadi 40, hata makanisa 90 nchini Angola) katika wilaya zao, makanisa hukua haraka na wahubiri wasiohitimu hufungua makanisa mengi. Wakati wachungaji wana makanisa machache katika wilaya zao, kwa kawaida makanisa hayakui sana, na wakati mwingine hayakui hata kidogo. Katiak hali hizi, waumini wanatarajia wachungaji wafanye kazi kubwa ya uinjilisti, pamoja na kazi ya kuwahudumia waumini waliobatizwa. Ellen White alisema, "Ikiwa wahubiri wataondokea starehe zao, ikiwa watavamia maeneo mageni, waumini watalazimika kuwajibika, **na uwezo wao ungeongezeka kutokana na utendakazi**.—Barua 56, 1901."[1] Ukweli huu ambao Ellen White alisema, umethibitishwa katika maeneo mengi ya ulimwengu mahali ambapo kuna makanisa mengi lakini wachungaji wachache. Imethibitishwa kwa nguvu zaidi haswa katika maeneo machache ya ulimwengu ambapo wachungaji hupewa maeneo ya kijiografia badala ya kupwea makanisa maalum (hili litaonyeshwa baadaye kwenye kitabu). Kanuni iyo hiyo hutumika katika malezi ya watoto. Watoto wanapojifunza kuwajibika na kujifanyia mambo wao wenyewe, wanaishia kuwa watu wazima wenye uwezo, kuliko wanapofanyiwa mambo yao yote na wazazi wao, mwaka baada ya mwaka.

### Usalama: Fikiria hali ifuatayo.

Tuseme kwa mfano, kwamba mchungaji wenu ameugua sana homa kali, asiweze kuhubiri katika kanisa lenu kwa mwezi mzima. Na hatari zaidi, ikiwa hakuna mchungaji mwingine mwenye kibali au lesne ya kuja kuwahubiria kwa kipindi hicho. Wazee, mashemasi na waumini wengine labada watalazimika kushughulikia mahubiri, kuwazuru wenye mahitaji, nk. Tafakari hayo kwa kifupi kisha ujibu hili swali. Je, ni wangapi kati ya waumini wa kanisa lenu watapotea milele, na kuungua katika ziwa la moto, au wakose kwenda mbinguni kwa sababu ya kutosikiza mahubiri au kutotembelewa na mchungaji aliyehitimu? Ni wangapi? Je, unafikiri pengine kumi watapotea? Pengine watano? Pengine wawili? Ukweli wa mambo ni kwamba hakuna hata mmoja anaweza kupotea kwa sababu ya kusikiza mahubiri au kutembelewa na wazee. Hakuna hata mmoja. Kwa nini? Kwa sababu washiriki tayari wana ufahamu wa maarifa ya wokovu na wanajua namna ya kuitoa mioyo yao kwa Mungu kila uchao. Iiwa kuna mtu angepotea, itakuwa ni kwa sababu tofauti, na lawama itakuwa yake mwenyewe.

---

[1] Ellen White, *Evangelism:* (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 382.

Je, na ikiwa mchungaji angekuwa mgonjwa kwa miezi sita na kusiweko mchungaji mwingine aliyeajiriwa kuja kuhubiri na kushughulikia hayo mahitaji mengine mengi ambayo kwa kawaida hufanywa na wachungaji? Ni waumini wangapi wa kanisa lako wangepotea milele, waungue katika ziwa la moto, au wakose kwenda mbinguni kwa sababu mchungaji wenu hangeweza kuhubiri au kufanya jambo jingine loltoe kanisani mwenu kwa miezi sita? Kama ilivyo katika mfano uliotangulia, hakuna hata mmoja atakayekosa wokovu kwa sababu hiyo.

Hebu sasa tufanye swala hilo kuwa ngumu zaidi. Tusema kwamba wachungaji wa makanisa yote wajipate gerezani kwa miaka mitano kwa sababu ya kuihubiri Injili. Je, ni waumini wangapi waliobatizwa watapotea kwa sababu ya kulazimika kusikiza mahubiri kutoka kwa viongozi wasiohitimu badala ya wachungaji wenye kibali? Tena, hakuna atakayepoteza uzima wa milele kwa sababu hiyo pekee. Ikiwa mwumini aliyebatizwa atapotea, itakuwa ni kwa sababu nyingine tofafuti, na tena, lawama itakuwa juu yake.

Kuna wakati katika historia yetu ya Kiadventista katika taifa ambalo wakristu walikuwa wakiteswa tulikuwa na wachungaji 200 na miongoni mwao wachungajji 198 walikuwa gerezani. Nilikutana na mchungaji mmoja kutoka mataifa hayo ambaye angali anakumbuka siku ile ambayo baba yake, akiwa mchungaji wakati huo, alipopelekwa gerezani. Hakuwahi kumwona babake tena. Waumini wa kanisa hio hawakupotea njia ya wokovu kwa sababu hiyo. Walimtegemea yesu kuidumisha imani yao na wakabakia imara. Waumini katika taifa hilo wangali waaminifu.

Sasa, hapa kuna swali la muhimu zaidi. Je, watu wangapi ambao sio Wakristo waliobatizwa, wasiojua njia ya wokovu, huenda walipotea katika miaka mitano iliyopita na wakaenda makaburini mwao bila uhakikisho wa wokovu? Je, ni wangapi watafufuliwa wakati wa ufufuo wa pili, waungue katika ziwa la moto, na wakose kwenda mbinguni kwa sababu wachunjaji waliohitimu wamekuwa wakiwahubiria na kuwatembelea waumini, badala ya kutafuta kondoo waliopotea kwa miaka mitano iliyopita? Je, ni wangapi wamepotea kwa sababu wachungaji wamekuwa wasibisha milango ambayo tayari i wazi?

Sabato moja katika wilaya yenye makanisa matatu na ambayo nilihudumu kama mchungaji, niliacha ibada kanisani wakati kulikuwa na ibada maalum katika kanisa mojawapo (haikuwa lazima nihubiri sabato hiyo) nami nikaenda kumtembelea mtu mmoja na mkewe, ambao walikuwa wameacha kuja kanisani. Walishangaa sana kujua kwamba nilikuwa nimeacha huduma kanisani ili kuwatembelea. Ziara hiyo iliwaathiri sana. Waumini waliopotea ni wa thamani sana kwa Yesu, na waumini waaminifu wanastahili kufahamu hivyo. Wanahitaji kuona kwamba wao wenyewe wanastahili kuwatembelea wenzao na kuwatafuta waliopotea. Washiriki wa kanisa, wawe wamehitimu au la, wanatosha kutembelea washiriki waliotelezea na kuwasaidia kuwarejesha katika ushirika kanisani.

*Luke 15:4–7*

4 Ni nani kwenu, mwenye kondoo mia, akipotewa na mmojawapo, asiyewaacha wale tisini na kenda nyikani, aende akamtafute yule aliyepotea hata amwone?

5 Naye akiisha kumwona, humweka mabegani pake akifurahi.

[6]Na afikapo nyumbani kwake, huwaita rafiki zake na jirani zake, akawaambia, Furahini pamoja name, kwa kuwa nimwekwisha kumpata kondoo wangu aliyepotea.

[7]Nawaambia, vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu.

## Maswali ya Kuzingatia

1. Je, unahisi kuwa wewe au waumini wenzako manweza kupoteza wokovu ikiwa mchungaji wenu ataondoka kwenda kuanzisha makanisa?

2. Je, wokovu wa roho moja iliyopotea una umuhimu gani kwakko, ukilinganisha na umuhimu wa kundi kubwa linalojua njia ya wokovu?

3. Je, roho moja iliyopotea ilikuwa na umuhimu gani kwa Yesu?

4. Je, mchungaji atatarajiwa kutenda kama Yesu?

5. Ni kwa njia gani, kuhusu maswali yaliyopo hapo juu, mchungaji anaweza kuwa kama Yesu ikilinganishwa na namna wanavyofanya mambo yao katika makanisa yetu sasa?

6. Je, kanisa lako litachukulia vipi hali ambapo mchungaji wenu hawezi kulitunza kundi lake kwa mwezi? Miezi sita? Mwaka?

# Sura ya 6

## Majukumu ya Washiriki na Wachungaji

Majukumu ya mchungaji yameainishwa vizuri katika Bibilia, na hasa katika maandishi ya Paulo. Wajibu wake umewekwa wazi pia katika maandishi ya Ellen White. Hakuna haja ya sisi kuwa wajinga juu ya suala hili.

*General Conference Bulletin,* Aprili 12, 1901, p.204.

“Kazi ya mhudumu ni kuhudumu. Wahudumu wetu wanapaswa kufanya kazi chini ya utaratibu wa maandiko kuhusu huduma. Habari imenifikia kwamba kote Marekani kuna mashamba tasa. Nilipokuwa nikizuru kusini hadi Ofisi Kuu, niliona mji baada ya mji ambako kazi bado haijafanyika.

“Shida iko wapi? Wahudumu wanazunguka makanisa, ambayo yanajua ukweli, huku maelfu wakiangamia nje ya Kristo.” [1]

**The word, *"hovering,"* is commonly used in American English to illustrate someone who is intently supervising something.**

Ellen White anaendelea katika hayo makala,

“Ikiwa maagizo sahihi yangetolewa, ikiwa njia sahihi zingefuatwa, kila mshiriki angefanya sehemu yake kama kiungo cha mwili. Angefanya kazi yake ya umishonari kama mkristo. Lakini makanisa yanakufa, na wanataka mchungaji awahubirie. Wanahitaji kufunzwa kuleta zaka kwa Mungu kwa uaminifu, ili awaimarishe na kuwabariki. Wanastahili kuletwa katika utaratibu wa kutenda kazi, ili pumzi ya Mungu iwafikie. Wanapaswa kufunzwa kwamba isipokuwa tu waweze kujisimamia bila mchungaji, wanahitaji kugeuzwa upya na kubatizwa upya. Wanahitaji kuzaliwa mara ya pili.”[2]

Je, waona kwamba tunahitaji kufikiria tena namna tunavyowatumia wachungaji? Ikiwa mmebarikiwa sana kiasi cha kuwa na mchungaji anayesimamia kanisa lenu, tafadhali msitumie wakati wake kuwatunza ninyi wenyewe. Je, kwa nini msimwache mchungaji awaongoze katika kuongoa roho za watu? Acha mchugnaji awafunze kwa ajili ya kumtumikia Mungu, uinjilisti, na kufungua makanisa. Acha kanisa lenu lijulikane kama kanisa ambalo linawafundisha vijana kazi ya umishonari kwa bidii, na kisha kuwafadhili na kuwatuma.

---

[1] Ellen White, *The General Conference Bulletin*, April 12, 1901, 204.

[2] Ibid.

Hii ni mojawapo ya taarifa za kushangaza kuhusu kile ambacho wachungaji hawapaswi kufanya.

*Australasian Union Conference Recorder,* Agosti 1, 1902, aya 7.

"Wachungaji wetu hawapaswi kuzunguka makanisa, **wakiyachukulia makanisa kwa kiwango fulani kuwa kazi yao maalum.** Na makanisa yetu hayapaswi kuona wivu au kuhisi yamepuuzwa wasipopokea huduma za mchungaji aliyehitimu. Wao wenyewe wanastahili kujitwika jukumu na kufanya kazi kwa bidii kuokoa roho."[3]

Je, ulielewa hilo? Hiyo ina maana kwamba hakuna mgao wa kazi kwa wachungaji kanisani! Wachungaji wanastahili kuwa kama mtume Paulo na kufungua makanisa mapya badala ya kutunza yale maze. Katika siku za awali za dhehebu la Waadventista, wachungaji hawakupewa jukumu la kutunza makanisa. Walikuwa kama mtume Paulo. Walianzisha makanisa mapya na kuwateua wazee waliochaguliwa na kanisa. Baada ya hapo, wao wazee ndio waliokuwa na jukumu la kuhudumu na kutunza makanisa. Kisha, Paulo angeenda katika maeneo mengine mapya na kurudia mchakato uo huo, na ndiyo sababu moja Paulo alikuwa akiyaandikia makanisa barua. Alikuwa ameyaacha makanisa chini ya uongozi wa wazee – yeye hakuwapo tena.

Mungu ana mpango kwa kanisa lake le; mbinu ile ile kama siku za Paulo. Mungu hajabadilika – na mpango wake haujabadilika.

Je, washiriki wanastahili kusema nini kwa mhubiri wa Injili? Je, walie na kunung'unika ikiwa mchungaji hatawahubiria kila wiki, au wadhihirishe roho ya kweli ya umishonari? Katika *Testimonies for the Church, vol. 6,* uk. 30, Ellen White anatuambia haswa namna ya kutenda na nini haswa tuseme kwa wachungaji ambao hutumia muda wao wote kuyatunza makanisa yaliyopo.

"Badala ya kuwafungia wachungaji wakiyatumikia makanisa ambayo tayari yanajua ukweli, acha waumini wa makanisa wawaambie hawa wafanyakazia: "Nendeni mkatumikie roho za watu zinazoangamia gizani. Sisi wenyewe tutaendesha mikutano, na kwa kukaa ndani ya Kristo, tudumishe maisha ya kiroho. Tutatumikia roho zilizo karibu nasi, na tutatuma sala zetu na zawadi zetu kuwasaidia wafanyakazi wenye kuhitaji zaidi katika maeneo fukara.'"[4]

Katika *Pacific Union Recorder*, Agosti 1, 1901, Ellen White aliashiria kuwa washiriki wa kanisa wanapaswa kuchukua jukumu kubwa wenyewe katika kuanzisha makanisa.

"**Kwa wote wanaoamini, Mungu ameweka mzigo wa kufungua makanisa.** Madhumuni ya wazi ya kanisa ni kuwaelimisha wanaume kwa wanawake kutumia uwezo wao wa ndani kwa manufaa ya ulimwengu, kutumia uwezo ambao Mungu amewapa, kwa utukufu wake." Amewafanya wanadamu mawakili wake. Nao watumie vipawa alivyowatunuku katika kuendeleza kazi yake na kuupanua Ufalme wake. Makanisa yetu, makubwa kwa madogo, hayafai kuchukuliwa kana kwamba yatategemea sana msaada wa mhudumu. Washiriki

---

[3] Ellen White, *Australasian Union Conference Record,* August 1, 1902, par. 7.

[4] Ellen White, *Testimonies for the Church* Vol. 6: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1901,) 30.

wanastahili kudhibitika katika imani ili wawe na ujuzi mzuri wa kazi ya umishonari. Wanapaswa kuiga mfano wa Kristo, wakiwahudumia walio karibu nao. Kwa uaminifu, watimize ahadi walizotoa wakati wa ubatizo, ahadi kwamba watatekeleza matunfozo waliyopata katika maisha ya Kristo. Wanastahili kushirikiana katika kutenda kazi ili kudumisha kanuni za kujikana na kujitolea katika kanisa, ambazo Kristo, huku uungu wake ukivikwa ubinadamu, alifuata katika kazi yake ya umishonari. Ni kule kutoa ujuzi wa upendo na huruma za Kristo kunakofanikisha juhudi zote za umishonari."[5]

Kukiwa na msaada wa aina hii kutoka kwa makanisa, wachungaji wangekuwa na matokeo bora kwa kazi zao. Wanaporejea makanisani mwao mara kwa mara, ripoti za misheni wanazoweza kutoa huenda zikasisimua. Wachungaji na makanisa yangekuwa na hadithi nzuri zenyenguvu – hadithi za makanisa mapya ya Kiadventista katika miji ambayo haikuwa na uwepo wa Waadventista hapo awali. Ripoti za makanisa mapya kufunguliwa pamoja na waumini wapya wanaofurahia ukweli zingeletea makanisa yaliyopo furaha kuu. Kazi ya Kristo ingekuwa inaendelea huku makanisa yakiharakisha kurudi kwake. Tungeenda nyumbani upesi zaidi. Amina na Amina.

Wachungaji wetu wanastahili kuwa wakiiga mfano wa kanisa la kwanza katika kitabu cha Matendo ya Mitume, na waumini wanastahili kuunga mkono juhudi hizo. Mtume Paulo ndiye mfano wa kipekee.

Kutoka kwa kitabu, *Gospel Workers,* uk. 58, "Kwanza kabisa kati ya wale walioitwa kuhubiri injili ya Kristo ni mtume Paulo, asimamaye kwa kila mchungaji kama kielelezo cha uaminifu, kujitolea na bidii. Uzoefu wake na maagizo yake kuhusu utakatifu wa kazi ya mhudumu, ni chanzo cha msaada na msukumo kwa wale wanaojihusisha na huduma ya Injili."[6]

Paulo alitumika kwa ajili ya kondoo mmoja aliyepotea, huku akiwaacha wale tisini na tisa zizini. Safari zake zilimpeleka katika maeneo ya ulimwengu ambayo ujumbe wa wokovu wa Kristo kamwe hukuwa umesikika. Alibisha milango iliyokuwa imefungwa. Maneno yake mwenyewe katika sura ya 15 ya Warumi, yanaonyesha shauku kwa utume wa Kristo katika kuokoa wanadamu.

*Warumi 15:20– 22*

20 kadhalika nikijitahidi kuihubiri Injili, nisihubiri hapo ambapo jina la Kristo limekwisha kutajwa, nisije nikajenga juu ya msingi wa mtu mwingine:

21 bali kama ilivyoandikwa, wale wasiohubiriwa habari zake wataona, na wale wasiojasikia watafahamu.

22 ndiyo sababu nalizuiwa mara nyingi nisije kwenu.

---

[5] Ellen White, *Pacific Union Recorder*, August 1, 1901, Volume 1, page 1, paragraph 7.

[6] Ellen White, *Gospel Workers:* (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1915,) 58.

Paulo hakuifanya iwe tabia yake kukaa mahali kama mchungaji wa kanisa lililopo na kuwahubiria washiriki mwaka baada ya mwingine. Alijua fika kuwa waliopotea watabakia kupotea bila mchungaji aliye hai kuwatafuta.

*Warumi 10:13–15*

13kwa kuwa, kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.

14Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri?

15Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!

Injili laizma iende kwa ulimwengu wote kabla ya Yesu kurudi. Je, ni vipi tena mataifa yote yateweza kubarikiwa kama alivyoahidiwa Abrahamu? Je, ni vipi tena mataifa yataweza kuokolewa?

*Wagalatia 3:8*

8Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamanai kwamba Mungu atawahesabia haki Mataifa kwa imani, lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema, katika wewe Mataifa yote watabarikiwa.

Je, sisi ni uzao wa Ibrahimu leo? Je, sisi ni uzao wa kiroho wa Israeli? Je, mataifa yote yatabarikiwa kupitia sisi?

Bibilia inatuambia kuwa kazi itasitishwa karibuni kwa haki.

*Warumi 9:27–28*

**27** Isaya naye atoa sauti yake juu ya Israeli, kusema, Hesabu ya wana wa Israeli, ijapokuwa ni kama mchanga wa bahari, ni mabaki yao tu watakaookolewa.:

**28** Kwa maana Bwana atalitekeleza neno lake juu ya nchi, akilimaliza na kulikata

*Warumi 9: 28* ni ya masharti kuhusu ni lini kazi itasitishwa. Ellen White anasimulia jinsi na lini haya yatatukia.

Bwana Mungu wa mbinguni hatatuma juu ya ulimwengu hujumu zake kwa kutotii na kuasi hadi atakapotuma walinzi wake kutoa onyo. Hatafunga kipindi cha upelelezi hadi ujumbe uwe umetangazwa bayana. Sheria ya Mungu inafaa kutukuzwa; madai yake yawasilishwa katika ukweli na utakatifu wake, ili watu waletwe katika maamuzi ya kukubali au kuipinga ile kweli. **Hata hivyo, kazi itasitishwa katika haki. Ujumbe wa haki ya Kristo ni kutangaza kutoka upande mmoja wa dunia hadi mwisho wa dunia kutayarisha njia ya Bwana. Huu ndio utukufu wa Mungu, ambao utafunga kazi ya malaika wa tatu.”[7]**

---

[7] Ellen White, *Testimonies for the Church*, Vol. 6: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1901,) 19.

## Maswali ya Kuzingatia

1. Je, majukumu ya wachungaji kama yanavyoainishwa na Mungu katika Bibilia ni gani?

2. Je, ni majukumu gani ambayo umepewa wewe au mchungaji wako ambayo yanaweza kuchukuliwa kuwa ni ya ziada?

3. Kando na mchungaji, ni nani ambaye anaweza kupewa hayo majukumu ya ziada? Na je, hii itaathiri vipi kanisa lako?

# Sura ya 7

## Ni Nani Atatoa Huduma ya Uchungaji kwa Makanisa Yaliyopo?

Japo sura ya 5 iliangazia suali la iwapo washiriki wanaweza kupoteza wokovu wao ikiwa wachungaji wao wangepewa majukumu ya kuanzisha makanisa mapya badala ya kuhudumia makanisa yaliyopo, haikutoa maelezo mengi kuhusu namna makanisa yangepokea huduma za wachungaji bila ya kuwa na wachungaji. Ikiwa wahudumu watakuwa kwingine wakianzisha makanisa mapya, ni nani atakayewajibikia kuyatunza makanisa? Ni nani atakayesimamia makanisa ikiwa wahudumu hawatakuwepo?

Kutoka kwa *General Conference Bulletin*, Machi 30, 1903, Ellen White anaandika, “Tunapoona kile Mungu anaweza na atatutendea, tunapofahamu kuwa kanisa lake ndilo jambo kuu kwake katika ulimwengu huu, kwa nini hatuko tayari kuliamini Neno lake?”. [1]

Mungu analipenda kanisa lake na ana mpango wa utunzaji wake, mpango ule ule uliomo katika maandiko na katika maandishi ya Ellen White. Kanisa la mungu sharti liwe na wachungaji. Mungu anawapenda waliookolewa sawia na waliopotea. Anawapenda washiriki walioko kanisani sawia na wale ambao bado hawajapata kusikia habari njema. Hataliacha kanisa lake pasipo walezi. Lakini hao walezi ni akina nani?

Maandishi ya Mtume Paulo yanafundisha sana kuhusu suala hili. Paulo ndiye mfano katika maandiko wa kuigwa na mchungaji wa leo katika kazi ya huduma. Paulo alitumia muda wake mwingi kuanzisha makanisa katika maeneo ambayo hapo awali hayakuwa na makanisa. Huku akitumia wakati wake na haya makanisa mapya akiyaelekeza kuhusu utenda kazi, kamwe (kama tulivyoona) hakuwatumikia kama mchungaji wao kwa kipindi cha maana cha wakati.

Ili kuelewa mpango wa Mungu wa utunzaji wa makanisa, tunahitaji kutazama namna Agano Jipya linavyotumia baadhi ya misamiati. Angalia maneno yafuatayo yanayopatikana katika toleo la *King James,* na mashina ya maneno ya Kiyunani ambayo yametafsiriwa kutoka kwayo.

1. Maneno haya matatu (mhudumu, mchungaji, na malisho), hutokana na mzizi wa neno la Kigiriki *"poimen.*"

2. Maneno haya mawili (Simamia na askofu), hutokana na mzizi wa neno la Kigiriki *episkopos*.

3. Neno “mzee” linatokana na mzizi wa neno la Kigiriki *"presbuteros*."

Baadhi ya maneno ya Kiyunani na ya Kiingereza, huwa na mfumo wa nomino na kitenzi.

[1] Ellen White, *The General Conference Bulletin*, March 30, 1903, page 10, par. 1.

Kwa mfano, tunaweza kusema: “wachungaji (nomino) wanaweza kuchunga (kitenzi) makanisa,” au “wakulima (nomino) wanaweza kulima (kitenzi) mashamba (nomino) yao.” Tutaangalia mafungu kadhaa ili kufahamu mpango ambao Roho Mtakatifu ametoa kwa utunzaji wa makanisa. Kwa tathmini nzuri na kamilifu ya mafungu haya ya maneno, nitakuelekeza kwa kazi ya Mchungaji Blake Jones, katika karatasi yake iliyowasilishwa kwa Jumuiya ya Kitheolojia ya Waadventista, Novemba 22, 2014, ijulikanayo kama: *Mtume au Mzee? Hitaji Muhimu la Kufafanua Jukumu la Wachungaji wa Kiadventista.*” Karatasi yake ilikuwa baraka kwangu katika kuyafahamu haya mafungu zaidi. [2]

*Ephesians 4:11–12*

11Yeye ndiye aliyewapa watu vipawa, wengine kuwa mitume, wengine kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji (*poimenas*) na walimu;

12wapate kuwatayarisha watu wa Mungu kwa kazi za huduma, kwa ajili ya kujenga kanisa, ambalo ni mwili wa Kristo:

Katika *Waefeso 4:11*, neno la Kiyunani la "wachungaji," ni *poimenas*, wingi wa nomino *poimen*. *Poimen* ni mzizi wa neno na huweza kutumiak kama nomino (umoja au wingi), au kama kitenzi, kutegemea jinsi linavyoandikwa. Kama nomino, linapatikana mara 18 katika Agano Jipya la Kigiriki: mara 15 linatafsiriwa kwa umoja kama “mchungaji,” na mara moja tu katika wingi kama “wachungaji.” Katika muundo wa kitenzi, *poimaino*, linapatikana mara 11: mara 4 limetafsiriwa kama “tawala,” na mara saba limetafsiriwa kama “lisha,” “alishaye,” au anayelisha.”

*Waefeso 4:11*, ndio wakati tu limetafsiriwa kama “wachungaji” na hutumika kuwatambua watendakazi wa kanisa. Hata hivyo, katika Waefeso, majukumu ya wachungaji hayajafafanuliwa. Ili kujifunza kuhusu majukumu haya, hatuna budi kuangalia mafungu mengine, ambamo muundo wa kitenzi, *poimaino*, hutumika katika kurejelea watendakazi wa kanisa.

Kuna sehemu mbili tu ambapo muundo wa kitenzi, *poimaino*, unatumika mintarafu majukumu ya watendakazi wa kanisa.

Katika *Matendo ya Mitume 20:17 na 28* tunapata kwamba ni wazee (*presbuteros*), ambao wamefanywa na Roho Mtakatifu kuwa wasimamizi (*episkopos*) wa makanisa, nao wanastahili kulisha (*poimaino*) kanisa la Mungu.

*Matendo ya Mitume 20:17 na 28*

17Paulo akiwa Mileto, alituma ujumbe kwenda Efeso kuwaita wazee (*presbuteros*) wa kanisa wakutane naye.

---

[2] Blake Jones, *An Apostle or Elder? The Critical Need to Define the Adventist Ministers’ Role,* November 22, 2014. This is a paper which was presented to the Adventist Theological Society on November 22, 2014. The author, Blake Jones, can be contacted at blakejones123@gmail.com

[28]Jilindeni nafsi zenu, na mlinde kundi lote la kondoo ambalo Roho Mtakatifu ameliweka chini ya uongozi (*episkopos*) wenu, mtunze (*poimaino*) kanisa la Mungu ambalo amelinunua kwa damu ya Mwanae.

Vivyo hivyo, katika 1 Petro 5:1-3, Tunaona kuwa ni wazee (presbuteros) ambao wanasimamia makanisa na kuyatunza (poimaino) makundi kwa hiari.

*1 Petro 5:1–3*

[1]Ninawasihi wazee (*presbuteros*) waliomo miongoni mwenu, nikiwa mzee mwenzenu na shahidi wa mateso ya Kristo na mshiriki katika utukufu utakaofunuliwa:

[2]Lichungeni (*poimaino*) kundi la Mungu mlilokabidhiwa, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari, si kwa tamaa ya fedha bali kwa moyo wenu wote;

[3]Msijifanye mabwana wakubwa kwa wale mnaowachunga bali muwe vielelezo kwa kundi hilo.

Katika *Matendo ya Mitume 14:23,* tunaona kuwa ni wazee (*presbuteros*) waliowekewa mikono katika kila kanisa.

*Matendo ya Mitume 14:23*

[23]Na baada ya kuwachagulia wazee (*presbuteros*} viongozi katika kila kanisa, wakawakabidhi kwa Bwana waliyemwamini kwa maombi na kufunga.

Katika *Tito 1:5-7,* tunaona kwamba Paulo aliagiza kwamba wazee wawekewe mikono katika kila mji. Sifa za wazee pia zimeorodheshwa. Tunaona kuwa neno "Askofu" linatumia mbadala na mzee. Mzizi wa Kiyunani wa neno 'Askofu' ni nomino 'episkopos', lenye maana ya 'kiongozi', inayotumika pia katika Matendo ya Mitume 20:28 "ameliweka chini ya uongozi wenu." *Episkopos* pia lina muundo wa kitenzi, *episkopeo,* lenye maana ya kuongoza au kuchukua uongozi, na limetumika pia katika 1 Petro 5:2 "lichungeni."

*Titus 1:5–7*

[5]Nilikuacha huko Krete kusudi urekebishe mambo yote yaliyokuwa hayakunyooka, na uchague wazee (*presbuteros*) wa kanisa katika kila mji, kama nilivyokuagiza:

[6]Mzee wa kanisa asiwe na lawama yoyote; awe mume wa mke mmoja; awe ni mtu ambaye watoto wake ni waamini na wala sio jeuri au wasiotii.

[7]Kwa kuwa askofu (*episkopos*) amekabidhiwa kazi ya Mungu, anapaswa kuwa mtu asiye na lawama. Asiwe mwenye majivuno, mwepesi wa hasara, mlevi, mgomvi, wala asiwe mtu mwenye tamaa ya mapato yasiyokuwa halali.

"Itaonekana kuwa jambo la kushangaza kuwa na ofisi tofauti iliyojitenga, ambayo haijawahi kutajwa kabla au baadaye katika Agano Jipya, ambayo kazi yake ni kuchunga

kanisa, ilhali jukumu la kuchunga kanisa lilisemekana kwingineko kuwa jukumu la wazee."[3]

J. N. Loughborough alikuw mmoja wa waanzilishi wa Uadventista wa awali. Alimuona Ellen White katika njozi za umma kumliko mtu mwingine yeyote isipokuwa muwewe, James White. Katika mwaka wa 1907, alichapisha kitabu kijulikanacho kama *"The Church: Its Organization, Order and Discipline."* Kitabu hiki kilitumika kwa miaka mingi kama mwongozo wa kanisa hadi mwongoz rasmi ulipopitishwa mnamo.[4] Katika kitabu hicho mwandishi alisema, "Neno mchungaji linatokana na *poimen*, nalo lina maana ya mchungaji mifugo halisi, mchungaji na hasa kanisani, mwalimu, na kiongozi wa kiroho waa kanisa fulani. Ufafanuzi wa neno hili unaonyesha kuwa linaashiria ofisi sawa na ile ya*presbuteros* (mzee), na *episcopos* (askofu), ofisi ya mtaani iliyoambatanishwa na kanisa maalum."[5]

Katika Agano Jipya, mtu ambaye ni mzee wa kanisa ameteuliwa na Roho Mtakatifu kuwa mwangalizi wa kanisa la mtaani. Mzee ni sawa na mchungaji wa siku hizi ambaye hajasomea uchungaji.

Katika siku za mwanzo za Kanisa la Kiadventista, kwa kutumia mpango wa Biblia wa huduma kama unavyoainishwa katika Agano Jipya, kasi ya ukuaji wa dhehebu letu ilikuwa ya ajabu. Madhehebu mengine yaliajabia kukua kwetu kwa kasi. Tulikuwa na mafundisho ambayo hayakupendeza wengi, siku ya ibada isiyo maarufu, na changamoto nyingine nyingi ambazo hazikuwepo kwa makanisa mengine, na bado tulizidi kukua kwa kasi kuwaliko. Sababu ya kukua kwetu kwa kasi ilikuwa rahisi. Wazee walikuwa wakisimamia makanisa yaliyokuwepo, hali iliyowapa wachungaji uwezo wa kuingia mijini na maeneo ambayo hayakuwa na Uadventista, huku wakianzisha makanisa mapya. Makanisa yaliyokuwepo yangeeneza Injili katika maeneo yao, chini ya uongozi wa wazee. Roho Mtakatifu aliyatunza makanisa yaliyokuwepo kwa kuwatumia wazee kama wachungaji, na Kristo akwa mhudumu wao huku wazee na washiriki wakijitolea kwa bidii kuongoa roho.

Baadaye katika kitabu hiki, utaona ni jinsi gani kasi ya ukuaji ilipungua, hususan baada ya mwaka wa 1932. Huo ndio wakati mabadiliko rasmi yalifanywa kuhusu aina ya kazi ambazo wachungaji walitarajiwa kufanya.

*Testimonies to Ministers and Gospel Workers,* kurasa 305-307, pana mfano wa matarajio ya marais wa kimaeneo, wazee na mashemasi kuelekea mwishoni mwa miaka ya 1800. Huku Ellen White akiwa Cooranbong, Australia, aliandika yafuatayo mnamo Septemba 10, 1896.

"Marais wengi wa kimaeneo huwa hawatekelezi majukumu yao – kuhakikisha kuwa wazee na mashemasi wa makanisa wanafanya kazi zao makanisani, kwa kuhakikisha kuwa zaka kamili imeletwa kwenye hazina…Marais wa kimaeneo, fanyeni kazi yenu; msinene yaliyo yenu, bali

---

[3] Blake Jones, *An Apostle or Elder? The Critical Need to Define the Adventist Ministers' Role,* November 22, 2014. This is a paper presented to the Adventist Theological Society on November 22, 2014. The author, Blake Jones, can be contacted at blakejones123@gmail.com

[4] The ***OFFICIAL*** Ellen G. White Website http://www.whiteestate.org/pioneer/loughborough.asp

[5] J.N. Loughborough, *The Church: Its Organization, Order and Discipline* (Washington, D.C., Review and Herald Publishing Association, 1907) p. 129, paragraph 2.

kwa wazi "Asema Bwana Mungu." Wazee wa makanisa, fanyeni kazi yenu. Nendeni nyumba hadi nyumba, ili kundi la Mungu lisipuuze jambo hili kubwa, linalohusu baraka au laana. [6]

Ni rahisi kuona kuwa mpango wa Biblia ulikuwepo. Marais wa kimaeneo walistahili kuwajibikisha wazee na mashemasi kukusanya zaka na sadaka. Hii iliruhusu wachungaji kwenda na kufungua makanisa katika maeneo ambayo hayakuwa yamepata kusikia ujumbe wa Malaika wa Tatu. Wazee wa makanisa yaliyopo walihudumu kama wachungaji wasiohitimu na wasiolipwa mshahara leo. Walikuwa wahudumu wa matembezi kuliko wa leo. Wachungaji walianzisha makanisa mapya na kisha kuhamia maeneo mageni ili kuanzisha makanisa mengine mapya. Kwa sababu wachungaji walikuwa wa kutembea sana, ilikuwa muhimu kwamba mfumo wa zaka na sadaka utumike kuwalipa wachungaji. Hawangeweza kukaa katika eneo moja kwa muda mrefu ya na kuwa na kazi ya mara kwa mara kama ilivyokuwa kwa wazee wa kanisa.

Ni jambo la kuvutia kuwa hata katika masuala ya nidhamu, wazee waliwajibika kama wachungaji wa leo. Mnamo 1880, Ellen White alitoa ushauri kwa makanisa kuhusu namna ya kutekeleza nidhamu kanisani. Katika sehemu moja ya ushauri huo, kunaonyeshwa uhusiano uliopo baina ya wazee wa kanisa na mashemasi na marais wa kimaeneo. "Makanisa machanga yanaweza kuwa na viongozi katika wazee na mashemasi waliochaguliwa ili kuutwika mzigo na kujali ufanisi wa kanisa, ila wasiwe wepesi kwa mtazamo wao binafsi na majukumu kuyaondoa majina katika sajili ya kanisa. Wasis na bidii sana ya kufanya maamuzi mazito kama hayo. Wanapaswa kuwasiliana na aliyeteuliwa kama rais wa eneo lao, na kushauriana naye." Tafadhali ikumbukwe kwamba hakuna mahali pametajwa kuwa mchungaji aitwe aache shughuli za uinjilisti na kufungua makanisa, aje kutatua maswala ya kinidhamu katika makanisa yaliyopo.

Kwingineko anazungumzia umakinifu katika uchaguzi wa wazee na mashemasi, kwani wataaminiwa na kundi la Mungu. "Bwana aangazie mawazo na mioyo ya wote wanaohusishwa na kazi takatifu ya Mungu, umuhimu wa kubainisha ikiwa wale ambao watahudumu kama mashemasi na wazee ni watu wanaofaa kuaminiwa kundi la Mungu."[7]

W. H. Branson alisema vyema katika *The Ministry, Volume 4, Number 1, January 1931*, "Mwokozi mwenyewe alituwekea mfano. Tunamwona akienda kutoka jiji moja hadi jingine, akifunza katika mitaa yenye watu wengi, milimani na kwenye pwani, wala hatumwoni popote akiwa ametulia kama mchungaji wa sinagogi. Tunamwona Mtume Paulo akienda nchi hata nchi, akiwateua wazee katika kila kanisa na kuwahudumia waumini, ila yeye mwenyewe akikaza mwendo kuelekea maeneo mapya na kupanda bango la ukweli katika maeneo mapya."[8]

Wakati uo huo, washiriki walipaswa kuwa wakifanya nini? Mungu ana mwelekeo maalum kwa washiriki kanisani. Kristo ameahidi baraka maalum kwa washiriki wanaofanya kazi kuongozo roho zilizopotea.

"Ikiwa watu wetu wangezihudumia roho zinazohitaji msaada wao, wao wenyewe wangehudumiwa na Mchungaji Mkuuu, na maelfu yanayozunguka jangwani yangefurahi zizini.

---

[6] Ellen White, *Testimonies to Ministers and Gospel Worker:* (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1923,) 305.

[7] Ellen White, *Manuscript Releases*, Vol. 21: (Silver Spring, MD: Ellen G. White Estate, 1990,) 3.

[8] W. H. Branson, *The Ministry*, Volume 4, Number 1, January 1931, page 10.

Badala ya kuzembea miongoni mwa watu wetu, kila roho iende kuwatafuta waliopotea. Kila roho ifanye kazi, sio kwa kuwatembelea washiriki wenza, bali kwa kuzuru maeneo yenye giza duniani, ambako hakuna makanisa.“[9]

Ikiwa una ujasiri kwa Yesu na uondokee starehe zako kwenda kuwatafuta waliopotea, Yesu atakuwa mhudumu wako. Atakuwa mchungaji wako. Sio wakati wote Mungu huwachagua wale ambao tayari wan sifa nyingi zinazohitajika. Ingawa tunapaswa kutia bidii ili kufuzu, hilo silo alitakalo Mungu zaidi. Anaweza kukutendea yale ambayo huwezi kujitendea ikiwa utajisalimisha kwake kikamilifu. Anaweza kukupa msaada na sifa zote unazohitaji ili kumtumikia, ikiwa uko tayari kufuata uongozi wake, kuuliza na kukubali maagizo na mwongozo wa Roho Mtakatifu, na kujitoa kwake kikamilifu kila siku. Lakini cha kusikitisha, bado hatujashirikiana na Mungu jinsi tunavyopaswa. Matokeo yake ni kuwa roho nyingi bado zinapotea siku baada ya siku.

Katika *Luka 10:2* Yesu alisema, “Mavuno ni mengi lakini wafanya kazi ni wachache, kwa hiyo mwombeni Bwana wa mavuno awapeleke wavunaji zaidi katika shamba lake.” Hakusema tuombee wafanya kazi watumwe kwa wale ambao tayari wamevunwa.

Leo hii, Mungu anatafuta watu kama Isaya, “Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.” Isaya 6:8. Isaya hakuwa na sifa zote zinazohitajika kufanya kazi yake. Mungu hakuwa anatafuta mtu mwenye ustadi wote muhimu. Alikuwa akitafuta mtu aliyekuwa tayari kutumiwa na Mungu, abadilishwe na Mungu, na siku baada ya siku ahitimishwe na Mungu, atengenezwe na kufinyangwa na Roho wake Mtakatifu.

Je, Mungu anakuita leo? Je, anakutafuta ukiri, “Mimi hapa, nitume.”

### Maswali ya Kuzingatia

1. Je, tutawezaje kueneza ujumbe wa Malaika wa 3 haraka zaidi?
2. Je, makanisa yanayosimamiwa na wazee yatatusaidiaje kueneza ujumbe wetu haraka zaidi?
3. Wakati wa kuchagua wazee na mashemasi, ni nini kinachomfanya mtu afae kufanya hizi kazi? Kumbuka kuwa Biblia ina jawabu la hili pia.
4. Ni nini kinachomstahisha mwumini kushiriki ukweli na wengine? Ni nini huwazuia?
5. Ni nini hukuzuia?
6. Je, wewe binafsi, unawezaje kuzishinda changamoto hizi ili uweze kushiriki vyema zaidi habari njema ya Yesu?
7. Je, unafikiri ni kwa sababu gani, kasi ya ukuaji wa kanisa letu na washiriki huongezeka zaidi wachungaji wanapokuwa ziarani kuhudumu?

[9] Ellen White, *The Review and Herald*, June 25, 1895 par. 6.

# Sura ya 8

## Asili ya Mfumo wa Huduma wa Kiprotestanti

Ni rahisi kuona kwamba mfumo wa huduma tunaotumia leo hii katika maeneo mengi ya ulimwengu sio sawa na ule uliotumiwa na mitume na Waadventista wa awali. Leo, katika sehemu kubwa ya ulimwengu, wachungaji wa Kiadventista wanawajibikia makanisa yaliyopo badala ya kuwaachia wazee wayasimamie makanisa. Wachungaji wa mengi ya makanisa mengine ya kiprotestanti wanatumia mfumo uo huo. Je, asili ya mfumo unaotumiwa na makanisa ya kiprotestanti ni gani?

Siku moja nikiwa nimemtembelea shemasi katika mahali pake pa biashara, mojawapo ya mada yetu katika mazungumzo ilikuwa: je, asili ya mfumo wa huduma tunaotumia leo ni gani? Kabla ya kuwa Mwaadventista wa Sabato, shemasi huyo alikuwa amelelewa kama Mkatoliki wa Kiroma, na alikuwa amehudumu kama mvulana wa altare utotoni mwake. Naye alitoa maoni yaliyonivutia. Ninaamini kuwa Mungu alimwongoza katika kutoa maoni yake. Alisema, "Lazima liwe ni jambo la Kikatoliki." Nilikuwa na ensaiklopidia ya Kikatoliki kwenye kompyuta yangu, na kwa hivyo nikaichunguza na kupata asili ya mfumo wa huduma wa Kiprotestanti.

Katika karne ya 16, wakati wa Matengenezo ya Kiprotestanti, Kanisa Katoliki la Roma lilikuwa na wasiwasi kufuatia kuhama kwa washiriki wake waliojiunga na makanisa ya Matengenezo. Martin Luther na wenzake walikuwa wamefanya kazi nzuri katika kujenga msingi wa madhehebu mengi ya Kiprotestanti. Martin Luther alifariki mnamo 1546, lakini athari ya kazi yake iliishi katika historia yote. Wengine walifuata nyayo zake na ukweli wa Biblia, na wangali wanafanya hivyo hata sasa.

Kanisa Katoliki la Kirumi lililazimika kushughulikia changamoto ya Matengenezo ya Kiprotestanti, na likaishughulikia katika kile kinachojulikana kama Baraza la Trenti. Baraza la Trenti halikuwa kikao kimoja tu, bali msururu wa vikao 25 kwa kipindi cha zaidi ya miaka 18, kuanzia Desemba 1545 hadi Desemba 1563. Katika kikao cha 24, kilichokongamana Novemba 1563, habari ifuatayo ilichapishwa na inapatikana hata sasa katika Ensaiklopidia ya Kikatoliki.

Ufafanuzi wa neno "mchungaji," na majukumu ya mchungaji ni kama ifuatavyo:

"Mchungaji. Hili neno linaashiria kuhani ambaye ana <u>tiba ya mioyo</u> (*cura animarum*), yaani, ambaye kwa sababu ya ofisi yake, anawajibika kukuza hali ya kiroho ya waumini kwa njia ya kuhubiri…

Baraza la Trenti (Sess. XXIV, cap. xiii, de Ref.) inaionyesha kuwa ndiyo mawazo ya kanisa kwamba kadiri iwezekanavyo, dayosisi zigawanywe katika parokia za kisheria (taz. Parokia),

zinazosimamiwa na mapadre wa kudumu katika parokia…Kando na Wachungaji kuwa na haki, pia wana majukumu. Lazima wahubiri na kutunza mafundisho ya kidini kwa waumini." [10]

**"Dayosisi", katika madhehebu ya Kikatoliki na Kiprotestanti, ni eneo la kijiografia. "parokia ya kisheria" ni kikundi cha makanisa ambacho kinasimamiwa na kuhani au mchungaji. Kwa kulinganisha, Waadventista hutumia neno 'eneo au konfarensi' kurejelea eneo la kijiografia, na 'wilaya ya uchungaji' katika kurejelea kikundi cha makanisa yanayosimamiwa na mchungaji.**

Mapadri wa parokia walitakiwa kusimamia kwa makini washiriki wa Kanisa Katoliki, ambao tayari walikuwa waaminifu, wasije wakageukia makanisa ya Matengenezo. Mapadri walipaswa kufanya kila lililowezekana kuhakikisha kuwa waumini wao hawabanduki, bali wanasalia katika Kanisa Katoliki. Ingawa mfumo huu wa huduma ulianza zamani sana kabla ya Baraza la Trenti kuundwa (pengine karne ya pili, Baada ya Kifo), Baraza hilo lilibainisha wazi wazi majukumu ya mapadri wa parokia. Hapo mbeleni, mapadri walitagusana kibinafsi kidogo sana na waumini, kando na wakati wa Misa za Jumapili. Misa zilihudhuriwa zaidi na matajiri, huku waumini maskini wakishiriki kwa nadra. Aidha, kazi ya padri wa parokia haikuhusisha sana uenezaji wa injili kwa wale ambao kamwe hawakuwahi kuisikia. Kwa kweli, mfumo huu haukuwa na juhudi zozote za uinjilisti, hata! Ndiyo maana mtume Paulo hakuutumia mfumo huo. Aidha, kanisa la awali la Kiadventista halikuutumia mfumo huo. Ellen White hakuutetea mfumo huo. Badala yake, alionya vikali na kushauri dhidi yake. Mfumo huo, ambao kwa karne nyingi ulihusishwa na kanisa Katoliki, ulipigia debe wazo la washiriki kuwategemea makuhani kwa hali zao za kiroho, badala ya kuwahamasisha kukua kiroho kupitia ibada za kibinafsi na mafunzo ya Biblia. Mfumo wa awali wa Kiadventistat ulikuwa tofauti: ulikuwa kama ule mfumo wa kitume uliotumiwa na mtume Paulo.

Wakati wa Matengenezo, Waprotestanti walijiondoa na Kanisa Katoliki la Roma kwa sababu ya kanuni za Biblia. Wakati huo, Waprotestanti walidumisha mfumo wa kuwa na wachungaji wa kulipwa mishahara ili kusimamia washiriki na hali zao za kiroho. Karne chache baada ya Mageuzi ya Kiprotestanti, wachungaji wa awali wa Kiadventista walikuwa na haraka kubwa ya kueneza Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa kasi. Hili lilihitaji mfumo bora wa huduma – mfumo wa Biblia unaopatikana katika Agano Jipya. Baada ya kuhubiri na kufungua makanisa mapya, wachungaji walikuwa wakiwawekea mikono wazee wa makanisa wayatunze makanisa mapya. Kisha, wachungaji wangeenda mahali kwingine kuendelea kuhubiri na kuanzisha makanisa zaidi mahali ambapo Ujumbe wa Malaika wa Tatu haujawahi kuhubiriwa.

Tulipofuata mfano wa mtume Paulo na kurudia mashauri na maonyo ya Ellen White, kanisa letu liliongezeka kwa kasi. Madhehebu mengine yaliajabia ukuaji wetu. Wakati wa miaka ya mwisho mwisho ya maisha ya Ellen White, kuna wachungaji wa kudumu walioteuliwa kusimamia makanisa makubwa bila kuhamahama, lakini hatua hii ilikuwa kando na sheria ya ya kuwapa wachungaji maeneo ya kuhubiri na kufungua makanisa mapya. Alipokuwa angali hai, alishauri mara kwa mara huku akionya dhidi ya kuwa na wachungaji wanaosimamia makanisa yaliyopo bila kwenda nje kuhubiri. Baada ya kifo chake, desturi ya kuwa na wahudumu wa makazi iliongezeka kwa kasi. Katika mwaka wa 1932, Mwongozo wa kwanza wa kanisa la

[10] Catholic Encyclopedia, vol. 11, page 537. Copyright 1911, by Robert Appleton Company, Copyright 1913, by The Encyclopedia Press, Inc

Kiadventista ulichapishwa, na majukumu rasmi ya wachungaji yakabadilika.[11] Wachungaji waliidhinishwa rasmi kutumika kama wachungaji wa makazi, na kwa jumla ukuaji wa kanisa ulipungua sana kwa kipindi cha wakati. Mfumo wetu wa huduma ukazidi kufanan na ule uliotumika na makanisa mengine ya Kiprotestanti. Kwa sababu hiyo, kila kitu kilichotabiriwa na dada White kama matokeo ya wachungaji kubakia makanisani kikawa uhalisia. Mengi ya makanisa yetu leo hii ni dhaifu na katika hali ya kupungua. Vijana hawapatikani katika makanisa mengi. Makanisa yanadai huduma za wachungaji wa kulipwa ili kuwahudumia. Baadhi ya makanisa katika mataifa yaliyoendelea yako hali mahututi. Kinyume na ilivyokuwa, wachungaji hawako huru kwenda kuanzisha makanisa katika maeneo mageni, na wakazi wa maeneo hayo wamesalia kutofahamu ukweli wa siku ya mwisho.

Katika barua iliyoandikwa mnamo Mei 15, 1980, Mzee D. A. Delafield, Katibu Msaidizi katika Jumuiya ya Ellen G. White, alimwandikia Mchungaji Jere Webb, akimpa majibu ya maswali kadhaa aliyokuwa ameuliza. Swali mojawawapo liliangazia chimbuko la dhana ya kila kanisa kuwa na mchungaji wake. Mzee Delafield alijibu vifuatavyo: "Kuhusu suali la kwanza, sijawahi kuona hoja ya kila kanisa likiwa na mchungaji wake ikiungwa mkono - -yaani, katika ukuaji wa historia ya kanisa la Kiadventista. Nafikiri wazo hili limeingia kwetu kutoka kwa makanisa ya kipentekoste, ambako kila kanisa hupewa mchungaji wake pasipo kujali ukubwa wa hilo kanisa. Katika makanisa ya kipentekoste, na hasa yenye ulegevu wa misimamo ya kimaadili, nadhani dhana ya kuwa kila kanisa liwe na mchungaji wake imepelekea jaribio la kutosheleza hilo hitaji. Ili kuwa na hakika ya iwapo tunajadili kanisa la Kiadventista au makanisa mengine, itakuwa muhimu ikiwa mpango kama huo utatolewa. Ila nafikiri kuwa mfumo wa Agano Jipya wa wazee wa makanisa kuteuliwa katika kila kanisa, ni mpango wa Mungu unaofaa kutolewa kwa wazee wa kanisa, kusudi wachungaji wapate nafasi ya uinjilisti na kuanzisha makanisa mapya."[12]


Mtazamo wa haraka wa data utaonyesha namna kasi ya ukuaji wa makanisa na washiriki Kaskazini mwa Marekani ilipungua kadiri mtindo wa mahubiri ulivyobadilika. Kutoka 1863 hadi 1932, kipindi cha miaka 69, tulitumia mtindo wa uinjilisti wa Biblia, kama unavyopatikana katika Agano Jipya. Kutoka mwaka wa 1932 na kuendelea, tukaiga mtindo tofauti wa huduma, sawia na ule wa madhehebu mengine ya kiprotestanti. Kabla ya kutathmini ulinganisho wa kasi ya ukuaji, kuna haja ya kusema jambo. Kanisa la Waadventista wa Sabato halina mfumo wa uongozi wa kiimla kwa wasimamizi wake, wachungaji, au makanisa. Vikao vya Ukanda Mkuu huhudhuriwa na wajumbe wapiga kura kutoka maeneo yote ulimwenguni. Wajumbe rasmi hujumuisha wafanyakazi wa kanisa na washiriki wanaowakilisha maeneo mbalimbali duniani. Mabadiliko yaliyopelekea tofauti za utendakazi wa wachungaji hayakutokana na Rais yeyote, wala kikao chochote cha Ukanda Mkuu. Mwanzoni, mabadiliko hayo yalitokea hatua kwa hatua, huku washiriki na wafanyakazi wa kanisa wakiachana na mfumo wa kitume, na ushauri wa Ellen White.


---

[11] General Conference of Seventh-day Adventists, *Church Manual:* (Washington, DC: General Conference of Seventh-day Adventists, 1932,) 23.

[12] D. A. Delafield, *Letter to Pastor Jere Webb*: May 15, 1980. (Ellen G. White Estate: Washington, DC.)

**Kaskazini mwa Marekani – Kulinganisha Viwango vya Ukuaji wa Makanisa na Washiriki, kutoka mwaka wa 1863 hadi 1932, na kutoka 1932 hadi 2017.**[13]





---


[13] Information for the statistics used for the colored graphs can be obtained from the following documents:

2018 Adventist Statistical Report

1932 Statistical Report of Seventh-day Adventist Conferences, Missions, and Institutions

General Conference Yearly Statistics from 1863 to 1900




Kadiri lengo la uinjilisti na kufungua makanisa katika maeneo mapya lilivyobadilika na kuwa uwepo wa wachungaji wa kusimamia makanisa yaliyopo, kiwango chetu cha ukuaji katika ubatizo na makanisa mapya kilipungua ajabu.

## Maswali ya Kuzingatia

1. Katika sura ya 8 ulijifunza kuwa wazo la kuwa la wachungaji wa makazi lilitokana na mfumo wa Kikatoliki wa padri wa parokia wala hakuna wazo lolote kama hilo lenye msingi wa mafunzo ya Kiadventista - mbona basi tunazidi kushikilia mfumo huu wa huduma?

2. Je, kuna faida gani kwendelea kuwa na wachungaji wa makazi?

3. Rejelea swali la pili. Kwa nini faida hizo zisipatikane kupitia kwa wazee wa kanisa?

4. Rejelea tena swali la pili. Ni yepi kati ya mahitaji hayo ambayo twapaswa kuwa tukimtegemea Mungu, badala ya wachungaji, wazee na mashemasi – ambao ni wanadamu?

5. Je, tunaweza kupata faida gani ikiwa tutamtegemea Mungu kwa mahitaji yote yaliyotajwa katika maswali ya hapo juu?

# Sura ya 9

## Athari ya Kutotumia Mfumo Asili wa Kiadventista katika Uinjilisti

Kama ilivyoonekana katika sura iliyopita, mfumo wa huduma katika Kanisa la Waadventista wa Sabato umebadilika tangu kuanzishwa kwa dhehebu letu. Hapo mwanzo, kanisa lilichochewa na uinjilisti, na shughuli za wachungaji zilidhihirisha hilo. Waumini waliishi kwa wokovu wa waliopotea. Kwa wakati huo, kanisa halikuwa na mpango wowote wa kuwa na wachungaji wa makazi kwa makanisa yaliyokuwapo. Kazi yao ilikuwa kufungua makanisa mapya na kufanya uinjilisti katika maeneo ambayo hayakuwa na makanisa ya Kiadventista, wakiyawekea msingi wa Ujumbe wa Malaika wa Tatu. Kisha, wachungaji wangehamia maeneo mageni, na kufanya vivyo hivyo. Makanisa yaliyoanzishwa yalikuwa yakisimamiwa na wazee wa kanisa waliochaguliwa. Ulikuwa wakati ambao kanisa la Kiadventista liliiga mfumo wa kanisa la kipentekoste. Makanisa mengi mageni yalianzishwa, na kwa jumla ukuaji wa kanisa la Kiadventista ukaongezeka.

Tangu miaka hiyo ya awali, mabadiliko mengi yamefanywa katika orodha ya majukumu ya wachungaji wa Kiadventista. Ellen White alisema: "Kumekuwa na kuhubiri kwingi katika makanisa yeut, kiasi kwamba yamepoteza ladha ya huduma ya uinjilisti. Wakati umewadia wa kubadilisha utaratibu. Hebu mchungaji awahusishe waumini wake kumsaidia katika majukumu ya nyumba hadi nyumba, katika kueneza kweli ya injili katika maeneo ya mbali. Hebu wote washirikiane na hekima ya mbingu katika kuieneza kweli kwa wengine. — The *Review and Herald*, Juni 11, 1895."[1] Japo kumekuwa na ari mpya ya kuanzisha makanisa katika siku za hivi karibuni, pia kumekuwa na juhudi nyingi (muda, nguvu na rasilimali) miongoni mwa wachungaji katika kudhibitisha makanisa yaliyopo. Ukweli wa mambo ni kuwa hizi juhudi za kurekebisha makanisa yaliyopo hazizai matunda. Ellen White alionya dhidi ya wachungaji kutumia muda wao kurekebisha makanisa.

Ellen White anaandika katika *Testimonies for the Church*, volume 7, ukurasa wa 18 na 19:

"**Mungu hajawapa wachungaji kazi ya kuyaweka makanisa sawa. Pindi kazi hiyo imalizikapo, hurudiwa mara tena.** Hivyo basi, washiriki wanaolindwa na kutunzwa huishia kuwa dhaifu kidini. Ikiwa asilimia 90 ya juhudi zinazowekwa kwa wanaoifahamu kweli ingetumika kwa wasioifahamu kweli, je, si kazi ya Mungu ingeendelea zaidi ajabu! **Mungu amezuia mibaraka yake kwa sababu watu wake hawajafanya kazi kulingana na maelekezo yake.**

"Inawalemaza wanaoifahamu kweli kuona wachungaji wetu wakitumia muda na talanta zao kuwahudumia badala ya kuwafikia wale ambao hawajamkubali Kristo. Katika mengi ya

---

[1] Ellen White, *Welfare Ministry:* (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1952,) 110.

makanisa yetu ya mijini, mchungaji huhubiri Sabaato baada ya Sabato, nao washiriki huja kanisani Sabato baada ya Sabato bila ushuhuda wa mibaraka waliyopokea kwa sababu ya kuwatolea wengine mibaraka. Kwa wiki nzima hawajatimiza maagizo waliyopokea Sabato iliyotangulia. Almuradi washiriki hawana juhudi zozote katika kuwalisha wengine neno walilopokea, lazima kutakuwa na ulemavu mkubwa wa kiroho."[2]

Hili limekuwa likiendelea Marekani ya Kaskazini sawia na maeneo mengine mengi ulimwenguni. Hatua zimepigwa kutoka kwa mfumo wa kitume katika Kanisa la Kiadventista la zamani hadi mfumo unaoshuhudiwa sasa, katika makanisa ambayo yanazidi kutegemea zaidi huduma za mchungaji na asili ya uumini. Hatua nyingi zimepigwa katika kuuondokea mfumo wa kitume katika huduma hadi pale tulipo sasa. Tutakuwa tukiangazia sita kati ya hatua hizo, lakini kwanza tujifunze kuhusu mawazo ya kitume ya Waadventista wa awali, kama inavyodhihirishwa katika maandishi ya Ellen White na viongozi wa awali wa Kiadventista.

## Mawazo ya Kitume, Waadventista wa Awali

Pengine mojawapo ya nukuu za kuvutia zaidi kutoka kwa Ellen White kuhusu mada hii ni pale anaposema wazi kuwa wachungaji hawapaswi kuwa na wilaya za makanisa yaliyopo. Tuliona hilo dondoo katika sura ya sita, lakini hebu tuangalie sentensi chache zinazofuatia. "Wachungaji wetu hawapaswi kuzunguka makanisa, wakiyachukulia makanisa kuwa majukumu yao maalum. Nayo makanisa yetu hayafai kuona wivu na kuhisi yametelekezwa ikiwa hayatapokea huduma za mchungaji. Wao wenyewe wanapaswa kujitwika mzigo na kutumika kwa bidii ili kuokoa roho. Waumini wanastahili kuwa imara ndani ya Kristo, ili wazae matunda kwa utukufu wa mbingu. Kama mtu mmoja, wanastahili kujitahidi kuafikia jambo moja, -kuokoa roho.[3]

Makanisa yaliyopo hayakupaswa kuwa lengo la mchungaji, bali yalipaswa kuwa na lengo la kutimizwa na mchungaji – uanzishaji wa makanisa mapya. Baada ya wazee na mashemasi kuchaguliwa kutunza kanisa jipya, mchungaji angeondoka kwenda kuanzisha kanisa jipya kwingineko.

Katika siku za mwanzo kabisa za harakati za Kiadventista, mara nyingi wachungaji walifanya kazi bila fedha za kutosha. Walizoea kuwa wahamiaji, wakienda sehemu mbalimbali bila familia zao kwa muda mwingi kila mwaka. Dondoo lifuatalo limenukuliwa kutoka ujumbe uliotolewa na mzee James White katika Kikao cha Ukanda Mkuu huko *Battle Creek, Michigan*, kilichofanyika mnamo Juni 3-6, 1859.

"Hatuna wachungaji wa makazi kwa makanisa yetu; lakini wachungaji wetu wote ni wamishonari, kama walivyokuwa wahudumu wa awali wa Yesu Kristo, na kwa sababu hiyo wakati mwingi wanakosa fursa ya kukaa nyumbani. Kwa ajili ya Kristo, na kwa wokovu wa wanadamu wenzao, wanajinyima starehe ya kukaa na wenzi wao, na kwenda katika ulimwengu baridi wenye ubinafsi, na kuzitesa nafsi zao katika kuihubiri kweli ya isiyo maarufu ya Biblia. Mungu awabariki! Hata hivyo, lazima wadumishwe, na Mungu amefanya iwe jukumu la kanisa

---

[2] Ellen White, *Testimonies for the Church*, Vol. 7: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1855,) 18-19.

[3] Ellen White, *Australasian Union Conference Record,* August 1, 1902, par. 7.

kuwasaidia, wanapoendelea na huduma yao ya upendo… Huku kanisa likiwa na kazi kubwa mbele yake, muda uliosalia wa kuikamilisha lazima ni mfupi. Matukio ya mwisho ya unabii yanatimizwa, na maonyo ya mwisho yanatolewa kwa kanisa… Wachungaji wetu sharti waonekane kuwa waangalifu katika gharama zao na wenye kujitolea zaidi kwa kazi zao. **Wengi wao huhubiri kati ya mada mbili na mia tatu kila mwaka.** Na inasikitisha kuwa mara kwa mara wanapitia mateso, kutojaliwa, na kujinyima kwa sababu ya ukosefu wa namna." [4]

Katika *Signs of the Times,* jarida la kushuhudia, lilichapishwa kati ya 1874 na 1979. Katika toleo la Disemba 17, 1874, Uriah Smith aliandika makala yenye mada "Waadventista wa Sabato. Ramani Fupi ya Asili yao, Maendeleo na Kanuni." Katika kuelezea namna Waadventista wa Sabato walivyopanga makanisa yao kadiri yalivyoanzishwa, aliandika 'Hii ni rahisi sana. Kikundi cha waumini kiliunganika, wakichukua jina Waadventista wa Sabato, na kuambatisha majina yao na agano la kuzitunza amri za Mungu na imani ya Yesu Kristo. Biblia pekee ndiyo kanuni yao ya imani. Karani huchaguliwa kuzitunza stakabadhi za kanisa, na mzee anayechaguliwa na kanisa, huteuliwa kuyajali maslahi yao ya kiroho. Ikiwa kanisa ni kubwa, shughuli zake ndogo ndogo husimamiwa na shemasi mmoja au wawili, wanaochaguliwa na kanisa kwa shughuli hizi . . . **Hakuna kanisa hata moja huanzishwa na kupewa mchungaji**. Makanisa hayo huendesha shughuli zake za ibada bila kuongozwa na mchungaji, ila tu pengine watembelewe mara kwa mara na mmoja, nao wachungaji wakiachwa huru kutumia muda wao wote kupeleka habari njema kwa wale ambao kamwe hawajapata kuisikia." [5]

Katika kulinganisha tofauti za mbinu za uinjilisti na viwango vya ukuaji kati ya Knisa la Kiadvenista la Baptisti na lile la Waadventista wa Sabato, James White aliandika katika jarida la *Review and Herald,* mnamo Novemba 20, 1879, "Tofauti kubwa zaidi kati ya Waadventista wa Baptisti na Waadventista wa Sabato, ni katika utendakazi wao. Ili wapate kuhurumiwa na kupata faida na upendeleo wa kidini, Waadventista wa Baptisti, katika kipindi cha mapema sana cha historia yao, walijikusanya katika maeneo fulani. Kwa sababu hiyo, ushawishi wao ulimwenguni umekuwa mdogo, na ukuaji wao ni wa kobe…Ukuaji wa Waadventista wa Sabato umekwa wa haraka sana. Kuwepo kwetu kama kanisa lililoratibishwa kulianza mnamo 1860. Hatuna wachungaji wa makazi, lakini kama John Wesley, wachungaji wetu huchukulia ulimwengu mzima kama parokia yao. Wao huenda kila mahali kulihubiri neno la Mungu, na kila mahali wao hupata waumini wapya. Shamba la Bwana ni pana, nao wafanyakazini wachache."[6] Ikumbukwe kuwa Waadventista wa Baptisti wana mizizi yao kule Uingereza kutoka miaka ya 1600. Leo hii, mnamo 2018, washiriki wake si zaidi ya 3000 hadi 4000, pamoja na makanisa 100 nchini Marekani, na washiriki takriban 50,000 kote ulimwenguni, kwa mujibu wa habari zilizopatikana kwa njia ya simu kutoka makao yao makuu duniani. Kwa kulinganisha, Kanisa la Waadventista wa Sabato, ambalo liliratibishwa kuwa dhehebu mnamo 1863, lilikuwa na zadid ya 13,000 (haswa nchini Marekani) mnamo 1879, na zaidi ya 50,000 kote duniani mnamo 1897, wakati ambao James White alikuwa akiandika makala hayo.

[4] James White, *Advent Review and Sabbath Herald,* June 9, 1859, p. 21.

[5] Uriah Smith, *The Signs of the Times*, Volume 1, Number 11, December 17, 1874. p. 84.

[6] James White, *Review and Herald,* Volume 54, Number 21, November 20, 1879. p. 164.

**Suala hilo linaonyeshwa vizuri katika nukuu zifuatazo kutoka kwa Ellen White.**

Mnamo 1855 aliandika, "Wachungaji wetu hawapaswi kutumia muda wao kuwatumikia wale ambao tayari wameikubali kweli. Huku upendo wa Kristo ukiichoma mioyo yao, wanastahili kwenda kuwaleta waliopotea kwa Mkombozi. Kando ya chemchemi zote za maji, yafaa wapande mbegu za ile kweli. Watembee mahali hata mahali; na kanisa hata kanisa liinuliwe. Wanaotangaza msimamo kwa ile kweli wapangwe kama kanisa, kisha mchungaji aendelee na safari hadi maeneo mengine muhimu pia." [7]

Mnamo 1886 aliandika, "Ndugu zangu mlio wachungaji, msikubali kubakia nyumbani mkitumikia meza; msizunguke makanisani mkiwahubiria walioimarika katika imani. Wafunzeni watu kujiangazia nuru, pasipo kuwategemea wachungaji. Wawe na Kristo kama msaidizi wao, wajifunze kusaidiana wao kwa wao, ili mchungaji awe huru kuingia maeneo mageni. Kuna kazi muhimu ya kufanywa duniani. Maeneo mapya yafunguliwe, na bidii na roho ya umishonari iliyodhihirishwa na Kristo inahitajika sana. Laiti nguvu ya Mungu ingeweka kweli katika kila moyo! Laiti wote wangeona haja ya kuwa na uhusiano wa kudumu na Mungu, na wa kuyajua na kuyatenda mapenzi yake siku baada ya siku!" [8]

## Kuangalia hatua 6 zinazohusika katika kuachana na mfumo wa huduma wa Biblia hadi tulipo sasa

### *Hatua #1: Wachungaji walianza kutumia muda mwingi zaidi na makanisa*

Pindi wachungaji walipoanza kutumia muda mwingi na makanisa, muda uliotumika kwa ajili ya lengo la kanisa la kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea ulipungua. Ellen White akaangazia sual hili na jumbe kutoka kwa Mungu. Ifuatayo ni mifano michache ya yale aliyoyaandika.

"Ikiwa wachungaji wangejiondoa; ikiwa wangeenda katika maeneo mapya, washiriki wangelazimika kuchukua majukumu, na uwezo wao ungeongezeka kutokana na kufanyizwa kazi.—Letter 56, 1901.[9]

"Shamba la Bwana ni kubwa zaidi kuliko uwezo wa wafanyakazi waliopo. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba kila mmoja afanye kazi kadiri ya uwezo wake. Yeyote akataaye kufanya hivi, anamdhalilisha Bwana wa shamba, na akisalia mzembe, Bwana atamkataa. Kadiri mwanadamu ajitoleavyo kumtumikia Bwana, ndivyo Mungu hufanya kazi ndani yake na kwa yeye. Mungu anapoona juhudi ndogo kwa kweli zinawekwa katika kuongoa roho katika maeneo ya mbali, anapoona fursa za kipekee zikipotea, na kwamba daktari wa kiroho anatumia nguvu na uwezo wake kuwatumikia walio wazima na kuyapuuza maradhi ya walio katika hatari ya kufa, anaghadhabishwa. Hawezi kusema "vyema sana" kwa kazi kama hiyo; kwa sababu haiharakishi

---

[7] Ellen White, *Testimonies for the Church*, Vol. 7: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1902,) 19-20.

[8] Ellen White, *Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists:* (Basie: Imprimerie Polyglotte, 1886,) 139.

[9] Ellen White, *Evangelism* p. 382, 1946. (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 382.

bali inakawisha maendeleo ya kazi yake, wakati kasi kuu inahitajika zaidi. Muda na nguvu na rasilimali zinatengwa kwa wale wanaoifahamu kweli, badala ya kutumika kuwaelimisha wale wasioijua kweli. Wale wanaofaa kuwatafuta kondoo waliopotea wanayatunza makanisa yetu kana kwamba ni kondoo wagonjwa. Ikiwa watu wetu wangezitumikia roho zinazohitaji usaidizi wao, wao wenyewe wangetumikiwa na Mchungaji Mkuu, na maelfu waliotawanyika jangwani wangefurahi zizini. Badala ya kukaa kwa watu wetu, kila roho iende kufanya kazi ya kutafuta na kuongoa roho zilizopotea. Kila roho na ifanye kazi, sio katika kuwatembelea waumini, lakini katika kuzuru maeneo yaliyogubikwa giza duniani, kusiko na makanisa.*"* [10]

Tafadhali kumbuka kuwa Ellen White aliashiria kuwa washiriki pamoja na wachungaji, walipaswa kufanya kazi na "kutembelea maeneo yaliyogubikwa na giza duniani, kusiko na makanisa."

Mnamo Aprili 15, 1901, katika Kikao cha 34 cha Ukanda Mkuu, huko Battle Creek, Michigan, Ellen White aliwahutubia wachungaji, katika hotuba iitwayo "*An Appeal to Our Ministers."* Katika mazungumzo yake alisema:

"Moyo wangu unasononeka, ninapolitazama shamba na kuona maeneo tasa. Je, hii ina maana gani? Ni nani wanaosimama kama wawakilishi wa Yesu Kristo? Ni nani wanaohisi mzigo kwa ajili ya roho ambazo haziwezi kuipokea kweli hadi itakapoletwa kwao? Wachungaji wetu wanazunguka makanisani, kana kwamba malaika wa rehema hafanyi juhudi katika kuokoa roho.

Mungu anawahesabia lawama wachungaji hawa, kwa roho zilizo gizani. Yeye hakuiti kwenda katika mashamba ambayo hayahitaji tabibu. Anzisheni makanisa yenu mkiwa na ufahamu kuwa yasimtegemee mchungaji kuwasubiri na kuendelea kuwatunza. Wao wanaijua kweli; wanajua kweli ni nini. Wanastahili kuwa imara na kudhibitika sana, ili wapande juu na juu zaidi. Lazima wawe na msingi imara katika imani."[11]

Utagundua kwamba washiriki hawastahili hata kuwangoja wachungaji 'wawasubiri na kuendelea kuwatunza.' Wanastahili kuwa imara peke yao."

***Hatua #2: Tabia ya kuwatuma wachungaji kufanya kazi kwa makanisa ilianza mapema miaka ya 1890, wakati Ellen White alikuwa angali hai. Maagizo yake dhidi ya tabia hii hayakufuatwa.***

Tabia ya kuwapa wachungaji makanisa ya kusimamia ilianza kabla ya kifo cha Ellen white mnamo 1915, licha ya ushauri wake kutoka kwa Mungu dhidi yake. Kuanzia mapema 1895, tunaona katika maandishi yake kuwa makanisa yalikuwa yanaalika watu kufanya kazi katika makanisa, na kwamba maombi hayo yalikuwa yakijibiwa.

"Miji iliyo Marekani, katika taifa hili na mataifa mengine, haishughulikiwi ipasavyo, na bado tunahimizwa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Badala yake, makanisa mengi, kibinafsi na kwa pamoja, yametengwa mbali na Mungu na Roho wake, hata kuziachilia roho za watu kuangamia karibu nao, huku wakizidi kuwaita watu kufanya kazi kanisani. Wamechukua

---

[10] Ellen White, *The Review and Herald*, July 25, 1895, paragraph 6.

[11] Ellen White, *General Conference Bulletin*, Volume 4, Extra Number 12, April 16, 1901, page 267.

kazi hizi, huku wenye dhambi wakiporwa jumbe ambazo Bwana angewapa. Ikiwa kanisa lingekuwa hai na lenye kufanya kazi, washiriki wake wangeugua mioyo kwa ajili ya roho za watu. Washiriki binafsi wangejitahidi kuangaza nuru ya kweli kwa wale ambao bado hawajaifahamu.*”* [12]

Ingawa tabia ya kuwaweka wachungaji kama wasimamizi wa makanisa ilianza wakati Ellen White alikuwa angali hai, ilikuwa na mipaka. Hii inaweza kuonekana kutoka kwa taarifa ifuatayo, iliyoandikwa na Mzee A.G. Daniels, mnamo 1912, ambaye alikuwa Rais wa Ukanda Mkuu kwa wakati huo.

"Kwa kiwango chochote kikubwa bado hatujawaweka wachungaji wetu kuwa wasimamizi wa makanisa. Katika baadhi ya makanisa yaliyo makubwa tuna wachungaji waliochaguliwa, lakini kisheria tumejiweka tayari  kwa kazi za nje, kazi za uinjilisti, na ndugu zetu na dada zetu wamejiweka tayari kudumisha utendakazi wao kanisani, na kuendesha kazi za kanisa bila mchungaji wa makazi. Na ninatumai kuwa hii kamwe haitaacha kuwa desturi ya dhehebu hili**; Kwa maana tunapoacha kazi yetu ya kusonga mbele na kuanza kukaa makanisani, tukifanya kazi zao za kuwaza, kuomba, na zile kazi ziwapasazo kufanya, basi makanisa yetu yataanza kuwa dhaifu, na kupoteza roho na uhai wake, na kisha kupooza, nayo kazi yetu itakuwa hatarini."** [13]

Aliendelea kusema, "Sasa nilipoingia katika huduma, sikuwahi kutarajia kuwa nitafanya kazi nyingine yoyote isipokuwa kuhubiri katika maeneo mapya. Sikuwa na wazo lolote hata kidogo kuhusu kitu kingine chochote. Kamwe halikuniingia akilini wala moyoni mwangu, wala sikuwa na hamu ya kufanya kitu kingine. Nilikuwa na wazo moja, nalo lilikuwa kwenda nje na kuhubiri ujumbe wa malaika wa tatu  kwa watu ambao hawakuujua. Kwa muda mrefu sikuwazia jambo jingine Na kama mtu mwingine yeyote razini, nikaanza kusoma kuhusu njia bora za kufanya kazi hiyo kwa umakini zaidi. Hilo lilinipelekea kusoma kuhusu njia na sera za kazi, namna ya kufanya kazi; na, ndugu zangu nitasema, kwa miaka kumi na miwili au nadhani kumi na mitatu, muda wangu wote ulitumika kwa kile ambacho twaweza kuita kazi ya nyanjani, au uinjilisti. Sikuwa na majukumu ya uongozi wa kimaeneo, au utawala wa namna yoyote. Kazi yangu ilikuwa wakati wote tu ni kulima, kulima na kulima, katika maeneo mapya." [14]

Ingawa hapo mwanzo wachungaji wangetumwa kuyasimamia makanisa makubwa tu, mtindo huo uliendelea kushika kasi. Matokeo yake yalikuwa mabaya. Biblia inasema katika *Wagalatia 5:9*, "Chachu kidogo huchachua donge nzima." Ellen White alipinga peupe uwepo wa wachungaji wa kusimamia makanisa, kwa sababu mazoea haya yangepelekea kupotea kwa roho nyingi na kudhoofika kwa makanisa. Maonyo yake hayakuzingatiwa kwa uzito kama yalivyostahiki.

Baada ya kifo cha Ellen White, kadiri ile chachu ilivyoongezeka, mtindo wa kuwafanya wachungaji kuwa wasimamizi wa makanisa ulianza kuonekana kwa urahisi mapema miaka ya 1920. Kamati ya Ukanda Mkuu ilishtushwa na ukuaji huu wa kasi. Ushahidi wa wasiwasi wao

---

[12] Ellen White, *The Review and Herald*, June 11, 1895, paragraph 4.

[13] A. G. Daniels, *Pacific Union Recorder,* Vol. 11, No. 01, April 4, 1912, paragraph 2.

[14] Ibid., paragraph 6.

ulionekana katika kumbukumbu za mkutano wa Baraza la Kamati ya Ukanda Mkuu. Kumbukumbu za Oktoba 15, 1923, zina ripoti ya kamati yenye mapendekezo 20. Pendekezo la 18 lilisema: "Kwamba tunaangalia kwa hofu ongezeko la desturi ya kuwafanya wachungaji kuwa wasimamizi wa makanisa kama wachungaji wa makazi. Tunazihimiza kamata za kimaeneo zimakinike katika kutathmini hili suala, kwa mtazamo wa kuhimiza uwezo wa kujitegemea na uongozi katika makanisa yetu yote, na kuwaacha wachungaji wote wenye uwezo wawe huru kuanzisha na kuendeleza kazi katika maeneo mapya."[15]

***Hatua #3: Wachungaji walitumwa kwa makanisa yote.***

A. G. Daniels alistaafu kama rais wa Ukanda Mkuu mnamo 1922. Zoezi la kuwatuma wachungaji kuyasimamia makanisa lilishika kasi kadiri muda ulivyosonga. Licha ya maonyo ya mara kwa mara kutoka kwa viongozi wa kidini na Ellen White, makanisa yalizidi kung'ang'ania wachungaji wa makazi, nao wakatimiziwa matakwa yao.

F. M. Wilcox alisema, "Kwa bahati mbaya, kuna mtindo wa wachungaji wa makazi unaozidi kuongezeka katika dhehebu letu, na muda wa wengi wa wachungaji wetu, badala ya kutumika kupeleka habari njema kwa maeneo mapya, unatumika kutatua changamoto za kanisa, na kuwatumikia waume kwa wake ambao wanapaswa kuwa ngome badala ya watu wa kutumikiwa. Hatuwezi kuhisi kuwa huu ni mpango wa Mungu." [16]

G. A. Roberts na W. C. Moffett,[17] walisema katika *Review and Herald,* Novemba 11, 1926, "Kuna mtindo unaozidi kushika kasi wa kuwafunga wachungaji kama wahudumu wa makazi juu ya makanisa Katika kila harakati za mageuzi ya kidini, hii imekuwa mojawapo ya hatua za kwanza zinazopelekea kuoza na kutokua." [18]

Kufikia 1930, mtindo wa kuwapa wachungaji makanisa ya kusimamia ulianza kuwa jambo la kawaida. Hili linaonekana katika makala ya J.L. McElhany ya 1930, akiwa rais wa eneo la Kaskazini mwa Marekani kwa wakati huo.[19] Ilichapishwa katika tole la *Ministry Magazine,* mnamo Januari 1931.

"Je, tutaendelea hivi mwaka baada ya mwaka, tukiyatunza makanisa yetu na kuwa na utepetevu katika kazi ya umishonari, kisha tutazamie kazi hii kukamilika? Kilio kinachoshinikiza makanisa yetu ni usaidizi wa kiuchungaji, na mojawapo ya changamoto zinazowakabili viongozi

[15] General Conference Committee Minutes for 1923, October 15, 1923, page 486.

[16] F. M. Wilcox, "Standing by the Preacher," Review and Herald, June 4, 1925, page 5. F. M. Wilcox was editor of the Review and Herald from 1911 to 1944.

[17] W. C. Moffett was the president of the Southern New England Conference from 1926 to 1928 and president of the Eastern Canadian Union from 1928 to 1932. G. A. Roberts was the Inter-American Division President from 1936 to 1941.

[18] G. A. Roberts and W. C. Moffett, "Building the Home Base," *Review and Herald* (November 11, 1926): page 8.

[19] J. L. McElhany served later as president of the General Conference from 1936 to 1950.

wa kimaeneo ni kuwatuma wachungaji wa makazi katika makanisa yetu. Mtindo huu ni kinyume kabisa na maagizo ya wazi ambayo tumepokea kutoka kwa Roho ya Unabii." [20]

Hapo mwanzo, aghalabu wachungaji wa makazi hawakuwa wanakaa sana katika wilaya zao kabla ya kuhamishwa hadi wilaya mpya, na shughuli ya ubatizo ilipewa kipao mbele. Wachungaji wote walitarajiwa kuendesha shughuli za uinjilisti. Baba-mkwe wangu alipojitosa katika uchungaji mnamo 1939, ingawa alipewa jukumu la kanisa, alitarajiwa kuongoza mkutano wa injili katika mwaka wake wa kwanza, na kuwa na walau mtu mmoja wa kubatizwa, la sivyo aondolewe kwa uchungaji. Leo hii inasikitisha kuwa uinjilisti katika makanisa yetu sio jambo linalosisitizwa kama zamani.

***Hatua #4: Baadhi ya makanisa yakaanza kuhitaji kuwa wanaozingatiwa kuwa wachungaji wawe na sifa fulani maalum.***

Kufikia mwisho wa miaka ya 1960 au mapema 1970, viongozi wa kimaeneo yalianza kuhoji makanisa yangependelea wachungaji wa aina gani kabla ya kuwapa uhamisho kutoka wilaya moja hadi nyingine. Mtindo huu ulizaa ubinafsi katika baadhi ya makanisa. Hivyo, makanisa mengi yakawa ni maeneo-nafsi ya umishonari. Kwa kuyauliza makanisa yangetaka wachungaji wa aina gani, washiriki na wachungaji walipata taswira kuwa utunzaji wa kanisa ni bora zaidi kuliko kuwatafuta waliopotea. Kifungu "Mhubiri wa Injili" kikawa na maana tatanishi. "Wahubiri wa Injili" walikuwa wanatumia muda zaidi kutoa mahubiri kwa watu walioifahamu kweli, na muda mchache zaidi kuwahubiria waliopotea.

***Hatua #5: Wachungaji wakaanza kuhojiwa na makanisa tarajiwa.***

Hatua iliyofuatia ni kwamba makanisa yalitaka yawe na uwezo wa kuwahoji wachungaji kabla ya wao kutumwa na viongozi wa kimaeneo. Hii ilitoa fursa ya makanisa kuchagua mchungaji maalum kama yalivyomtaka, kabla ya mchungaji kutumwa katika kanisa au wilaya. Ikiwa kanisa halingependezwa na mchungaji fulani wakati wa mahojiano, iliwalazimu viongozi wa kimaeneo kutafuta mchungaji mwingine. Katika hali hii, washiriki walimchukulia mchungaji kama mtu wa kuyatimiza mapenzi yao. Mbinu hii inaweza kuathiri malengo ya Mungu kwa kanisa. Uinjilisti unakosa kuzaa matunda, na utunzaji wa makanisa yaliyopo unatiliwa maanani. Viwango vya ubatizo na ukuaji hubakia chini kwa wakati huu, vikilinganishwa na miaka ambayo wachungaji hawakuwa wakipewa makanisa ya kusimamia. Uanzishaji wa makanisa mapya hukupewa kipao mbele kama zamani. Kwa kipindi hiki, namfahamu mchungaji aliyehudumu kwa miaka 20 bila mkutano wa injili hata mmoja, na la ajabu ni kuwa alihesabiwa kuwa mchungaji mwema kwa sababu waumini walimpenda.

***Hatua #6: Huduma ya kitaaluma inayoelekea katika mtindo wa ukusanyikaji inaendelea katika baadhi ya maeneo***

Makanisa sasa yanaanza kuyapa maeneo yao orodha za wachungaji ambao yangependa kuhoji. Wakati mwingine wachungaji wanatuma wasifu wao ili waorodheshwe miongoni mwa wachungaji wanaoweza kuhudumu katika kanisa fulani. Katika hali hii, inakuwa ni vigumu kwa mchungaji kuwa na msimamo kuhusu suala lisilo maarufu. Katika baadhi ya visa, hali ya kiroho inaweza kudorora. Wakati mwingine, waliopotea wanasalia kupotea kwa kuwa lengo la

---

[20] J. L. McElhany, *The Ministry*, Vol. 4, No. 1, January 1931, page 7.

kuwatafuta halizingatiwi ipasavyo. Inaweza kuwa vigumu sana kwa mchungaji mwenye mzigo mzito wa kuokoa waliopotea kufanya kazi katika mazingira kama haya. Mungu amewaita na kuwapa jukumu la kuwaokoa waliopotea, lakini kwa sababu ya kuajiriwa na kanisa wanatazamiwa kutumia muda wao mwingi na waliokolewa. Mchungaji mmoja ninayemfahamu aliuliza katika majadiliano ya kikundi, “Je, uchungaji ni wito au ni taaluma."

Nakumbuka nilipoingia mara ya kwanza katika huduma ya kitaaluma. Hapo awali, nilianzisha makanisa bila kuwa mchungaji mtaalamu, nikichuma mapato yangu kutoka huduma za afya. Nilitumia muda wangu mwingi na watu ambao hawakuijua kweli. Nikaitwa kutoka kuanzisha makanisa kusiko kwa kitaaluma na kupewa kanisa la kusimamia kitaaluma katika wilaya moja ya eneo. Baada ya kuwa katika wilaya hiyo kwa muda, nilijua kuna jambo halikuwa sawa, ila sikuweza kutambua haswa ni jambo lipi kwa wakati huo. Nakumbuka nikimwomba Mungu na kumwuliza kitu kama hiki: Je, nitawezaje kudumisha uhusiano wangu na waliopotea ikiwa nitaendelea kutumia wakati wangu mwingi na washiriki ambao wanaifahamu kweli na tayari wamebatizwa? Kabla ya kuwa mchungaji wa kulipwa, daima nilifanya kazi na kundi lengwa la uinjilisti. Hata hivyo, nilipoajiriwa na kanisa sikuweza kupata muda mwingi wa kukaa na watu waliopotea, ambao walikuwa hawajawahi kuusikia Ujumbe wa Malaika wa Tatu. Sasa ninafahamu fika kuwa huu haukuwa mpango uliokusudiwa na Kristo kwa kanisa. Huu sio mfumo wa Biblia kwa washiriki au wachungaji. Mungu an njia bora.

Ili kufahamu mfumo wa Biblia/Agano jipya kwa waumini na wachungaji wastahili kuwa vipi leo, tunahitaji kuchunguza tena mfumo wa Biblia katika sehemu tatu: uongozi wa kanisa la nyanjani, uchungaji wa kitaaluma, huduma isiyo ya kitaaluma.

### Maswali ya Kuzingatia

1. Ni nini kinahalalisha kwendelea kwetu kutumia wachungaji wa makazi?

2. Je, kuihubiri injili kuna maana gani?

3. Unapofikiria neno mchungaji, je unapata mawazo ya kiongozi wa washiriki au anayeokoa roho zilizopotea?

4. Je, kuhubiri kwa mchungaji kunaathirika vipi anaposumbukia jinsi washiriki watachukulia mahubiri yake?

# Sura ya 10

## Mfumo wa Biblia – Usimamizi wa Kanisa la Nyanjani Leo

Katika Agano Jipya na katika historia ya zamani ya Kiadventista, wazee waliochaguliwa na makanisa walifanya kazi kama vile wachungaji wanavyofanya kazi leo. Pamoja na Biblia, haya yamenakiliwa katika maandishi ya Ellen White, wakiwemo viongozi mashuhuri wa Kiadventista, wachungaji, na waandishi. Hili limeangaziwa katika sura awali za kitabu hiki. Viongozi wengine wa kanisa pia wametajwa katika Agano Jipya, kama vile mashemasi, nk.

Watu waliochaguliwa katika nyadhifa hizi waliteuliwa kwa njia ya uchaguzi na kila mshiriki. Viongozi wa makanisa ya nyanjani – wazee na mashemasi, hawakuteuliwa na mitume wala viongozi huko Yerusalemu. Mitume waliwateua wazee na mashemasi, ambao walikuwa wamechaguliwa na makanisa tofauti. Mtindo huo unastahili kuigwa hata sasa, ikiwa tutafuata mtindo wa Biblia wa kusimamia makanisa ya nyanjani kwa kweli.

Katika *Manuscript Releases*, volume 12, ukurasa wa 284, Ellen White anatoa ushauri kuhusu uteuzi wa viongozi katika makanisa mapya. Mtume aliyejazwa na Roho alisema, "Usimwekee mtu yeyote mikono kwa haraka.'*[1 Timotheo. 5:22]*. Usiwe na haraka ya kutengeneza viongozi, ukiwawekea mikono watu ambao hawajawahi kupimwa na kudhibitishwa. Kanisa na liongozwe kwa jinsi hii: wachache wabadilishane, mmoja akiongoza juma hili na mwingine juma lifuatalo au majuma mawili, na kwa namna hiyo kuwahusisha watu katika utendakazi kanisani; na baada ya kipindi mwafaka cha majaribio, kwa sauti ya kanisa achaguliwe mtu atakayetambuliwa kuwa kiongozi, wala si kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja, au yule yule aendelee ikiwa amekuwa wa baraka kwa kanisa."[21]

Uhusiano baina ya marais wa kimaeneo na wazee wa makanisa ya nyanjani wafaa kuwa kama ule wa marais wa kimaeneo na wachungaji wasio wa kitaaluma, katika maeneo ambayo wachungaji wasio wa kulipwa wanatumika. Katika makanisa ya Agano Jipya na katika makanisa ya mwanzo ya Kiadventista, wazee wa makanisa walikuwa sawa na wachungaji wa leo wasioajiriwa. Kama ilivyotajwa katika sura iliyotangulia, baadhi ya majukumu ya wazee wa kanisa yalikuwa kushughulikia nidhamu kanisani, pamoja na zaka na sadaka.

Katika maandishi ya Ellen White na viongozi wa Kiadventista wa kanisa awali, wachungaji hawakuwa wa makazi. Badala yake, walihusishwa na uinjilisti katika maeneo mageni, wakiwaachia wazee na mashemasi waliochaguliwa kusimamia makanisa yaliyopo. Katika divisheni mbalimbali za kiadventista ulimwenguni ambako njia hii inafuatwa sana, jumla ya ubatizo na makanisa mapya yanayoanzishwa kila mwaka ni ya juu zaidi kuliko zile divisheni ambazo hazitumii mbinu hii. Sura inayofuata ina data ya takwimu inayodhibitisha mtazamo huu.

---

[21]Ellen White, *Manuscript 1-1880*, (February 18, 1880), paragraph 42.

Ikiwa kanisa limebarikiwa kuwa na zaidi ya mzee mmoja, wazee wote wanashiriki mamlaka na majukumu ya kuongoza na kulitunza kanisa. Kama kwingineko kwote, wazee wawili au zaidi ni bora kuliko mmoja. Wazee tofauti watakuwa na talanta mbalimbali, uwezo, maarifa na tajriba za maisha. Ikiwa mzee mmoja atakuwa dhaifu katika sehemu moja ya huduma, mzee mwingine atakuwa na nguvu katika sehemu hiyo. Hata katika makanisa madogo yenye mzee mmoja, kuwatumia mashemasi kwa busara kunaweza kuwa kwa msaada sana katika kulitunza lile kundi na kuwafikia wengine nje. Mfumo wa Biblia unaweza kutoa uongozi uliokamilika, kuliko kuwa na mchungaji mmoja anayesimamia kila kitu. Kwa mtazamo mpana kuhusu jukumu la wazee katika Biblia, tazama utafiti wa P. Damsteegt.[22]

Katika mwongozo wa kanisa la Kiadventista, wazee wanaruhusiwa (kwa ruhusa ya rais wa eneo lao) kufanya mengi ya yale ambayo wachungaji walioteuliwa wanaweza kufanya, ila hawawezi kuwawekea mikono wazee na viongozi wengine, kuunganisha arusi, na kutenga makanisa mapya. Wazee wa makanisa yan nyanjani hawawezi kutumika nje ya maeneo yao, kando na mahali ushirika wao ulipo. Pamoja na hayo, wao hutumika kwa ule mwaka tu ambao wamechaguliwa kufanya kazi. Katika baadhi ya visa, na kwa ruhusa ya rais wa eneo, mzee wa kanisa anaweza kutumikia zaidi ya kanisa moja kwa wakati mmoja. Kwa maelezo zaidi, angalia Mwongozo wa Kanisa la Kiadventista. Hata hivyo, wachungaji waliowekewa mikono wanaweza kufanya majukumu yote ya huduma nje ya wilaya zao, pasipo kuchaguliwa na makanisa ya nyanjani.[23]

Orodha ya sifa za mzee wa kanisa inayopatikana katika 1 Timotheo 3 ni sawa na zile sifa ambazo mtu angependa kuziona kwa mhudumu au mchungaji.

*1 Timotheo 3:1–7*

1 Neno hili ni kweli, kwamba mtu akitaka kuwa askofu, anatamani kazi njema.

2 Basi, askofu awe mtu asiye na lawama. Awe mtu wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtaratibu, mkarimu na ajuaye kufundisha;

3 Asiwe mlevi, wala mgomvi, bali awe mpole; asiwe mbishi wala mtu apendaye fedha;

4 mwenye kusimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu;

5 (Kwa maana kama mtu hawezi kuitawala nyumba yake mwenyewe atawezaje kuliangalia kanisa la Mungu?)

6 Asiwe mtu aliyeongoka karibuni asije akajiona na kuhukumiwa kama Shetani alivyohukumiwa.

7 Kadhalika, awe mwenye sifa njema kati ya watu wa nje ya kanisa, asije akalaumiwa na kuanguka katika mtego wa Shetani.

---

[22] Damsteegt, P. Gerard, "Have Adventists Abandoned the Biblical Model of Leadership of the Local Church?" (2005). *Faculty Publications*. 60. https://digitalcommons.andrews.edu/church-history-pubs/60

[23] The Seventh-day Adventist Church Manual can be downloaded for free at www.adventist.org

Ili kujikumbusha kwamba kuwa na wachungaji wa kitaaluma hakuna msingi wa Biblia, itakuwa muhimu kuangalia sehemu nyingine ya barua (barua ile ile iliyotajwa katika sura iliyopita) iliyoandikwa na D.A. Delafield kwa Mchungaji Jere Webb. "Ukweli wa kazi yetu ni kwamba tuko makini na kuokoa roho. Ole wetu ikiwa hatutahubiri kulingana na Injili. Kusonga mbele, kuna umiliki wa Kiadventista unaozidi nguvu. Hatuwezi kutulia, na kufikiri kuhusu kuwateua wahudumu wa kutwa na kucha, wapate kusimamia makundi madogo. Kazi yao ni kuwaongoza watu wapate kushiriki katika ratiba ya kushuhudia. Hawana lazima ya kukaa kama kuku anayewafunika vifaranga wake wadogo na kuwatia watu joto kwa uwepo wao. Wanastahili kuwafunza watu jinsi ya kujipasha joto kupitia uzoefu wa kazi ya kuokoa roho. Hata hivyo, wazee wateuliwe kwa kila kanisa. Viongozi wasioajiriwa wachukue hatamu ya usimamizi . . ."[24]

Japo makanisa yanatofautiana kwa ukubwa, kanuni za uongozi za Biblia ni zile zile. Licha ya ukubwa wa kanisa na idadi ya wazee, mpango wa Mungu daima ndio bora. Hebu tuangalie mfano unaodhihirisha faida ya kuiga mfano wa Biblia wa usimamizi wa kanisa.

Katika mfano wetu, hebu tuzingatie kanisa lenye washiriki 200 na wazee 6. Wazee hawa si vijana, lakini wamekomaa kwa miaka na tajriba. Wamefanya makosa maishani mwao na kujifunza kwayo. Wana kiasi maishani mwao. Wamewalea wanao na ndoa zao ziko imara. Wanajulikana na kuheshimika kama watu wema katika jamii, wanaotii sheria. Ni wakarimu. Wanawajua washiriki na kulifahamu kanisa lao pia. Kila mzee ana nguvu na talanta tofauti; na kwa pamoja, wanafanikisha usimamizi bora wa kanisa.

**Hapa kuna swali unahitaji kujibu.**

Je, ni heri kuwaruhusu wazee hawa 6 wasimamie kanisa, au itakuwa heri kuruhusu mahafala mgeni au mchungaji mwenye uzoefu mkubwa, aje kusimamia kanisa hili pamoja na wazee? Ni gani bora?

Mungu ana kazi takatifu kwa mahafala wageni ambao wamefuzu karibuni kutoka chuoni, sawia na wachungaji wenye uzoefu, lakini hakuna msingi wa Kibiblia kuwa mchungaji achukue majukumu ya wazee sita, atunze kanisa, na 'kujenga juu ya msingi wa mtu mwingine' (Warumi 15:20). Hakuna msingi wowote wa hili katika Biblia au maandishi ya Ellen White. Kuna ushauri mwingi dhidi yake, lakini hakuna wowote unaounga mkono.

Mbali na hayo, hakuna busara katika kuhitaji mhubiri wa Injili kufanya kazi ambayo Mungu, kwa njia ya Roho Mtakatifu, hususan amewapa wazee wa makanisa (Matedo ya Mitume 20:28). Itakuwa ni kufanya kazi kinyume na maagizo maalum ya Roho Mtakatifu.

[24] Delafield, D. A., *Letter to Pastor Jere Webb*, May 15, 1980, Ellen G. White Estate, Washington, DC.

# Sura ya 11

## Mfumo wa Biblia – Uchungaji wa Kitaaluma Leo

Inastahili kuwekwa wazi kuwa wahubiri wa injili na wachungaji wa makanisa ya nyanjani wana majukumu mawili tofauti. Kwa ufafanuzi, mhudumu ni mtu anayetumwa akiwa na ujumbe – ni mjumbe. Leo hii, wahudumu wa injili wanastahili kuwa katika kiwango cha mitume katika Biblia. Kabla ya lile tukio la njia ya Dameski, Paulo alikuwa mtume wa Wayahudi kabla ya kuokoka. Alikuwa ametumwa na viongozi wa Kiyahudi huko Yerusalemu, kupeleka ujumbe kwa masinagogi ya Dameski. Ujumbe kwa hayo masinagogi ulikuwa wa kuwatesa Wakristo. Alipookolewa na moyo wake kumgeukia Kristo, Paulo akawa mtume wa Kristo. Baada ya hayo, Paulo alitembea huku na kule kwa muda, kwani alitumwa katika maeneo mengi kwa Mataifa, kuwahubiri Injili ya Kristo. Wakati huu, kanisa la Kiadventista halina budi kuipeleka injili kwa wahitaji. Hailipasi kanisa kabisa kuwashikilia wahudumu wa injili kuwatumikia washiriki ambao wameipokea injili tayari.

Waadventista wa Sabato ni wa kipekee miongoni mwa madhehebu ya Kikristo. Mungu ametupa jukumu muhimu zaidi kuliko Wakristo wengine. Wahudumu wetu wanastahili kupeleka Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa wahitaji. Ni muhimu wawe tayari kutembea kuliko wahudumu wa makanisa mengine kwa sababu lazima Ujumbe wa Malaika wa Tatu ufike kote ulimwenguni kabla ya marejeo ya Kristo. Hata hivyo, wachungaji hawatembei. Wao wamewekwa katika maeneo maalum, kuyashughulikia mahitaji na maslahi ya makanisa yaliyoanzishwa. Wachungaji sio "wachungaji wa injili"; wao ni wachungaji wa makanisa ya nyanjani. Japo wanahubiri na kufunza injili, wao hufanya hivyo katika maeneo yanayazunguka makanisa yao.

Kwa nini ni muhimu kuhubiria ulimwengu mzima, hususan Ujumbe wa Malaika wa Tatu? Ujumbewa Malaika wa Tatu una mafunzo ambayo hayapatikani katika madhehebu mengine. Kila mada inayoonekana katika mabango yetu ya uinjilisti, kwa njia moja au nyingine huwa katika muktadha wa Ujumbe wa Malaika wa Tatu. Baadhi ya mifano ni ujumbe wa Sabato, kubadilishwa kwa Sabato, sheria yote ya Mungu, asili ya uovu, na ujumbe wa Danieli 2 na 7. Kweli hizi za Biblia hazipatikani katika makanisa mengine mengi. Hata hivyo, ujumbe wa Patakatifu unapatikana tu katika Kanisa la Waadventista wa Sabato.

Ujumbe wa Patakatifu una ukweli kuhusu hukumu ya upelelezi, ambayo ilianza mnamo 1844 na ingali inaendelea. Sasa hivi, unapokisoma kitabu hiki, watu wengi hawaelewi kuwa wanaweza kupata hukumu ya milele wangali hai. Hatima yao ya milele inaweza kuamuliwa ingawa hawafahamu kabisa kwamba inaendelea. Tutawezaje basi, kuwa washiriki wasiojali, kiasi cha kuwashikilia wahudumu wa injili kuwahubiria waumini wa Kiadventista ambao tayari wanaufahamu huu ukweli, huku mamilioni ya watu wakibakia bial kuonywa kuhusu hukumu ya mwisho wa wakati? Muda unayoyoma mwaka hata mwaka, mwongo baada ya mwongo, kizazi hata kizazi, lakini mamilioni ya watu bado hayajafikiwa na habari hii. Tutawezaje kuishi hivyo? Je, tunaweza hata kudai kuwa tunamtumikia Mkombozi wetu?

Biblia inatupa mifano ya kile ambacho kinatubidi kufanya na jinsi ya kukifanya. Kutoka kwa Ellen White, "Mfano bora zaidi miongoni mwa wale walioitwa kuihubiri Injili ya Kristo ni mtume Paulo, ambaye kwa kila mhudumu ni kielelezo cha uaminifu, kujitolea, na bidii ya mchwa. Uzoefu wake na maagizo yake kuhusu utakatifu wa kazi ya mchungaji, ni msaada na msukumo kwa wote wanaohusika katika huduma ya injili."[25] Ikiwa tunataka kujua mfumo wa Biblia wa huduma ya kitaaluma unastahili kuwa vipi, basi lazima tuchunguze mifano mitatu ya huduma ifuatayo:

1. Huduma ya Yesu alipokuwa hapa duniani.
2. Huduma ya mtume Paulo.
3. Huduma ya waanzilishi wa Kiadventista.

## Huduma ya Yesu Duniani

Tunahitaji kujua ni ambacho Yesu alifanya na pia kile ambacho hakufanya alipohudumu duniani. Kamwe, Yesu hakuwahi kuishi kama mchungaji wa sinagogi. Alihubirini katika masinagogi, lakini lengo lake lilikuwa kuwaelekeza waumini kwake mwenyewe, kama Masihi waliyetarajia. Kimsingi, alikuwa akihubiri ili kuwabadilisha kwa kile ambacho baadaye kingejulikana kama Ukristo.

Yesu alikuwa mtembezi. Mara kwa mara alikuwa akitembea mahali hadi mahali, akiwatafuta waliopotea ili kuwasaidia, kuwaponya, na kuwahubiria. Yesu alifaulu katika kusudi lake la kuwaokoa waliopotea. Hakutumia muda mwingi na wale ambao tayari walikuwa wamemkubali, isipokuwa iwe kwamba walimfuata na kupokea mafunzo kadiri alivyoendelea kuwaokoa waliopotea. Ellen White alikuwa na haya ya kusema kuhusu jinsi Yesu alivyowafunza wanafunzi wake, "Ilikuwa ni kwa mawasiliano na mahusiano ya moja kwa moja Yesu alipata kuwafunza wanafunzi wake. Wakati mwingine aliwafunza akiwa nao milimani; wakati mwingine kando ya bahari, au akitembea nao njiani, akiwafunulia siri za ufalme wa Mungu. **Yesu hakuhubiri jinsi watu wanavyohubiri leo**. Popote mioyo ya watu ilikuwa tayari kupokea ujumbe wa Mungu, aliwafunulia njia ya wokovu. Hakuwaamuru wanafunzi wake akisema fanyeni hivi au vile, bali alisema, "Unifuate." Katika safari zake nchini na mijini, aliandamana nao, wapate kuona jinsi alivyokuwa akifundisha watu. Alifungamanisha haja zake na zao, nao wakaunganika naye katika kazi." Mbinu ya mafunzo ya Yesu kwa wanafunzi wake yaweza kuwa sawa kwa namna fulani na kile kinachojulikana sasa kama "mafunzo kazini,"[26] au unasihi.

Wahubiri wa leo wanaweza pia kutoa mafunzo ya aina hiyo. Katika kampeni za mikutano ya awali ya uinjilisti, Marekani na ughaibuni, nimewahi kutumia mbinu hii ya kutembea pamoja na washiriki, katika hali ya kuwatembelea waliohudhuria mikutano manyumbani mwao. Katika kuendesha gari kuwatembelea wageni wasio Waadventista, mara kwa mara kuna wakati wa kutoa mafunzo na kuwasanihi washiriki wanaoandamana na mhudumu au mwinjilisti. Pia, vikao vay mafunzo maalum kwa washiriki wote walio tayari kuhusishwa na kazi ya uinjilisti ni vya maana sana. Hii inakuza sana uwezo wao wa kuhudumia waumini wengi. Katika hali nyingi, hakuna wahudumu wa kutosha kufanya kazi hii wakati wa kampeni za injili. Nilitumia mbinu hii huko Romania nilipokuwa nikifanya mkutano wa injili katika kanisa mojawapo, wakati

---

[25] Ellen White, *Gospel Workers*: (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 58.

[26] Ellen White, *The Desire of Ages*: (Mountain View, CA.: Pacific Press Publishing Association, 1898,) 152.

mchungaji wao hakuwepo Romania. Mahudhurio yalikuwa makubwa. Nilitumia mkalimani kuwafunza washiriki kuhusu kuwatembelea watu, katika vikao maalum na katika ziara halisi. Matokeo ya kampeni hiyo yalikuwa mibaraka iliyopelekea wengi kubatizwa. Washiriki wasioajiriwa waliwezeshwa kuwa bora katika kuokoa roho. Kuwazuru watu na kutangamana nao ni jambo la muhimu katika kazi ya injili. Japo arafa na mitandao ya kijamii ni faidifu sana katika uinjilisti, hakuna hekima katika kuzichukulia kuwa toshelezi au vibadala vya kuwatembelea watu ana kwa ana.

"Katika kila roho Yesu aliona lazima ya kutoa wito kwa ufalme wake. Alifikia mioyo ya watu akiwaendea kama aliyewatakia mema. Aliwatafuta katika mitaa ya umma, manyumbani mwao, kwenye mitumbwi, katika sinagogi, kandokando ya bahari, na katika karamu ya arusi. Alikutana nao katika shughuli zao za kila siku na kudhirisha hamu katika mambo yao ya kidunia. Alipeleka maagizo yake katika nyumba zao, akiwapelekea uvuvio chini ya dari zao. Huruma yake ya kibinafsi ilifanikisha kuvutia nyoyo."[27]

"Mbinu ya Kristo pekee itatoa ufanisi wa kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alitangamana na watu kama mtu aliyewatakia mema. Aliwaonyesha huruma, akawahudumia, nao wakamwamini. Kisha akawaalika akisema, "Nifuate"[28]

Yesu alisema katika *Marko 2:17,* "Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi." Daktari hawezi kufaulu sana katika kuwatibu wagonjwa, ikiwa mawazo yake yako kwingineko, kando na wagonjwa wake.

Mifano inayopatikana katika huduma ya Kristo, inadhihirisha kuwa Yesu alitumia wakati wake kwa wanadamu waliopotea. Hilo ndilo lilikuwa lengo lake. Wanafunzi wake hawakuwa lengo lake kuu. Badala yake, walipata mafunzo wakiwa kazini, kulenga watu waliopotea kama lilivyokuwa kusudi lake. Kwa hivyo, aliwatuma wapeleke ujumbe wa wokovu hadi miisho ya dunia. Wahudumu wa leo wanastahili kujitahidi kuiga mfano wa huduma ya Kristo.

Katika kufundisha wanafunzi wake, aliwatuma 'wawili kwa wawili' katika maeneo ambayo watu walihitaji kufahamu habari ya wokovu kwa njia ya Yesu. Hakuwa na mazoea ya kumtuma mtu kuhubiri peke yake katika maeneo mbalimbali. Hebu tuangalie mafungu mawili yanayofahamika katika kitabu cha Luka, na tutaona jambo ambalo watu wengi hupuuza.

*Luke 10:1–2*

[1]Baada ya hayo, Yesu akawachagua wafuasi wengine sabini na wawili akawatuma wawili wawili katika kila mji na kila sehemu aliyokusudia kwenda.

[2]Akawaambia, "Mavuno ni mengi lakini wafanya kazi ni wachache, kwa hiyo mwombeni Bwana wa mavuno awapeleke wavunaji zaidi katika shamba lake.

---

[27] Ellen White, *The Desire of Ages*: ((Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1898,) 151.

[28] Ellen White, *The Ministry of Healing*: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1905,) 143.

Yesu alipowatuma wale sabini, aliwatuma “wawili kwa wawili,” na kuwaambia kuwa mavuno ni mengi sana na kwamba wavunaji walikuwa wachache tu. Kisha, akawaagiza waombe wavunaji zaidi. Je, kwa nini Yesu hakuwatuma mmoja mmoja, ili waende mahali maradufu? Aliwatuma “wawili kwa wawili,” kwa sababu wafanyakazi walikuwa wachache. Ikiwa kungekuwa na wafanyakazi wa kutosha, angewatuma kwa makundi makubwa badala ya wawili tu katika kila sehemu. Wawili ndio idadi ndogo zaidi ambayo Mungu anaweza kuidhinisha kwa ajili ya kufanya kazi katika maeneo ambayo hayajafikiwa. Yesu alinena tu yale mambao ambayo yalikuwa yameidhinishwa na Mungu Baba.

*Yohana 8:28-29* inatuambia yafuatayo:

> 28Kwa hiyo Yesu akawaambia, “Mtakaponiinua juu, mim Mwana wa Adamu, ndipo mtakapofahamu ya kuwa, ‘Mimi Ndiye
>
> 29Baba yangu ambaye amenituma yupo pamoja name, hajaniacha; kwa kuwa siku zote nafanya mapenzi yake.”

Kwa kulinganisha *Luka 10:1-2* na *Yohana 8:28-29*, tunajifunza kuwa Yesu hakuwahi kufanya kitu chochote ambacho kilikuwa kinakinzana na Mungu Baba na kile ambacho Baba alikuwa amemfunza. Kutokana na hili, tunaweza kufahamu kuwa Mungu Baba ndiye aliyemwajibiza Yesu kuwatuma wale sabini “wawili kwa wawili,” ingawa kulikuwa na wafanyakazi wachache.

Ellen White anatuambia, “Nimeamriwa kusema kwamba mahali kuna juhudi za kuanzisha kazi ya injili katika maeneo mageni, haipaswi kuwe na **watumishi chini ya wawili** wanaoshirikiana katika huduma. Kristo alipowatuma wanafunzi wake katika ziara za huduma, aliwatuma wawili kwa wawili. Huu ndio mpango wa Bwana.”[29]

Mnamo 1892, Ellen White aliandika, “Je, imekuwaje kwamba tumeiacha mbinu ya kazi iliyoanzishwa na Mwalimu Mkuu? Inakuwaje kwamba wafanyakazi wake sasa hawatumwi wawili kwa wawili? “Oh,” mnasema “hatuna wafanyakazi wa kutosha kufanya kazi shambani.” Basi mmiliki eneo ndogo. Watumeni wafanyakazi katika maeneo ambayo yaelekea mlango umefunguka, na kufundisha ukweli muhimu kwa wakati huu. Je, hatuwezi kuona hekima ya kuwatuma wawili wawili kwenda pamoja kuihubiri injili?”[30]

Katika *Gospel Workers,* ukurasa 481, Ellen White anasema, “Bwana hamtengei mtu yeyote eneo moja maalum la kutumika peke yake. Hii ni kinyume na mpango wake. Amepanga kuwa katika kila sehemu ambayo kweli inatangulizwa, watu wenye mawazo na vipawa tofauti wataletwa ili kutia nguvu ushawishi katika kazi ile. Hakuna mtu mmoja ambaye ana hekima ya kutosha kutimiliza mahitaji ya watu bila usaidizi, na hakuna mtu anastahili kujiona kuwa ana uwezo wa kufanya hivyo. Ukweli kwamba mtu ana uwezo katika sehemu fulani, sio ushahidi kuwa uelewa wake katika mada nyingine zote ni kamili, na kwamba hekima ya mtu tofauti haifai kuunganika na yake.”[31]

---

[29] Ellen White, *Manuscript Releases,* vol. 15: (Washington, D.C.: Ellen G. White Estate, 1986,) 59.

[30] Ellen White, *The Advent Review and Sabbath Herald*, April 19, 1892, first page.

[31] Ellen White, *Advent Review and Sabbath Herald*, April 13, 1886, paragraph 2.

Mtume Paulo anatuambia jinsi Bwana hutoa vipaji vya Roho Mtakatifu kwa watu tofauti. Katika *1 Wakorintho 12:7–11*, anasema:

> "7Roho Mtakatifu hudhihirishwa kwa kila mtu kwa faida ya wote.
>
> 8Maana mtu mmoja hupewa neno la hekima na huyo Roho, na mwingine hupewa neno la ufahamu kutoka kwa Roho huyo huyo;
>
> 9Mtu mwingine hupewa imani na huyo Roho na mwingine karama za kuponya;
>
> 10Huyo huyo Roho humpa mwingine uwezo wa kufanya miujiza, mwingine unabii, mwingine uwezo wa kutofautisha kati ya roho mbalimbali, mwingine aina za lugha na mwingine uwezo wa kutafsiri lugha:
>
> 11Lakini ni Roho huyo huyo mmoja anayefanya haya yote, naye hugawa karama kwa kila mtu, kama yeye mwenyewe apendavyo."

Roho Mtakatifu hampi mtu mmoja vipaji vyote vinavyohitajika kuwafikia watu katika maeneo ambayo hayajaweza kufikiwa.

Mbinu ambayo ilianzishwa na Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu, bado haijabadilishwa tangu enzi ya Yesu Kristo hadi sasa. *Malaki 3:6*, "Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu " *Zaburi 89:34*, "Mimi sitalihalifu agano langu, Sitalibadili neno lililotoka midomoni mwangu."

## Huduma ya Mtume Paulo

Kwa kuwa tayari tumechunguza huduma ya mtume Paulo kwingineko katika kitabu hiki, sehemu hii itaangazia sehemu chache ambazo hazikushughulikiwa hapo awali. Kwa kufanya hivyo, itakuwa muhimu kulinganisha makundi ya kidini katika falme ya Kirumi wakati wa Paulo, na makundi ya kidini ya sasa. Katika siku za mtume Paulo, kulikuwa na aina 3 za makundi ya kidini..

***Makundi ya Kidini katika Falme ya Kirumi Enzi ya Paulo***

1. Kulikuwa na Wakristo wa Mataifa na wa Kiyahudi waliokubali ukweli wote wa Agano la Kale ikiwemo SAbato na amri nyinginezo, pamoja na ukweli kuhusu Kristo kama Mwokozi wao. Kundi hili laweza kulinganishwa vyema na Waadventista wa sasa.
2. Kuna Wayahudi waliokubali ukweli wa Biblia katika Agano la Kale pamoja na Sabato na amri nyinginezo lakini hawakuwa wamekubali ukweli kuhusu Kristo kaam Mwokozi wao.
3. Pia kulikuwa na Mataifa ambao hawakukubali ukweli wa Biblia.

***Makundi ya Kidini ya Sasa***

1. Kuna Wakristo wa Kiadventista wanaokubali ukweli wote wa Biblia.
2. Kuna Wayahudi na Wakristo wa aina nyingine ambao hukubali baadhi ya ukweli, lakini sio ukweli wote wa Biblia.

3. Kuna wengine ambao hawakubali ukweli wa Biblia, labda kwa sababu ya ujinga au kukataa.

Ingawa Paulo alikuwa mtume kwa Mataifa, alikuwa na mazoea ya kuhubiri katika sinagogi kwanza, alipokuwa akiingia maeno mageni. Kwa sababu Wayahudi tayari walikuwa na ufahamu wa Biblia, hakuhitaji muda mwingi wa ziada kuwafunza kanuni zote muhimu na mitindo ya maisha. Alihitaji tu kuwashirikisha ukweli wa Kristo kama Mwokozi wao. Wengine walimkubali Kristo kama Mwokozi wao, na Paulo akaweza kutia nguvu na kuongeza idadi ya wafanyakazi katika maeneo mapya kwa haraka. Mbinu hii ilifanikisha kazi yake na kuwezesha injili kuenea kwa haraka zaidi. Ikiwa Paulo angetumia muda wake wote na Mataifa kwanza, ingemchukua muda mrefu zaidi kupata wafanyakazi wenye maarifa na uwezo wa kumsaidia kueneza injili.

Vivyo hivyo, wahudumu wa Kiadventista wa sasa, wanaoenda katika maeneo ambayo hayajafikiwa na imani ya Kiadventista, wanaweza kufanya vyema ikiwa mara kwa mara watahudhuria ibada za Jumapili (shule za Jumapili) katika madhehebu mengin na kushiriki katika majadiliano.

Kuhusu mbinu ya aina hii, Ellen White alisema, "Wacha baadhi ya wafanyakazi wahudhurie mikutano ya kidini katika makanisa mengine, na kadiri fursa ipatikanavyo, washiriki. Yesu alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili alienda katika shule ya makuhani na walimu katika hekalu na kuwauliza maswali. Katika shule hii ya hekalu, mafunzo yalitolewa kila siku, kama vile tufanyavyo mafundisho ya Biblia. Yesu aliuliza maswali kama mwanafunzi, lakini maswali yake yalizua mambo mapya hata kwa hao makuhani wapate kutafakari. Kazi kama hiyo inaweza kufanywa leo. Vijana wenye busara wanafaa kuhimizwa kuhudhuria mikutano ya Jumuiya ya Vijana wa Kikristo, sio kwa sababu ya kuzua mijadala ya ugomvi, bali kuyachunguza maandiko pamoja nao, na kupendekeza maswali faafu.

"Ikiwa kazi katika sehemu hizi mbalimbali ingefanyika kwa bidii baada ya mikutano yote ya makambi yetu,[32] roho nyingi zaidi zingekusanywa kama zao la mbegu iliyopandwa kwenye makambi." [33]

Mara kwa mara napenda kutembelea Shule za Jumapili. Ninapofika kanisani, huwa najitambulisha kwa anayeniamkua kama mchungaji wa Kiadventista, kisha namfahamisha kuwa mojawapo ya faida za kuhubiri siku ya Jumamosi, ni kwamba hunipa nafasi ya kutembelea makanisa mengine siku ya Jumapili.  Kwa kawaida, hali hii huwatuliza na kuwachekesha. Kisha mimi huhudhuria Shule ya Jumapili na kushiriki katika majadiliano kadiri inapofaa, tena kwa namna isiyozua ugomvi. Huwa napenda kukutana na wachungaji wao na kusali pamoja nao, ili Mungu awaongoze katika utumishi wao. Wakati wowote mchungaji mgeni anapohamia eneo tunamoishi, huwa napenda kumwendea na kumkaribisha mjini, na kusali pamoja naye. Urafiki unakua, na kwa njia hii ubaguzi na upinzani huweza kushindwa au kuepukika.

---

[32] Camp meeting in Ellen White's time were similar to evangelism campaigns today. Churches were often planted from the newly baptized members in these camp meetings.

[33] *Testimonies for the Church*. (1855). (Vol. 6, pp. 74–75). Pacific Press Publishing Association.

Ellen White alisema, "Wafanyakazi wetu wakiingia maeneo mageni, wanastahili kufahamiana na wachungaji wa makanisa kadhaa yaliyoko katika maeneo hayo. Fursa nyingi zimepotea kwa sababu ya kupuuza jambo hili. Ikiwa wahudumu watajiwasilisha kama marafiki na wenye kutagusana, na kudhihirisha kuwa hawaionei haya injili yao, itakuwa na athari chanya, na kuwapa hao wachungaji mtazamo mzuri wa hiyo kweli. Kwa vyovyote vile, ni muhimu kuwapa nafasi ya kuonyesha ukarimu wao ikiwa wangependa kufanya hivyo."[34]

Kwingineko katika kitabu hicho hicho alisema, "Wachungaji wetu wanapaswa kuhusiana kwa karibu na wachungaji wa madhehebu mengine. Kuwaombea na kusali pamoja nao, waombeavyo na Kristo. Jukumu hili takatifu ni lao. Kama wajumbe wa Kristo, tunastahili kuonyesha nia ya dhati kwa hawa wachungaji wa kundi."[35]

Nimealikwa katika makanisa tofauti ya Jumapili ili kufunza katika madarasa ya Shule ya Jumapili. Katika mojawapo, nilifunza ujumbe wa afya kwa majuma mawili. Katika shule nyingine, nilifunza kwa karibu miezi 5 nikiangazia mada za *Danieli 2* na *Danieli 7*, kanuni ya patakatifu, Sabato, na mageuzi ya Sabato. Katika miezi hiyo 5 pia, majuma 13 yalitumika katika kufunza mifano ya Kristo, nikitumia fomu nilizotoa katika kitabu cha Ellen White kiitwacho *Christ's Object Lessons.* Katika fomu hiyo, Alifundisha Upendo, kuna sura 13. Fursa hizi tofauti hazingewezekana kamwe, ikiwa singekuwa na uhusiano mwema na wachungaji hao, pamoa na kuhudhuria Shule zao za Jumapili na ibada za Jumapili wakati mwingine.

Paulo hakusimamia kanisa lolote kwa kipindi kirefu cha wakati baada ya kulianzisha. Hata katika kanisa la kipagani la Efeso, alikaa kwa miaka mitatu tu. Sehemu kubwa ya wakati huo ilitumika katika uinjilisti. Kufaulu kufanya uinjilisti katika maeneo yenye desturi za kipagani kunahitaji muda zaidi kuliko kufanya kaza na watu wenye ufahamu fulani wa Neno la Mungu. Hata hivyo, alipomaliza kazi yake hakuwauliza viongozi waliokuwa huko Yerusalemu kutuma mchungaji wa kulitunza kanisa la Efeso. Badala yake aliwateua wazee wa kanisa waliochaguliwa na waumini. Kisha akawaachia wazee hao jukumu la kulitunza kanisa, chini ya uongozi na maagizo ya Roho Mtakatifu.

Yesu na Paulo walitumia mbinu ya "wawili kwa wawili". Mbinu hiyo bado ni ile iliyotolewa na Mungu itumike na kanisa la masalio, kama inavyodhihirika pia katika maandishi ya Ellen White. Hata mfalme Sulemani, mtu mwenye hekima zaidi duniani, alikiri hivi:

*Mhubiri 4:9–12*

9Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; Maana wapata ijara njema kwa kazi yao.

10Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwingine wa kumwinua!

[34] Ellen White, *Evangelism:* (Washington, D. C: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 143. https://m.egwwritings.org/en/book/30.766?ss=eyJwYXJhbXMiOnsicXVlcnkiOiJldiAxNDMuNCIsImxhbmciOiJlbiJ9LCJzZ19pbmRleCI6IjAifQ%3D%3D#787

[35] Ellen White, *Evangelism:* (Washington, D. C: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 562.

11Tena, wawili wakilala pamoja, hapo watapata moto; lakini mmoja aliye peke yake tu awezaje kuona moto?

12Hata ikiwa mtu aweza kumshinda yule aliye peke yake, wawili watampinga; wala kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi.

Yesu aliwatuma watumishi wake “wawili kwa wawili“ kwa waliopotea; Paulo alienda “wawili wawili“ kuwatumikia waliopotea; Mfalme Sulemani, mtu mwenye hekima zaidi, alisema “Wawili ni bora kuliko mmoja“kwa maana wana thawabu nzuri kwa kazi yao.“; naye Ellen White akaandika kuwa tunahitaji kutuma watumishi “wawili wawili“ kwa waliopotea. Kwa kuwa Yesu, Paulo, Mfalme Sulemani, na Ellen White, wote wanakubaliana, mbona tunajiepusha na kuwatuma ‘wawili wawili‘ kwa waliopotea, badala yake twawatuma peke yao kuwatumikia waumini wa Kiadventista waliobatizwa katika makanisa yaliyoanzishwa?

Kama Yesu, Paulo alikuwa mtembezi wala hakuwa na mpango wa kutulia katika sehemu yoyote kama mchungaji kwa muda mrefu. Kamwe hakukusudia kuchukua usukani katika wilaya ya kanisa baada ya mchungaji mwingine kuondoka. Warumi 15:20-21, “, **kadhalika nikijitahidi kuihubiri Injili, nisihubiri hapo ambapo jina la Kristo limekwisha kutajwa, nisije nikajenga juu ya msingi wa mtu mwingine;** bali kama ilivyoandikwa, wale wasiohubiriwa habari zake wataona, na wale hawajasikia watafahamu.”

Jambo moja ambalo linastahili kufahamika ni kwamba wito wa huduma ya Injili ni wito Mtakatifu, wala sio chaguo la kitaaluma tu. Wito wa huduma ya Injili sio wa mshahara kila wakati. Je, unakumbuka ukisoma kuhusu nyakati ambazo Kristo aliwatuma wanafunzi wake kwenda safari za kimishonari bila pesa, mavazi, n.k?

*Mathayo 10:7–10*

7Na mnapokwenda, hubirini mkisema, “Ufalme wa mbinguni umekaribia;

8Waponyeni wagonjwa, wafufueni wafu, watakaseni wenye ukoma, wafukuzeni pepo, mmepokea bure, toeni bure.

9Msichukue dhahabu, fedha, wala shaba kwenye mishipi yenu ya pesa,

10wala mfuko wa chakula kwa ajili ya safari, wala mavazi mawili, wala viatu, wala fimbo, kwa maana mfanyakazi anastahili chakula chake.

Watu wengine huchukulia sehemu ya mwisho ya mstari wa 10 kumaanisha kuwa unapotumwa kuhudumu, unapaswa kupokea mshahara kutoka kwa ukanda wenu. Hilo laweza kuwa jambo nzuri, ila haliwezi kufanyika kila wakati. Hii ndio maana Paulo alijisimamia kwa kwa kufanya biashara ya kuunda hema. Lakini kuna nyakati zingine huenda ukalazimika kufanya kazi ya uinjilisti bila mapato ya kibiashara, kitaaluma, au kanisa. Tunahitaji kuelewa mstari wa 10 katika muktadha wa mafungu mengine ambapo Yesu anawatuma wanafunzi wake kwenda kuhubiri bila pesa wala msaada wowote wa kifedha. **Hawakuwa wanaenda kuwahubiria waumini katika makanisa yaliyoanzishwa. Walikuwa watunzwe na waliokuwa wameenda kuhudumia, watu wasio Wakristo. Kwamba hupokei mshahara kutoka kwa kanisa**

**haimaanishi kuwa Yesu hajakuita kupeleka Injili katia maeneo ambayo hayajafikiwa na Injili ya Kiadventista. Mungu ana njia nyingi za kukutunza iwe una mshahara au huna.**

“Baba yetu wa mbinguni ana njia nyingi za kutujalia, ambazo hatujui chochote. Wale ambao wanaikubali kanuni moja ya kupatia kazi ya Mungu kipao mbele, wataondokewa na mashaka na njia kunyooka mbele zao.”[36]

Mimi na mke wangu tulipitia aina hiyo ya huduma moja kwa moja, katika juhudi za kuanzisha makanisa. Tulikuwa kama Paulo aliyepata riziki yake kwa kuunda hema. Bila mshahara wa kanisa, tulianzisha makanisa katika eneo geni ambalo hapo awali liliishi Wakatoliki wengi. Kwa wakati mmoja, hata hivyo, sikuweza kupata kazi. Sikuwa na mapato. Tulitunzwa na wale tuliolenga kuhudumia, wasio Waadventista. Siku moja, majirani wasio waadventista walitutembelea wakisema, “Wes, nenda mtandaoni utuonyeshe aina ya *iPad* ambayo ungetaka.” Kwa muda, watu hawa wasiokuwa Waadventista walinipa vitu vingi nilivyotumia katika huduma yangu – *iPad* mpya, *iPhone* mpya, viatu vipya vya Sabato, suti mpya ya kuhubiria Sabato, magurudumu mapya ya gari langu, n.k. Kamwe sikuwahi kuulizia vitu hivi. Wakati mmoja tulitembelewa na mchungaji kutoka nchi nyingine. Tulipokuwa karibu kuondoka mjini kwenda kuzungumza katika vyuo vikuu viwili vya Kiadventista na idhaa ya *3ABN*, jirani mmoja asiye Mwaadventista alikuja kwetu na kusema, “Hapa kuna hundi kwa ajili ya safari yenu.” Hundi hiyo ilikuwa ya $700. Huyo jirani alinipa hela hizo bial mimi kumwomba. Mke wangu naye alipewa chakula cha mchana na wanawake jirani kwa karibu kipindi cha miaka 3, kati ya siku 3 na 5 kila wiki katika mikahawa tofauti; gharama yote ililipwa na wanawake jirani. Walitufanyia hayo yote bila sisi kuulizia. Tukatendewa kama wafalme.

Kuna mchungaji wa Jumapili katika eneo ambalo sasa tunaanzisha kanisa, ambaye husali mara kwa mara katika ibada yake ya Kwanza siku ya Jumapili, kwamba Mungu anibariki na huduma yangu. Kitu cha pekee nilichofanya tu kilikuwa kwenda kwake na kumkaribisha mjini alipoingia hapa mara ya kwanza kutoka parokia nyingine. Nikawa rafiki yake wa dhati. Anakiri kuwa siku ya Jumamosi ndiyo Sabato. Mungu hufanya kazi katika mioyo ya wachungaji wa madhehebu mengine. Tunastahili kutafuta urafiki nao, kuomba nao, na kuwaombea. Mungu hufanya kazi kwa njia za ajabu. Siku moja, hata wachungaji wa madhehebu mengine wataitikia wito na kujiunga na Kanisa la Kiadventista la masalio.

Kwa wale ambao lazima wafanye kazi kama Paulo aliyejikimu kwa kazi ya mikon yake, na kwa wale ambao mara kwa mara hawatakuwa na mshahara wowote, maneno ya Kristo katika *Mathayo 6* ni ya kutia moyo.

*Mathayo 6:11* “Utupe leo mkate wetu wa kila siku.”

Katika sala ya Baba Yetu, tumefundishwa kuomba mkate wetu wa kila siku. Kila siku mwambie Mungu unachohitaji wala usifadhaikie kesho. Zaidi ya hayo, katika mstari wa 31-34 anasema:

---

[36] Ellen White, *The Ministry of Healing:* (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1905,) 481.

*Mathayo 6:31–34*

[31]Msisumbuke, basi, mkisema, ‘Tule nini?‘ Au ‘Tunywe nini?‘ Au ‘Tuvae nini?

[32](Kwa maana mataifa yanatafuta vitu hivi vyote kwa bidii:) Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mnahitaji vitu hivi vyote.

[33]Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.

[34]Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Kila siku ina matatizo yake ya kutosha.

## The Adventist Pioneers’ Ministry

Waanzilishi wa Kiadventista walikuwa Waadventista kwa kuzisoma kweli za Biblia. Muundo wa huduma katika Biblia si ule wa kiprotestanti, ambao una tofauti kidogo zinazoonekana katika karibu makanisa yote yasiyokuwa Katoliki. Waadventista hao walitumia muudno wa Biblia ambao tumekuwa tukizungumzia. Walifanya kazi katika shamba la Bwana kwa njia ile ile iliyotumiwa na Yesu na Paulo. Haya tayari yameelezewa awali katika kitabu hiki. Kuna msemo maarufu nchini Marekani, “Usijaribu kurekebisha kitu ambacho hakijavunjika.” Muundo wa Biblia uliotumiwa na Yesu, mitume, na waadventista wa awali, sio muundo uliovunjika. Hujawahi kuwa na kasoro, wala huna kasoro leo hii. Hakuna haja ya kujaribu kuurekebisha.

Ni kwa nini basi tuliachana na muundo huo, na kutumia zaidi ya karne moja katika kutomtii Mungu? Jaribio letu la muda mrefu katika kutotii limetibuka kabisa! Kuungama na kutubu kunahitajika sasa.

# Sura ya 12

## Mfumo wa Biblia – Huduma ya Wasioajiriwa

Kuna haja ya kurudia nukuu ifuatayo kutoka maandishi ya Ellen White, ambayo yametumika awali katika kitabu hiki:

"Kwa wote wanaoamini, Mungu amewatwika jukumu la kuanzisha makanisa. Lengo maalum la kanisa ni kuelimisha waume kwa wake kutumia uwezo waliopewa kwa manufaa ya ulimwengu, na kwa utukufu wa Mungu. Mungu amewafanya wanadamu kuwa mawakili wake. Wanafaa kutumia talanta walizopewa kuendeleza kazi ya Mungu na kupanua ufalme wake. Makanisa yetu, makubwa kwa madogo, hayastahili kuendeshwa kwa namna ambayo yatategemea usaidizi wa wachungaji. Waumini wanafaa kukomaa katika imani kiasi cha kuwa na maarifa ya kutosha kuwa wamishonari wa kweli. Wanastahili kufuata mfano wa Kristo, wa kuwahudumia walio karibu nao. Kwa uaminifu, watimize nadhiri walizotoa wakati wa ubatizo, kwamba watatimiza mafunzo yatokanayo na maisha ya Kristo. Wanapaswa kushirikiana katika kutetea kanuni za kujikana na kujitolea, ambazo Kristo alizingatia katika ubinadamu alipokuwa akihubiri. Shughuli zote za umishonari huweza kufaulu maarifa ya upendo na huruma za Kristo yanapotolewa."[37]

Ikiwa Mungu mwenyewe ameweka mzigo wa kuanzisha makanisa mapya kwa wote wanaoamini, basi lazima tuamini kuwa mzigo huu ni mwepesi. Yesu alisema katika *Mathayo 11:28-30*, "Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, name nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." Lazima tufuate maagizo yale yale ambayo Musa alimpa Yoshua katika *Kumbukumbu la Torati 31:7-8*. "Kisha Musa akamwita Yoshua na kumwambia hivi mbele ya Israeli wote: "Uwe jasiri na imara, kwa sababu ni wewe utakayewaingiza watu hawa katika nchi ambayo Yehova aliwaapia mababu zao kwamba atawapa, nawe utawapa iwe urithi wao. Yehova ndiye anayepiga mwendo mbele yako, naye ataendelea kuwa pamoja nawe. Hatakutupa wala kukuacha. Usiogope wala usifadhaike." Hatuwezi kushindwa tunapofuata maagizo ya Mungu kwa imani na unyenyekevu kwa sababu "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu." *Zaburi 46:1.*

*Marko 9:23*, "Yesu akamwambia, Mambo yote yanawezekana kwa mtu mwenye imani." Ikiwa tunaamini kwa kweli, tutakuwa na imani. Na tukiwa na imani, itadhihirika kwa maendo yetu kwa sababu **"Imani bila matendo imekufa."** *Yakobo 2:26.* Hata ingawa huna mafunzo yoyote rasmi ya uchungaji kwa sasa, Mungu anaweza kukufunza unaposonga mbele kwa imani.

Kwa waumini wasioajiriwa kuhubirik kuwa na muundo kamili wa Biblia katika huduma, italazimu baadhi ya wachungaji kujiondoa, ili kuwawezesha wasiohitimu kupata uzoefu pasipo waliohitimu. Ellen White alisema, "Ikiwa wahubiri wangejiondoa, waende katika maeneo

[37] Ellen White, *Pacific Union Recorder*, August 1, 1901, Volume 1, page 1, paragraph 7.

mapya, waumini wangelazimika kuchukua majukumu, na kwa kutumika uwezo wao ungeongezeka. — Letter 56, 1901."[38]

Aliandika aya hii ya kuinua sana katika *Review and Herald*, mnamo Juni 9, 1895:

“Mungu amempa ‘kila mtu kazi yake.’ Je, kwa nini wachungaji na viongozi wa kanda mbalimbali hawatambui ukweli huu? Kwa nini hawaonyeshi kutambua usaidizi ambao waumini binafsi wanaweza kutoa? Waumini na waamke. Wachukue nafasi zao ili kuwasaidia wachungaji na wafanyakazi, wakisukuma mbele wito wa kanisa. Hakuna lazima ya kulinganisha talanta za watu. Ikiwa mtu ataijaribisha imani yake, na kutembea na Mungu wake kwa unyenyekevu, anaweza kuwa ana elimu kidogo, akahesabiwa kuwa mnyonge, lakini bado anaweza kutimiza sehemu yake teule sawasawa na mwenye elimu ya juu. Yeye ajitoaye kikamilifu kwa uongeozi wa Roho Mtakatifu huwa katika nafasi bora zaidi ya kumtumikia Mungu kwa njia kubalifu. Mungu atawatia moyo watu wasiotajika kumfanyia kazi. Ikiwa wachungaji na watu wenye ushawishi watajiondoa, na kumruhusu Roho Mtakatifu kutawala mawazo ya waumini wasioajiriwa na kanisa, Mungu atawaelekeza yawapasayo kufanya kwa utukufu wa jina lake. Hebu watu wawe na uhuru wa kutekeleza yale ambayo Roho wa Mungu anadhihirisha .”[39] — *The Review and Herald*, Julai 9, 1895.

Ellen White hata anawaambia washiriki kile watawaambia (kwa heshima) wachungaji ambao wanazunguka katika makanisa yaliyoanzishwa. “Badala ya kuwaweka wachungaji wakifanya kazi kwa makanisa ambayo tayari yanaijua kweli, hebu waumini na waseme kwa hawa watendakazi: ‘Nendeni mkaitumikie mioyo inayoangamia gizani. Sisi wenyewe tutaendesha huduma za kanisa. Tutaisimamia mikutano, na, kwa kukaa ndani ya Kristo, tudumishe hali za kiroho. Tutashughulikia mioyo iliyo kati yetu, na tutatuma sala zetu na zawadi zetu kuwasaidia wachungaji walio katika maeneo yenye umaskini mwingi.’”[40]

Katika mwaka wa 1989, kulikuwa na Waadventista wachache walioishi katika Kaunti ya Fultoni, Penislavania. Hakukuwa na kanisa la Kiadventista katika Kaunti hiyo. Kila wiki wangesafiri wakipitia sehemu ya Kaunti ya Fultoni, kisha kupitia jimbo la Vijinia ya Magharibi ili wafike kanisani. Wakaamua kuanzisha kanisa katika Kaunti ya Fultoni. Lengo lilikuwa kuleta uwepo wa Kiadventista katika Kaunti hiyo; msingi ambao wangetumia kufanya uinjilisti katika eneo hilo.

Kikundi hicho hakikutaka kuwa na mchungaji wa kuwahubiria kila wiki. Walikusudia kushughulikia mahitaji ya kichungaji kwa kufuata mfumo wa Biblia. Wakapanga kufanya uinjilisti wao wenyewe katika Kaunti hiyo, kama Waadventista wa Sabato wenye maarifa. Walitamani kwamba fedha walizotuma kwa ukanda wao kila mwezi zingetumiwa na ukanda wao kuanzisha kanisa lingine katika eneo lingine geni. Hawakutazamia kwamba wangenufaika na zaka na sadaka zao wenyewe.

---

[38] Ellen White, *Evangelism:*(Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1946,) 382.

[39] Ellen White, *Review and Herald*, July 9, 1895, page 434.

[40] Ellen White, *Testimonies for the Church*, Vol. 6: (Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association, 1901,) 30.

Baadhi ya washiriki katika kikundi hicho walipata jengo la kanisa ambalo lilikuwa likiuzwa katika mji uitwao *Needmore.* Mnamo Novemba 1989, kikundi cha misheni kilianzishwa huko *Needmore, Penislvania.* Kikundi hicho kiliendelea kukua hata kuwa kanisa rasmi katika ukanda wa Penislvania. Kanisa hilo linajulikana kama *Kanisa la Waadventista wa Sabato la Needmore.* Jina lake linaashiria kila kitu. Kwamba tunahitaji makanisa zaidi ya Kiadventista katika kila taifa, jimbo, kaunti, parokia, majiji, miji, na vijiji vingi kote ulimwenguni.

Leo hii, ninapoandika kitabu hiki (2019), *Kanisa la Waadventista wa Sabato la Needmore* lingali linaendeshwa kila wiki kama lililoanzishwa na watumishi wasioajiriwa na kanisa, katika eneo ambalo hapo awali hakukuwa na uwepo wa Waadventista wa Sabato. Washiriki wake wangali wanarudisha zaka zao kwa uaminifu kwa ukanda wao, bila kuupoteza muda wa mchungaji wa kitaaluma. Kansia hilo sasa limekuwa na linaendelea kustawi, ingawa liko mashambani.

Tuko kwenye vita dhidi ya Shetani na malaika zake. Jukumu letu ni kuwakomboa wenye dhambi waliopotea. Kila mshiriki anastahili kuwa na shughuli nyingi, ya mno ikiwa ni wokovu wa wenye dhambi waliopotea. Hakuna mtu wa kutohusishwa. Hakuna mtu wa kutengwa na huduma kwa Mungu katika kuwafikia watu wote ulimwenguni na habari njema ya wokovu kwa njia ya Kristo. “Mavungo ni mengi lakini wafanyakazi ni wachache.”[41] Je, wewe ni askari shujaa katika kupigana dhidi ya mpango wa Shetani wa kuangamizwa wote walioumbwa kwa mfano wa Mungu? Au wewe huenda tu kanisani siku ya Sabato, unasikiza mahubiri, kisha taratibu unajiendea zako wiki nzima, bila juhudi zozote za dhati katika kuwakomboa wenye dhambi waliopotea?

Lazima tuwe waangalifu sana. Ikiwa tunaridhishwa na kuhudhuria ibada kanisani tu, na kuwaacha wachungaji waliohitimu kufanya kazi yote ya kukomboa roho za watu huku tukidai mahubiri kila wiki, basi sisi ni watumiaji tu wala sio wazalishaji.

## Ushiriki wa Kila Mshiriki

“Mungu hajaweka jukumu la kuwakomboa wenye dhambi waliopotea kwa wale tu wanaolihubiri Neno. Ametoa kazi hii kwa wote. Maneno, ‘Basi enendeni ulimwenguni kote, na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe,’ yananenwa kwa kila mfuasi wa Kristo. Wote ambao wamewekwa wakfu kwa maisha ya Kristo wanateuliwa kufanya kazi kwa wokovu wa wanadamu wenzao. Tamaa ile ile aliyokuwa nayo ya kuwaokoa waliopotea idhihirike kwao pia. Sio wote wanaoweza kutumika mahali pamoja, lakini kwa kila mmoja wao kuna sehemu na kuna kazi. Kwa wote waliopokea baraka za Munguk wanafaa kujibu kwa huduma halisi; kila kipaji kitumike kwa kuendeleza Ufalme wa Mungu .”[42]

“Karibuni kazi itafungwa. Waumini waaminifu wa kanisa tetezi watakuwa kanisa shindig. Katika kukagua historia yetu ya zamani, baada ya kupiga kila hatua ya kuendeleza msimamo wetu hata tulipo, naweza kusema Bwana Asifiwe! Ninapoangalia matendo ya Mungu, ninajawa na mshangao na ujasiri katika Kristo kama Kiongozi. **Hatuna chochote cha kuogopa katika siku za usoni, isipokuwa tu ikiwa tutasahau namna Bwana ametuongoza, na mafundisho yake katika zama zetu.** Sasa sisi ni watu hodari, ikiwa tutaweka tumaini letu kwa Bwana; kwa kuwa

[41] Luke 10:2

[42] Ellen White, *North Pacific Union Gleaner*, December 4, 1907, page 4.

tunashughulikia kweli za nguvu za neno la Mungu. Tuna kila sababu ya kushukuru. Ikiwa tutaenenda katika nuru inayotuangazia kutoka neno hai la Mungu, tutakuwa na majukumu makubwa yanayolingana na nuru kubwa ambayo Mungu ametupa. Tuna majukumu mengi ya kutekeleza, kwa kuwa tumewekewa amana ya ukweli mtakatifu, wa kutolewa kwa ulimwengu wote katika fahari yake na utukufu wake wote. Sisi ni wadeni kwa Mungu, wa kutumia kila fursa ambayo ametupa kuupamba ukweli wa utakatifu wa tabia, na kutuma maonyo, na faraja, na tumaini na upendo, kwa wote walio katika giza la makosa na dhambi."[43]

Japo ni jambo zuri kufanya kazi ya uinjilisti katika eneo moja mwaka baada ya mwaka, haitoshi. Wala haitatosha hadi pale tutakapotimiza kazi ya kitume ambayo imetolewa na Mungu husussan kwa kanisa la Waadventista wa Sabato. Jukumu la waumini pamoja na wachungaji ni kuupeleka Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa wote wanaoishi katika sayari hii. Haipaswi kuwe na eneo lolote duniani lenye watu, ambalo halijawekewa mikakati maalum ya kuwafikia wakazi wa eneo hilo na Ujumbe wa Malaika wa Tatu. Tunapokuwa wazalishaji badala ya watumiaji katika kazi ya Mungu. Atabariki juhudi zetu, na Yesu atarejea "tukimaliza siri ya Mungu."

[43] Ellen White, *General Conference Daily Bulletin,* January 29, 1893, page 24).

# Sura ya 13

## Mpango wa Mungu Bado Unafanya Kazi Leo

"Katika sehemu ambazo kiwango cha ukweli hakijawahi kushushwa, roho nyingi zitaokolewa kuliko awali, kufuatia juhudi za kiasi kile kile.cha kazi. Bwana Yesu ana nguvu zote mbinguni na duniaani. Ukizitegemea, na kuunganisha nguvu za Mbingu na zako, roho za thamani zitaokolewa. Uwepo wa Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya wote. Kristo, aliye mpatanishi wetu, hutuhuisha tena kwa nguvu za uwepo wake. **Kila mhusika ashirikishwe, sio kwa kuyatumikia makanisa, bali kuwafikia walio katika giza la dhambi**. Roho za watu zikiokolewa, moja kwa moja zihusishe katika kazi . . . Walioongoka karibuni wafunzwe kuwa na ushirika na Kristo, wawe mashahidi wake, na kumtangaza ulimwenguni."[44]

Dhehebu la Kiadventista limekita mizizi kote ulimwenguni. Kanisa hili limegawanywa katika divisheni 14, pamoja na eneo moja la misheni. Kila divisheni, ambayo hujumuisha mataifa mbalimbali, huwa imegawanywa katika Yunioni na Makofarensi. Katika sura hii, tutakuwa tukilinganisha ongezeko la washiriki wapya na makanisa katika divisheni nne kuu ulimwenguni. Takwimu zitajumuisha kipindi cha miaka 12, kuanzia mwishoni mwa 2003 hadi mwisho wa 2015.

1. Ulinganisho utaonyesha tofauti katika viwango vya ukuaji kati ya aina mbili za divisheni:

2. Katika divisehni mbili, wachungaji huwekwa kuwa wasimamizi wa makanisa maalum katika wilaya za kanisa. Hii ndio njia ya kawaida inayotumiwa na kanisa leo
.
3. Katika divisheni zingine mbili, wachungaji hawapewi makanisa ya kusimamia. Badala yake, wanapewa maeneo ya kijiografia ambayo wanasimamia uinjilisti na kuanzisha makanisa mapya. Makanisa yaliyopo husimamiwa na wazee wa makanisa waliochaguliwa katika makanisa yao.

Katika ukanda wa magharibi, tutakuwa tukilinganisha Divisheni ya Marekani ya Kati na Divisheni ya Kusini mwa Marekani. Divisheni hizi mbili zimepakana (majirani) na zinafanana kidemografia. Zinafanana kisiasa, kitamaduni, na hata kiuchumi. Katika Divisheni ya Marekani ya Kati, wachungaji husimamia makanisa maalum. Lakini katika Divisheni ya Kusini mwa Marekani, badala ya wachungaji kupewa wilaya maalum, wachungaji hupewa maeneo ya kijiografia ili wayafanyie uinjilisti na kuanzisha makanisa miongoni mwa watu ambao hawajafikiwa na ile kweli.

Tutafanya ulinganisho kama huo katika divisheni mbili zinazokaribiana na kufanana kidemografia katika bara la Afrika – Divisheni ya Mashariki na Kati ya Afrika, na Divisheni ya Afrika Kusini/Bahari ya Indi. Katika Divisheni ya Mashariki na Kati ya Afrika, wachungaji

[44]Ellen White, *The Advent Review and Sabbath Herald,* July 25, 1895, page 402.

hupewa makanisa maalum wayasimamie. Katika Divisheni ya Afrika Kusini/Bahari ya Indi, wachungaji hutumwa kuhubiri katika maeneo ya kijiografia ambayo hayajafikiwa. Wazee waliochaguliwa katika makanisa yao huyatunza makanisa. Mtindo huu ni sawa na ule unaotumiwa na Divisheni ya Kusini mwa Marekani.

Kwa kulinganisha divisheni ambazo zimepakana na kufanana kidemografia, tunaweza kutathmini ufanisi wa njia hizo mbili za huduma. Tunaweza tukahitimisha kuhusu mbinu za utumishi, pasipo kutatizika na mfumo wa kidemografia. Mbinu ya kimaeneo, ambayo ni ya Kibiblia kama ilivyotumika na mitume na wachungaji asilia wa Kiadventista, inalinganishwa na mbinu ya kuwapa wachungaji makanisa maalum, kama inavyofanyika katika makanisa ya Kiprotestanti.

Katika picha zinazofuata, kuna misamiati ambayo sharti ifafanuliwe. Neno "ufuasi" lina maana ya wale waliobatizwa na kukiri imani. "Ongezeko la makutaniko" ni idadi ya makanisa na kampuni zilizoongezwa kwa divisheni katika kipindi hicho cha miaka 12. "Mishahara ya wachungaji kwa kipindi cha miaka 12" inawakilisha idadi ya wachungaji wanaolipwa mishahara kila mwaka, kwa jumla ya miaka 12. "Washiriki katika ufuasi" ni idadi ya washiriki waliopo kwa kila ubatizo au kukiri kwa imani. Ikiwa kanisa lina washiriki 100 na kubatiza 10 baada ya mkutano wa Injili, basi kanisa hilo litakuwa na washiriki 10 kwa kila 'ufuasi'. Safu za manjano ni zile divisheni, ambazo kazi za wachungaji ni za kimaeneo, ambako wanahusika na uinjilisti na uanzishaji wa makanisa. Usimamizi wa makanisa huwa ni jukumu la wazee wa makanisa na viongozi wengine. Divisheni nyinginezo huwatuma wachungaji kuyasimamia makundi ya makanisa. Ili kupata ramani inayoonyesha zinakopatikana divisheni za Kanisa la Kiadventista ulimwenguni, tembelea http://www.//adventiststatistics.org/ Takwimu iliyotumiwa kuunda jedwali lifuatalo ilipatikana kutoka kwa tovuti hiyo. Wewe pia unaweza kupata habari muhimu za takwimu kutoka kwa tovuti hiyo.

### Ulinganisho wa Ukanda wa Magharibi na Divisheni

| Divisheni | Ongezeko la Ufuasi katika Kipindi cha miaka 12 | Mshahara wa Mchungaji kwa Kila Ongezeko la Ufuasi | Jumla ya Ongezeko Katika Kipindi cha Miaka 12 | Mishahara ya Mchungaji kwa Kipindi cha Miaka 12 | Idadi ya Washiriki kwa Kila Ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|
| Kusini mwa Marekani | 9303 | 4.6 | 2711155 | 43215 | 10.2 |
| Marekani ya Kati | 5638 | 6.6 | 2278030 | 37137 | 16.7 |

Divisheni ya Kusini mwa Marekani inafanana na Divisheni ya Marekani ya Kati kidemografia. Hata hivyo, Divisheni ya Kusini mwa Marekani huwatuma wachungaji kuhubiri na kuanzisha makanisa mapya, katika maeneo ambayo yanahitaji makanisa. Kazi ya kimsingi ya wachungaji hao sio kuyasimamia makanisa yaliyopo, ambayo aghalabu husimamiwa na wazee wa makanisa na mashemasi waliochaguliwa. Divisheni ya Marekani ya Kati huwaweka wachungaji kuyatunza makundi ya makanisa, na wakati mwingine makundi makubwa.

Katika lahajedwali la Ukanda wa Magharibi, kiwango cha ukuaji wa idadi ya washiriki na makanisa mapya kilikuwa juu katika Divisheni ya Kusini mwa Marekani yenye wachungaji wa kimaeneo, kuliko Divisheni ya Marekani ya Kati. Ingawa Divisheni ya Kusini mwa Marekani ilikuwa na asilimia 16 zaidi ya wachungaji walioajiriwa kuliko Divisheni ya Marekani ya Kati, ilikuwa na asilimia 19 zaidi ya ufuasi na asilimia 65 zaidi ya makanisa yaliyoanzishwa. Lengo kuu la Divisheni ya Kusini mwa Marekani lilikuwa uanzishaji wa makanisa. Makanisa mapya yapatayo 3,665 yaliongezwa kuliko Divisheni ya Marekani ya Kati. Divisheni ya Marekani ya Kati, ambayo ilikuwa na wachungaji wa kusimamia makanisa, ilihitaji asilimia 61 zaidi ya washiriki waliopo kwa kila ubatizo au kukiri kwa imani. Mtindo wa kuwateua wachungaji kuyasimamia makanisa yaliyopo haikaribii ile ya wachungaji wa kimaeneo katika kuongoa roho.

## Ulinganisho wa Bara la Afrika na Divisheni

| Divisheni | Ongezeko la Ufuasi Katika Kipindi cha Miaka 12 | Mshahara wa Mchungaji kwa Kila Ongezeko la Ufuasi | Jumla ya Ongezeko Katika Kipindi cha Miaka 12 | Mishahara ya Mchungaji kwa Kipindi cha Miaka 12 | Idadi ya Washiriki kwa Kila Ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|
| **Afrika Kusini-Bahari ya Indi** | **5968** | **2.8** | **2337245** | **16856** | **12.8** |
| **Mashariki na Kati ya Afrika** | **6119** | **4.2** | **2322203** | **25504** | **13.3** |

Katika mfano wa Bara la Afrika, utagundua kwamba Divisheni ya Afrika Kusini/Bahari ya Indi na ile ya Mashariki na Kati ya Afrika zinazokurubiana kidemografia, zilikuwa na ongezeko lililofanana sansa la ufuasi na makanisa mapya. Katika Divisheni ya Afrika Kusini/Bahari ya Indi, uinjilisti ulipewa kipao mbele kuliko uanzishaji wa makanisa. Tofauti ya kimishahara inayohitajika kupata matokeo kama haya katika divisheni hizo mbili ni muhimu sana. Katika kipindi hicho cha miaka 12, Divisheni ya Mashariki na Kati ya Afrika ikiwa na wachungaji waliosimamia makanisa maalum, ilihitaji asilimia 51 zaidi ya wachungaji kuliko Divisheni ya Afrika Kusini/Bahari ya Indi yenye wachungaji wa kimaeneo, ili kufikia matokeo sawa katika ongezeko la washiriki na makanisa mapya.

Kwa ufupi, wachungaji na wahubiri wasioajiriwa wakiruhusiwa kufanya kazi kwa kutumia mbinu za Mungu, wanaweza kuwabatiza watu zaidi na kuanzisha makania mapya zaidi wakitumia fedha kidogo..

## Mifano miwili inayotosha kuzingatiwa

### Misheni ya Mongolia

Mnamo 1990, wamishenari Brad na Cathy Jolly kutoka *Adventist Frontier Missions*, walijitolea kuingina Mongolia kama wamishenari wa kwanza wa Kiadventista katika taifa hilo. Walijitahidi na kuanza kazi bora. Mnamo 1998, mradi huo ulielekezwa kwa Ukanda Mkuu duniani, na kujulikana kama Misheni ya Mongolia.

Mnamo 2016, *It is Written* ilifadhili ziara ya kimatibabu ya meno hadi *Ulan Batol*, mji mkuu wa Mongolia. Niliamua kwenda, lakini kabla ya kuondoka, niliitembelea tovuti ya *Takwimu za Kiadventista*[45] kuangalia takwimu za ukuaji katika misheni hiyo. Nikagundua jambo lililoteka mawazo yangu. Niliona kuwa mnamo 2008, kulikuwa na ongezeko la asilimia 50 ya idadi ya wachungaji waliowekewa mikono ama wenye leseni, lakini mwaka uliofuatia ukuaji wa misheni ulipungua kwa asilimia 50. Hakukuwa na ongezeko lolote la idadi ya makanisa au mashirika ila tu ongezeko la idadi ya wachungaji. Kufikia 2017, kiwango cha ukuaji hakikuwa kimerudia kile cha 2008 au kabla yake.

Nilimpigia simu Katibu Mkuu, Mchungaji Bold Batsukh, kuulizia kuhusu takwimu hizo. Jibu lake lilikuwa la ajabu. Aliashiria kuwa kuongeza idadi ya wahudumu kwa ajili ya makanisa yaliyopo hakukufaidi makanisa, kwa sababu waumini wasioajiriwa na kanisa walitulia bila kushiriki imani yao sana. Ni rahisi sana – kunapokuwa na wachungaji zaidi kwa makanisa yaliyopo, waumini wasioajiriwa hawashuhudii imani yao sana, na kwa hiyo kiwango cha ukuaji hushuka.

Hali hii inaweza kuonekana katika konfarensi nyinginezo na maeneo mengine duniani. Tukio la Mongolia sio la kipekee. Kila kunapokuwa na ongezeko la idadi ya wachungaji kwa kanisa au makundi ya makanisa yaliyopo, kiwango cha ukuaji kinaweza kutarajiwa kushuka kwa mwaka mmoja au miwili, pasipo kurejelea kasi ya ukuaji ya hapo awali. Ikiwa wahudumu watatumwa kuhubiri na kuanzisha makanisa mapya, badala ya kutumika kuongeza idadi ya wahubiri walioko makanisani, ongezeko la wahudumu halitaathiri pakubwa kiwango cha ukuaji katika eneo hilo au konfarensi.

### Eneo la Magharibi mwa Kenya – Mradi wa Elimu

Nilijifunza hadithi ifuatayo kutoka kwa Mzee Peter Kereri, aliyekuwa mwekahazina wa Eneo la Magharibi mwa Kenya kwa wakati huo. Baadaye nilithibitisha masimulizi yake kwa Mzee Christopher Misoi, Rais wa Eneo la *Great Rift Valley Conference*, Mzee John Tuwei –

[45] Spreadsheet Link for the Mongolia statistics http://adventiststatistics.org/stats_y_stats.asp?FieldID=C12034&view=y_stats&StartYear=1998&EndYear=2017&submit=Build+Table.

mkurugenzi wa shughuli za wachungaji wa Konfarensi ya Yunioni ya Magharibi mwa Kenya, na Daniel Bett – Mwalimu Mkuu wa *Shule ya Kingsway Preparatory*, nchini Kenya.

Mnamo 2002, Eneo la Magharibi mwa Kenya lilikuwa na wachungaji 90 waliokuwa wamewekewa mikono na kupata leseni. Karibu asilimia themanini ya wachungaji hao hawakuwa na shahada ya kwanza. Yunioni ya Mashariki mwa Afrika ikashirikiana na Chuo Kikuu cha Baraton kubuni mpango wa elimum ambapo wachungaji waliokuwa wameajiriwa katika maeneo mbalimbali nchini Kenya, wangeenda kusomea shahada ya kwanza ikiwa wangebakia kuajiriwa na kanisa daima. Mara mbili kwa mwaka, wachungaji hao waliruhusiwa kuyaacha makanisa yao, na kwenda Chuoni Baraton kwa miezi kadhaa ili kupata mafunzo yao. Kila mwaka waliyaacha makanisa yao kwa jumla ya takriban miezi mitano. Mpango huo wa elimu ulikusudiwa kuchukua miaka mitano. Kila mchungaji katika Eneo la Magharibi mwa Kenya alikuwa na makanisa karibu 26 kwa wastani katika eneo lake la usimamizi. Wachungaji 34 (karibu asilimia 40) walihusika katika mpango huo wa elimu. John Tuwei na Daniel Bett walikuwa wawili kati ya wanafunzi hao.

Wastani wa miaka minane ya ufuasi (ubatizo na kukiri kwa imani) kabla ya wachungaji hao kuanza mpango huo wa elimu ilikuwa takriban 3400 kila mwaka. Mwaka wa kwanza wale wachungaji 34 kati ya 90 katika Eneo la Magharibi mwa Kenya walipoondoka kwenda kusoma kwa karibu nusu mwaka (2003), idadi ya ufuasi iliongezeka hadi karibu 4200. Mwaka uliofuata, ufuasi ukaongezeka hadi zaidi ya 8100. Mwaka wa tatu, hadi zaidi ya 9300. Ili kuonga takwimu hizo kutoka tovuti ya Takwimu za Kiadventista, bonyeza kiungo hiki kilichoko hapa chini.[46] Waumini wenyewe walitia bidii katika uinjilisti, bila ya kuwepo kwa wachungaji wao. Wachungaji wao waliporejea kwendelea na utumishi wa kudumu, asilimia ya kiwango cha ukuaji ilishuka sana wala hakijawahi kurudia kiwango kile wachungaji walipokuwa hawapo.

Kwa kifupi, makanisa yanaimarika kiafya na kuzalisha zaidi yasipokuwa na wachungaji wa mdua mrefu walioajiriwa kuwasimamia badala ya kuangazia wokovu wa waliopotea.

## Mpango wa Mungu Hujabadilika

Kama Sabato, Mungu hajabadilisha mpango wake wa huduma kama ulivyokuwa siku za mitume. Mpango wake, ambao ni ule uliotumiwa na mtume Paulo, umerudiwa na kufafanuliwa na nabii wa sasa Ellen White. Hakuna kiwango chochote cha mageuzi kitawahi kufanananishwa na mpnago kamili wa Mungu. Hakuna mpango mwingine wowote unaweze kufanikisha uinjilisti kwa haraka. Mipango mingine mbadala hukawisha tu marejeo ya Kristo.

*Malaki 3:6* “Kwa maana mimi ni Yehova; sibadiliki . . .”

*Zaburi 89:34* “Sitavunja agano langu wala kubadili maneno yaliyosemwa na midomo yangu.”

*Hebrews 13:8* “Yesu Kristo ni yule yule jana, leo, na milele.”

Hakuna wakati mzuri wa kurudi kwenye mpango wa Mungu kuliko leo. Kwa nini kuchelewa?

---

[46] Western Kenya Field (Now known as the Great Rift Valley Conference) statistics http://adventiststatistics.org/stats_y_stats.asp?FieldID=C10560&view=y_stats&StartYear=1980&EndYear=2012&submit=Build+Table.

# Sura ya 14

## Wingu Kubwa Zaidi la Mashahidi

Sura ya kumi na moja ya Waebrania inatajwa kama sura ya imani katika Biblia. Inaanza katika *Waebrania 11:1* kwa kusema, “Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Sura hiyo inasimulia jinsi watu mashuhuri walivyoishi kwa imani katika historia yote, kabla ya wakati wa Kristo. Inafuatilia hifadhi ya habari ya wokovu katika maisha ya Abeli, kisha Enoko, Nuhu, Abrahamu na Sara, Isaka, Yakobo, Yusufu, Musa, Rahabu, Gidioni, Baraki, Samsoni, Yefthae, Daudi, Samueli, na kisha kushuhudia watumishi wengine wa Mungu ambao hawajatajwa. Watu hawa waaminifu, waume kwa wake, wakati mwingine walikuwa wakitembea kama watumwa na wafungwa. Walijaribiwa, wakateswa, na hata kuuawakwa kufanya mema tu. Wote waliishi kwa imani wakitazamia wakati Mwokozi atawakomboa wenye dhambi, japo hawakuishi kushuhudia kutimizwa kwa ahadi hiyo. Waliiona tu kwa jicho la imani. Sura ya 11 inaishia kwa maneno haya:

> *Waebrania 11:39–40*
>
> 39 Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ile ahadi:
>
> 40 Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

Katika mstari wa 40, Paulo alikuwa akizungumzia waliokuwa hai wakati wake. Ujio wa Kristo kwa mara ya pili ungekuwa mbali katika siku zijazo, lakini kwa kila kizazi kilichofuatia, ahadi ya wokovu imekuwa ile ile. Tunapozidi kusoma, Waebrania 12 inatoa changamoto sisimuzi kwetu:

> *Waebrania 12:1-2*
>
> 1 Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu,
>
> 2 tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkno wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.

Karibu miaka 2000 iliyopita, Paulo alizungumzia habari ya ‘wingu kubwa la mashahidi.’ Hata hivyo, leo hii, tuna ‘wingu la mashahidi’ kubwa zaidi. Kando na mashahidi wa Agano la Kale waliofahamika kwa Paulo, tuna wengine wengi katika Agano Jipya, pamoja na mashahidi ambao wamekuwepo katika historia ya Ukristo, hadi sasa. Tuna karibu miaka 2000 zaidi ya mashahidi waaminifu – mashahidi waliokuwa waaminifu kwa maagizo ya Mungu na kwa misheni ya Kirsto ya kuwaokoa wenye dhambi waliopotea. Tuna mfano wa Kristo, wanafunzi mitume, na wote waliobakia waaminifu kwa miaka yote ya kipindi cha giza; Waldensia, wanamageuzi, Wamileraiti, waadventista waanzilishi, na zaidi.

Zaidi ya hayo, tuna kipaji cha nabii wa sasa, Ellen White. Maandishi yake yanatusaidia kurejelea Maandiko Matakatifu tunakopata mbinue mwafaka za kumtumikia Mungu – mbinu zilizotolewa na Kristo, Roho Mtakatifu, na mitume. Maandishi yake huangazia masual haya ili tusiwe na vijisababu vyovyote vya kutofuata maagizo ya maalum ya Mungu.

*Ufunuo 14:13* inatuambia, "Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, andika, heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao." Fungu hili linazungumzia habari za wafu, wafanyakazi waaminifu waliopigania kupeleka ujumbe wa kweli katika maeneo mageni. Kazi zao zinadhirika katika maandishi yao. Ellen White alisema katika '*Counsels to Writers and Editors, ukurasa wa 28,' "*Mungu amenipa nuru kuhusu nakala zetu. Nazo ni nini? – amesema kuwa wafu wataongea. Vipi? – matendo yao yafuatana nao. Yatupasa kurudia maneno ya waanzilishi wa matendo yetu, waliofahamu kuwa inagharimu kuitafuta kweli kama hazina iliyofichwa, wakajitahidi kuweka msingi wa matendo yetu. Walisonga hatua kwa hatua chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu. Waanzilishi hawa wanaondoka mmoja baada ya mwingine. Neno nililopewa ni kwamba, Hebu maandishi ya awali ya watu hawa yachapishwe.' Baadhi ya maneno ya mashujaa hao wa imani waliolala yamechapishwa tena katika kitabu hiki. Mifano yao ya namna ambavyo kazi haiwezi kuwekwa kando. Mbinu zao zilikuwa za kibiblia." [47]

Tuna mafundisho ya kweli kutoka kwa Biblia, na tunajua jinsi ya kuyawasilisha. Tuna ujumbe wa afya na tunajua kuuwasilisha pia. Tuna hayo yote na zaidi, ya kuupa ulimwengu unaoangamia. Pia tumepewa maagizo maalum katika Biblia na maandishi ya Ellen White, kuhusu njia mwafaka zinazohitajika katika kuharakisha marejeo ya Bwana wetu. Tumeonywa katika maandishi ya Ellen White, kwamba kuwafanya wachungaji wayasimamie makanisa yaliyopo kutakawisha badala ya kuharakisha marejeo ya Kristo. Tumefahamishwa kwamba kuwaacha wachungaji wahudumie waumini wanoaifahamu kweli hakutaimarisha bali kutadhoofisha kanisa na washiriki wake. *2 Mambo ya Nyakati 20:20* inasema, "Mwaminini Bwana, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; waaminini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa." Biblia inatuonya katika *Waefeso 4:30*, "Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi." Kipaji cha unabii ni kipaji cha kiroho kinachotolewa na Roho. Kipaji hiki kilidhihirika kwa Ellen White, na maandishi yake kwa kanisa ni zao la kipaji hicho. Je, inawezekana kuwa tunamhuzunisha Roho Mtakatifu kwa kukataa kufuata ushauri ulio katika maandishi yake, ambao unatuagiza turejelee mbinu za Kibiblia ambazo sharti zitumike katika kueneza Ujumbe wa Malaika wa Tatu?

Katika siku hizi za mwisho wa historia ya ulimwengu, ninawasihi leo – sote tutubu na tusonge mbele katika kualika ulimwengu unaoangamia na kupotea ukubali wokovu. Tupeleke Ujumbe wa Malaika wa Tatu "wale wakaao juu ya nchi, na kwa kila taifa, na jamaa, na lugha, na watu." Kusiwe na eneo katika divisheni yoyote, yunioni, konfarensi, eneo au misheni, ambayo mwaka baada ya mwaka haijafikishiwa habari njema. Hilo litakuwa kinyume na kila kitu katika mpango wa wokovu, na kukawisha zaidi kutimia kwa Mathayo 24:14, "Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhudu kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."[48] Hebu na watumishi wasioajiriwa na kanisa wawaachilie wachungaji

---

[47] Ellen White, *The Advent Review and Sabbath Herald,* May 25, 1905 page 17.

[48] *Revelation 14:6*

wawe huru kutumika kama wahudumu wa injili kwa wale wanaoangamia gizani. Hebu viongozi wa makanisa wawe na imani na ufafanuzi wa Biblia kuhusu jukumu la wachungaji, nalo walipigie debe kwa sababu ni kweli. Nao wachungaji wakubali kwa urahisi mabadiliko ya jukumu lao, na wajifunze kufanya kazi kwa njia bora zaidi kwa kuwa ndio njia iliyochaguliwa na Mwenyezi Mungu. Hebu tumaini lao liwe ni uaminifu wa Mungu katika kubariki huduma zao na familia zao. Hebu wazee wa makanisa na viongozi wengine wakubali majukumu ambayo Roho Mtakatifu amewapa katika kusimamia masuala ya makanisa yaliyopo. Hebu na kila mshiriki afanye kila awezalo katika kueneza habari njema za Ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa wote wanaohusiana naye. Hebu sote tuipe kazi ya Mungu kipaumbele. Kisha siku moja hivi karibuni, na tena hivi karibuni sana, tutatazama juu na kusema, “Tazama, *huyu* ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja, Na tushangilie na kufurahia wokovu wake.” Isaya 25:9

Katika kutamatisha, nakuletea maneno ya Yohana Mfunuzi, mfungwa katika kisiwa cha Patmo kwa ajlili ya kumtumikia Mungu, ambaye matendo yake yalifuatana naye. Anafunga kitabu cha mwisho cha Biblia kwa maneno yafuatayo katika *Ufunuo 22:20–21*, "Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; naja upesi. Amina; na uje, Bwana Yesu. Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina."